

**UBABEDUME KATIKA MAJIGAMBO YA MIVIGA YA *SHILEMBE* NA  
*MCHEZASILI* WA *MAYO* YA WAISUKHA NCHINI KENYA KWA MTAZAMO  
WA KISEMANTIKI**

**Kibigo Mary Lukamika**

**Tasnifu iliyowasilishwa kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya  
Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha  
Masinde Muliro**

**MEI, 2019**

## UNGAMO NA IDHINISHO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa popote na yeyote kwa minajili ya kutuzwa shahada yoyote au jambo jingine lolote lile. Hairuhusiwi kurudufisha tasnifu nzima au sehemu yake bila idhini ya mtafiti au Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi..... Tarehe.....

**Kibigo Mary Lukamika**

**EDK/H/01/2015**

Tasnifu hii imeidhinishwa kutahiniwa kwa kibali chetu kama wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa kirasmi na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi..... Tarehe.....

**1. Dkt. Susan Chebet Choge.**

Mhadhiri Mwandamizi,  
Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi,  
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia,  
cha Masinde Muliro.

Sahihi..... Tarehe.....

**2. Dkt. Fred Wanjala Simiyu.**

Mhadhiri Mwandamizi,  
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine,  
Za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii.

## **HAKIMILIKI**

Tasnifu hii ni hakimiliki kwa mujibu wa mkataba wa BERNE, kifungu cha sheria cha hakimiliki cha mwaka wa 1999, kulingana na sheria za hataza za kimataifa na kitaifa. Hakuna ruhusa kutolesha au kuchapisha tasnifu hii au sehemu yake ila kwa madhumuni ya utafiti au uhakiki bila idhini ya mwandishi au Mkuu wa Kitivo cha Taaluma ya juu kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

## TABARUKU

Kwa Hayati wapenzi wavyele wangu,  
Musa na Agnetta Kibigo wapendwangu,  
Mlikuwa msaada mwema kwangu,  
Msingi wa maadili na elimu yangu,  
Rabana awalaze pema peponi!

Nawe Hayati mpendwa kakangu,  
Saul Onzere Luyayi mpendwangu,  
Ulinipa ari na mshawasha kakangu,  
Kukienzi Kiswahili ndugu yangu,  
Jalali akulaze pema peponi!

Kwa wewe mpendwa kakangu,  
Elphas Ukiru Luyayi mpendwangu,  
Ahsante kwa himizo kakangu,  
Kuniauni kila nilipobisha hodi,  
Manani akubariki kila kuchao!

Kwa mpendwa mume wangu,  
Laazizi Peter Lisero bwanangu,  
Shukran kwa kuwa msaada wangu,  
Kwa hali na mali mpendwangu,  
Mterehemezi akuneemeshe maishani!

Nanyi wapendwa watano wavumilivu wanangu,  
Mwanambee Wilbroda Ayoti kipenzi changu,  
Gentle Musa na Josephat Gray wapendwangu,  
Flavian Oyolo na Florian Bright wapenzi wangu,  
Rabuka awakirimie mema na fanaka maishani!

## SHUKURANI

Shukrani zangu za awali zimwendee Mola kwa kunitunuku uzima na siha. Ningependa kukishukuru Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro kwa kunisajili na kunipa nafasi ya kuyaendeleza masomo yangu katika kiwango cha Uzamifu. Ningependa kuwashukuru wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro hususan wale walio katika Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, kwa kunisaidia kujenga kazi hii. Shukrani zangu za dharti ziwaendee wasimamizi wangu weledi Dkt. Choge Susan Chebet na Dkt. Wanjala Fred Simiyu kwa uvumilivu, hekima, unyenyekevu na busara kubwa waliyoonyesha katika kunisaidia kuiboresha tasnifu hii hadi upeo wa ufanisi. Kwao nimejifunza si haba na walinikimu kwa mengi. Shukrani za kipekee zimwendee Dkt. Choge kwa kuziratibu programu zetu za Uzamifu na kuhakikisha kuwa, tunapiga hatua Kiisimu na Kifasihi.

Shukrani za dharti ziwaendee wahadhiri wote walionifunza katika kiwango hiki cha Uzamifu kama vile wasimamizi wangu wote wawili pamoja na Dkt. Opende Isaac Nilson wa Chuo Kikuu cha Kisii. Ninawashukuru kwa dharti kwa kuniwekea msingi madhubuti katika taaluma ya utafiti. Hakika, mchango wenu ulikuwa ni wa thamani kubwa kwangu. Mihadhara tuliyokuwa nayo kila mara kule St. Anne's Royal School, Matili, Walia's Kakamega na kwenye bewa la MMUST kule Webuye, ilifungua nadhari zangu na kunipa motisha ya kutia bidii za mchwa ajengaye kichuguu. Ziara za kitaaluma kule nyanjani kwenye makavazi ya Amagoro na pia kuzuru maeneo kama vile ya Hayati Elijah wa Nameme, pamoja na kuwahoji wasailiwa katika jamii ya Wabukusu ziliyapanua mawazo yangu na kunipa mwelekeo mpya kitaaluma, shukrani maalum zimwendee Dkt. Simiyu kwa juhudi hizo zote. Hongereni nyote kwa kunitaalumisha, kazi hii ni tunu kwenu.

Ninakupeni ahsante wazamifu wenzangu ambao tulipiga mbizi nao na kutiana shime; Bi Nyamete, Bi Musailo, Bi Mung'ahu na Bw. Andele. Jalali awabariki sana kwa mchango wenu wa busara kiakademia. Ninamshukuru Bw. Ben Khayumbi aliyepiga chapa kazi hii na kuiboresha katika kila hatua. Ninawapa pongezi wazazi wangu wapenzi; Hayati Bw. Zakayo Musa Kibigo na Hayati Bi Agnetta Kasaya Kibigo kwa kujitolea kwa hali na mali na kuhakikisha kuwa nimepata kisomo. Kaka zangu wapendwa Bw. Elphas Luyayi na Hayati Mwalimu Mkuu Bw. Saul Luyayi, dada zangu wapenzi Bi Priscilla Imali na Bi Esther Nyangasi. Ninampongeza mavyaa wangu mpendwa mama Hellen Oranga kwa kuniombea mema, ahsanteni kwa kunionyesha mwanga wa masomo.

Shukrani zimwendee mume wangu mpendwa Bw. Peter Lisero aliyeyafadhili masomo yangu, akanipa utulivu na kunihimiza nilipokaribia kutamauka. Ninawapongeza wapenzi wanetu watano; Ayoti, Musa, Gray, Fla na Flo ambao kama si kukubali kupuuzwa ili kazi hii iendelee basi huenda nisingeifikia hatua hii katika mchakato huo. Shukrani kwa watafitiwa kutoka katika jamii ya Waisukha; Bw. Anzumbu, Bi Beverline, Bw. Shitekha, Bi. Kakhai, Bw. Khiyanjila na Bw. Machoni miongoni mwa wengine. Ingawa siwezi kuwataja wote kila mmoja kwa jina, kwa unyenyekevu na taadhima ningependa kuutambua mchango wao na kumwomba Manani awakirimie baraka tele.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ubabedume miongoni mwa Waisukha jinsi unavyodhihirika katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*, vipashio vya lugha vinavyosheheni ubabedume katika majigambo hayo vilidondolewa na kuchambuliwa kwa mtazamo wa Kisemantiki. Ili kutimiza lengo hili, utafiti uliongozwa na madhumuni haya: Kubainisha vipashio vya lugha; nomino na vishazi na vitenzi katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* vinavyodhihirisha ubabedume miongoni mwa Waisukha, kuhakiki tamathali za usemi zinavyosheheni ubabedume kwa mtazamo wa Kisemantiki na kuchunguza nafasi ya lugha, historia na itikadi za Waisukha katika kujenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume wanapopiganisha fahali. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (UCHAMAWADI) na Nadharia ya Uwezo-Uume. Baadhi ya wachangiaji mashuhuri katika nadharia ya UCHAMAWADI ni wataalam kama vile; Gee (1990), Fairclough (1992), Teun Van Dijk (1993) na Wodak (2001). Nadharia hii iliwekwa msingi na kazi mbalimbali za wataalam hawa. Nadharia hii hutambua uamilifu wa lugha katika jamii. Mihimili yake mikuu ni; uhakiki, uwezo au mamlaka, historia na itikadi. Nadharia ya Uwezo-Uume iliasisiwa na Robert Bly (Well & Holland, 2001) na kuendelezwa na Izugbara (2005). Inahusisha mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii. Baadhi ya mihimili yake ni; itikadi za kijamii ambazo huongoza fikra, mitazamo na mielekeo ya wanajamii kuhusu hali mbalimbali za kijamii. Nadharia mbili zilitumiwa ili kuchangiana. Utafiti huu ulifanywa katika eneo Bunge la Shinyalu, Kaunti ya Kakamega. Watafitiwa walikuwa fanani na washiriki katika sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Usampulishaji ulifanyika kwa kutumia aina tatu za usampulishaji. Utafiti ulilenga kukusanya majigambo ishirini na saba kimaksudi kutegemea nasaba ishirini na saba za Waisukha. Hata hivyo, majigambo kumi na sita yalikusanywa kwa kutumia uteuzi wa kimapokezano. Uteuzi wa kimaksudi ulitumiwa kuteua nasaba saba zilizo na majigambo maarufu na uteuzi wa kinasibu ukatumiwa kuchagua majigambo tisa. Jumla ya majigambo yaliyotumiwa yalikuwa kumi na sita. Mbinu za Uchunzaji-Shiriki na Kiethnografia zilitumiwa na zilijumuisha kuishi na watafitiwa, kushiriki, kushuhudia sherehe hizo pamoja na kuwahoji ili kukusanya majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Data iliwasilishwa na kuchanganuliwa kupitia maelezo ya kifafanuzi na mifano, picha, vielelezo na filamu halisi. Matokeo yamebainisha kuwa lugha ni kipengele muhimu cha jamii ya Waisukha kwa vile humsawiri mwanamume Mwisukha kama aliye na mamlaka zaidi ya mwanamke. Hali hii itafaidi jinsia ya kike kwa vile wanaume watayashughulikia majukumu yao kikamilifu katika jamii. Utafiti umebainisha kuwa uwezo wa mwanamume umetamalaki katika majigambo ya Waisukha yaliyosheheni vipengele vya lugha. Unatarajiwa kuupanua uwanja wa Fasihi Simulizi na Isimu kwa kulikuza suala la kuchanganua majigambo, kipera cha Fasihi Simulizi kwa mtazamo wa Kisemantiki kwa kuhakiki vipashio vya lugha. Utafiti unatazamia kutoa mchango katika kuelewa umuhimu wa *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* pamoja na mila, desturi na itikadi za Waisukha zinazowasilishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa masimulizi ya Mwafrika. Hali inayoniua kuwachochea wasomi wa Fasihi Simulizi na Isimu wa baadaye kuchanganua masuala ya Fasihi Simulizi kwa kina zaidi kwa kuangazia vipashio vya lugha na vipengele vya kiisimu na kuweza kuzua mwingilianotaaluma.

## ABSTRACT

The purpose of this study was to investigate masculinity in the language used in praise poetry in the performance of the ritual of *Shilembe* and *Mayo* indigineous sport among the Isukha community by examining specific aspects of language basing on Semantic approach. In order to accomplish this objective, the study was guided by the following specific objectives: to examine the language aspects; nouns, phrases and verbs in the Isukha praise poetry and how they create, portray and maintain hegemonic masculinities, to examine the stylistic devices in Isukha praise poetry basing on the Semantic approach and to identify how language, history, ideology and power relations play a vital role in creating and maintaining hegemonic masculinities in Isukha community during bull fighting. The study was guided by two theories namely: Critical Discourse Analysis and Hegemonic Masculinity. Critical Discourse Analysis-CDA was propounded by the following people, Teun Van Dijk, Fairclough & Wodak in 1990. It is grounded in different works of these proponents. It identifies the use of language in the society. Its main tenets are; examining, power relations, history and ideology. Hegemonic Masculinity Theory was propounded by Robert Bky (Well & Holland, 2001) and continued by Izugbara (2005). It involves the relationships between women and men in the society. Some of its tenets include; Community ideologies that guide the mind and their perspectives on different issues of the community. The two theories were adopted because they complement one another. The research was conducted in Shinyalu Constituency in Kakamega County. The researchers were the artists and performers in the ritual of *Shilembe* and *Mchezasili* of *Mayo*. The study aimed at collecting twenty seven praise poems basing on the twenty seven clans of the Isukha community. However, Snowball sampling procedure gave us sixteen praise poems and purposive sampling was adopted in sampling seven clans that are famous in praise poetry. Random sampling was adopted to collect nine praise poems. The total number of praise poems used were sixteen. Ethnomethodological approach was used, included staying with the Isukha community, participant-observation, use of interviews, discussions with informants. Observation was also used to collect the language used in praise poetry during the *Shilembe* ritual and the *Mayo* indigineous sport among the Isukha community. The findings were presented using descriptions, pictures and a documentary film. The results of this research have shown that language is an important aspect of community as it exalts and portrays an Isukha man as one who has authority over the female gender. This will enable the male gender to take up its position fully and execute its duties appropriately in the society. The research has revealed supremacy remains dominant in gender relations. It is hoped that this research will expand on the understanding of the nature of the field of literature and linguistics so as to enhance the idea of analyzing praise poetry which is a genre of Oral Literature using Semantic approach by examining the language aspects. The research has contributed to the understanding of the *Shilembe* ritual and *Mchezasili* of *Mayo* during bull-fighting among the Isukha community as well as the reality of African Oral Literature. This will motivate the future Oral Literature and Linguistic scholars to analyse Oral Literature in depth basing on Language and Linguistic aspects and hence bring about interdisciplinary approach.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO NA IDHINISHO .....</b>	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>iv</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vi</b>
<b>ORODHA YA MAJEDWALI .....</b>	<b>xiii</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa utafiti .....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	6
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	7
1.4 Maswali ya Utafiti.....	8
1.5 Sababu ya Uteuzi wa Mada ya Utafiti.....	8
1.6 Upeo wa Utafiti .....	10
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	10
1.8 Misingi ya Kinadharia.....	11
1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi .....	12
1.8.2 Nadharia ya Uwezo-Uume .....	21
1.9 Hitimisho.....	25



1.10 Maelezo ya Istilahi.....	26
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>29</b>
<b>UHAKIKI WA MAANDISHI.....</b>	<b>29</b>
2.1 Utangulizi .....	29
2.2 Dhana ya Ubabedume .....	29
2.3 Maana ya Majigambo.....	36
2.4 Tafiti zilizofanywa kuhusu ubabedume .....	41
2.5 Tafiti zilizofanywa kuhusu majigambo, miviga na taaluma nyingine .....	45
2.6 Tafiti zilizofanywa kuhusu Waisukha.....	50
2.7 Tafiti kuhusu kipengele cha kiisimu: kisemantiki.....	53
2.8 Tafiti zilizofanywa kuhusu nadharia za utafiti huu .....	56
2.8.1 Nadharia ya Uwezo-Uume .....	56
2.8.2 Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi .....	58
2.10 Hitimisho.....	68
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>70</b>
<b>MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI .....</b>	<b>70</b>
3.1 Utangulizi .....	70
3.2 Muundo wa Utafiti .....	70
3.3 Mahali pa Utafiti .....	71
3.4. Umma Lengwa .....	72
3.5 Uteuzi wa Sampuli.....	72

3.5.1 Uteuzi wa Wasailiwa .....	73
3.5.2 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli .....	73
3.6 Mbinu za Kukusanya Data .....	76
3.6.1 Njia za Ukusanyaji wa Data .....	76
3.6.1.1 Vifaa vya Utafiti.....	76
3.6.1.1.1 Mahojiano.....	76
3.6.1.1.2 Uhakiki wa yaliyomo.....	76
3.6.1.1.3 Utazamaji naUchunzaji-Shiriki .....	77
3.7 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data.....	79
3.10 Majaribio ya Vifaa vya kukusanya data .....	84
3.11 Uwasilishaji wa Matokeo .....	85
3.12 Maadili ya Utafiti .....	86
3.13 Changamoto za utafiti .....	87
3.14 Hitimisho.....	90
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>91</b>
<b>UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO .....</b>	<b>91</b>
4.1. Utangulizi.....	91
4.2 Nomino, vishazi na vitenzi vinavyosawiri ubabedume.....	92
4.3 Vipashio vya Lugha vinavyosheneni Ubabedume kwa mtazamo wa Kisemantiki. .....	101
4.2.1.1 Majazi na Semantiki .....	107
4.2.1.2 Tashbihi na Semantiki.....	109

4.2.1.3 Chuku na Semantiki .....	112
4.2.1. 4 Jazanda na Semantiki .....	114
4.3 Lugha, historia na itikadi zinavyosawiri ubabedume katika majigambo .....	116
4.4 Sifa angama za ubabedume .....	117
4.4.1 Ushujaa .....	117
4.4.2 Mvumilivu .....	118
4.5 Hitimisho .....	121
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>122</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>122</b>
5.1 Muhtasari wa Tasnifu .....	122
5.2 Muhtasari wa Matokeo .....	123
5.2.1 Namna nomino, vishazi na vitenzi vinadhihirisha ubabedume .....	123
5.2.2 Tamathali za Usemi zinazosawiri Ubabedume kwa mtazamo wa kisemantiki .	124
5.2.3 Nafasi ya lugha, Historia na Itikadi za Waisukha katika kujenga Ubabedume .	125
5.4 Mapendekezo .....	130
5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi .....	132
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>133</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>148</b>
<b>KIAMBATISHO A: RATIBA YA UTAZAMAJI NA UCHUNGUZI- SHIRIKI...</b>	<b>148</b>
<b>KIAMBATISHO B: MAJIGAMBO YALIYOKUSANYWA NYANJANI NA KUCHANGANULIWA .....</b>	<b>149</b>
<b>KIAMBATISHO C: ORODHA YA WAHOJIWA .....</b>	<b>153</b>

<b>KIAMBATISHO E: MWONGOZO WA MAHOJIANO NA MIJADALA HURU</b>	<b>160</b>
<b>KIAMBATISHO F: RAMANI YA SEHEMU YA UTAFITI.....</b>	<b>161</b>
<b>KIAMBATISHO G: KIBALI KUTOKA KWA MKURUGENZI WA SHAHADA ZA JUU, CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA CHA MASINDE MULIRO.....</b>	<b>162</b>
<b>KIAMBATISHO H: IDHINI KUTOKA KWA KAUNTI YA KAKAMEGA .....</b>	<b>163</b>
<b>KIAMBATISHO I: IDHINI KUTOKA KWA TUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA NA UKARABATI (KENYA)-NACOSTI.....</b>	<b>164</b>
<b>KIAMBATISHO J: IDHINI KUTOKA KWA TUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA (KENYA).....</b>	<b>164</b>

## **ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 3.1 Sampuli Teule .....	75
Jedwali 4.1 Nomino zinazosawiri Ubabedume katika Majigambo .....	98
Jedwali 4.2 Vishazi vinavyosawiri Ubabedume katika Majigambo .....	101
Jedwali 4.4 Tamathali za Usemi zinasawiri Ubabedume katika Majigambo .....	116
Jedwali 4.5 Lugha, Historia na Itikadi zinavyosawiri Ubabedume .....	120

## MAELEZO YA VIFUPISHO NA AKRONIMU

<b>Kiamb:</b>	Kiambatisho
<b>Mchezasili:</b>	Huu ni mchezo asilia wa Waisukha wa kupiganisha fahali.  Katika kazi hii umerejelewa kama ‘ <i>Mchezasili wa Mayo</i> ’
<b>MHOJ:</b>	Mhojiwa
<b>MMUST:</b>	Masinde Muliro University of Science and Technology
<b>NACOSTI:</b>	National Commission for Science, Technology and Innovation
<b>NARC:</b>	National Alliance Rainbow Coalition
<b>P:</b>	Picha
<b>UCHAMAWADI:</b>	Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi
<b>Taz:</b>	Tazama
<b>TUKI:</b>	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
<b>TY:</b>	Tafsiri Yangu

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.0 Utangulizi**

Utafiti huu unachunguza ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* miongoni mwa Waisukha nchini Kenya kwa mtazamo wa Kisemantiki. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za uteuzi wa mada, upeo wa utafiti na umuhimu wa utafiti. Aidha, imeangazia misingi ya nadharia mbili zilizotumika katika utafiti huu. Usuli wa mada umegusia asili ya dhana ya upiganishaji fahali, historia ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* mintaarafu ubabedume. Mapitio ya maandishi yameonyesha mwanya uliopo katika utafiti wa awali na umuhimu wa kulishughulikia suala hili katika utafiti huu. Madhumuni ya utafiti huu yamewekwa wazi kwa mujibu wa kuonyesha vipengele vilivyoshughulikiwa kuufanikisha utafiti huu.

Maswali ya utafiti yametoa msingi na mwelekeo wa kuchunguza ubabedume katika majigambo ya Waisukha. Upeo wa utafiti umeonyesha sehemu ambayo utafiti huu unajikita au mipaka yake. Nadharia mbili zimetumika ili kuoanisha masuala ya Fasihi na Isimu. Sura hii imetoa mwelekeo wa utafiti huu.

#### **1.1 Usuli wa utafiti**

Huwezi kushughulikia masuala ya *Shilembe* na *Mayo* bila kuyahusisha na upiganishaji wa fahali. Dhana ya kupiganisha fahali ina historia ndefu na mkufu huu tunaweza kuufuatilia kuanzia kule Mesopotamia ambako fahali waliabudiwa na kutolewa kama

sadaka kwa miungu. Rekodi hii ya kwanza ya upiganishaji fahali inaelezea kisa ambapo Gilgamesh na Enkidu walipigana na wakamuua fahali wa mbinguni. Upiganishaji fahali ulihusishwa na Wagiriki na visakale vyao pamoja na visaviini. Vilevile, ulihusishwa na Warumi ambapo sherehe za binadamu na wanyama zilifanywa kama mashindano. Kule Uhispania, ‘Toreros’ ambaye ni fahali anayepigana hufananishwa na mashabiki wa mpira, ambao hufadhiliwa na wafadhili na kuonekana katika vyombo vya habari (Hemingway 1932). Katika karne ya kumi na tisa huko Ufaransa, wanajamii walianzisha upiganishaji fahali kwa njia yao ya kipekee. Michezo hii ilienea na kuwa katika mabara ya Afrika, Uropa na Asia katika enzi za Warumi (Kabaji 2008).

Nchini Tanzania, upiganishaji fahali uliasisiwa na Wareno. Walianzisha sherehe hii kwa Waunguja na Wapemba wa visiwa hivi. Sherehe hii ilijulikana kama *mchezo wa ng’ombe*. Fahali aliweza kushikwa kwa kamba na hakufaa kuumizwa wala kuuawa baada ya vita.

Magharibi mwa Kenya, fahali hupigana na fahali mwenzake kwa kutumia pembe. Katika jamii ya Wawanga wanaotoka Mumias, sherehe ya kupiganisha fahali hujulikana kama *Eshiremba* na hufanywa kwa njia ya kipekee kwa vile baada ya mazishi, fahali huwa wanaletwa kwa ajili ya kulitandaza kaburi. Watu wa jamii hii hupiganisha fahali kwa heshima ya marehemu mwanamume mzee aliyeheshimiwa kwa mchango wake mkuu katika jamii, huambatana na mwigo au maigizo ya vita vya mikuki.

Kabaji (2005) anaelezea kuhusu uumbaji wa masuala ya kijinsia kwa kutumia mfano wa jamii ya Wamaragoli. Anahoji kuwa sherehe ya *Ekeremba* ni muhimu kwa vile



hufanyiwa wanaume mashujaa katika jamii hii. Kulingana na mpito wa wakati, sherehe hii imefifia kwa ajili ya uchumi mgumu na dini za kigeni. *Shilembe* katika jamii ya Wanyore kutoka maeneo bunge ya Emuhaya na Luanda, huitwa *Shilemba* na huhusisha fahali na uharibifu wa mali pamoja na migomba ya ndizi hasa siku ya mazishi. Uharibifu huo huashiria kupotea kwa mwanamume mashuhuri katika jamii ya Wanyore. Baadaye wahusika huelekea kaburini na kulitandaza kaburi la shujaa huyo. Sifa ya kulitandaza kaburi imeenea katika baadhi ya jamii kwa vile inamwuhusisha mwendazake na miungu yaani aliyeaga huandaliwa njia yake ya kuingia katika dunia ya pili (Alembi 2002).

Katika jamii ya Waisukha walio katika eneo bunge la Shinyalu katika kaunti ya Kakamega, kuna sherehe maalum zijulikanazo kama *Shilembe* na *Mayo*. Sherehe ya *Shilembe* ni sherehe ya kipekee katika jamii ya Waisukha inayojikita katika miviga na huhusisha kupiganisha fahali kaburini mwa mwanamume aliyepata ushujaa kwa kumuua adui aliyekuwa Mzungu au Mnandi aliyepora ng'ombe wao. Hata hivyo, kuna mabadiliko mengi katika jamii hii yanayotokana na dini, mitazamo, vigezo vya kishujaa vilivyobadilika kwa vile Mzungu alirudi kwao na Mnandi haporu ng'ombe tena. Sherehe hii imetoka kwa wafu kwa kiasi fulani na si kama ilivyokuwa hapo awali. Kwa upande mwingine, *Mayo* ndiyo sherehe inayofanyika kila mara hasa siku za Sikukuu kama vile ya Mashujaa na pia hufanyika kila Jumamosi kama sanaa za maonyesho. *Mayo* ni sherehe ya *Shilembe* inayofanywa kisanaa. *Mayo* huhusisha mchezo wa kiasili wa Waisukha wa kupiganisha fahali. Utafiti huu ulihusisha miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* katika jamii ya Waisukha kwa sababu sherehe za *Shilembe* hazijitokezi sana ila shujaa

anapoaga dunia bali sherehe za *Mayo* huwepo kila Jumamosi na siku za sikuukuu nchini Kenya.

Waisukha ni mojawapo ya makabila ya Wabantu wanaoishi Magharibi mwa Kenya. Makao yao makuu ni katika Kaunti ya Kakamega, eneo bunge la Shinyalu. Jamii hii ni mojawapo ya makabila ya Waluhya. Imegawika katika takriban nasaba ishirini na saba. Orodha ya koo hizo ni kama zifuatazo; Vayokha, Vitsende, Varuli, Vakhaiwa, Vamilonje, Vamakhaya, Vimalia, Vichina, Vimahalia, Vashitaho, Vakhulunya, Vakusi, Vakhondi, Varimbuli, Vasulwa, Vaterema, Vasikhovu, Vakhombwa, Vatula, Vashilita, Valila, Vasakala, Vashilukha, Vashimutu, Vateheli, Vatsunga na Vasalwa (Were 1976). Nasaba hizi ni muhimu katika jamii hii na pia katika utafiti huu kwa sababu Waisukha hujigamba kutegemea koo zao.

Hapo awali, sherehe ya *Shilembe* ilikuwa ikifanyiwa wanaume shujaa katika jamii hii walioaga dunia hususan baada ya Vita vya Kwanza na Pili vya Dunia au MAUMAU. Fahali wawili waliokuwa wakitumiwa katika sherehe hizi walikuwa wakiandaliwa mapema kwa kuzinoa pembe zao ili ziweze kuitekeleza kazi ya kupigana kaburini kikamilifu. Dhana ya kunoa pembe inaelezwa na Kabaji (2008) kuwa iliashiria ubabe kwa vile pembe hizo zilipewa fursa ya kusimika kuashiria kule kuwa tayari kwa dhakari kufanya tendo la ngono. Fahali walipopigana walifaa kwenda haja ndogo kaburini ili kuonyesha ile hali ya mwanamume kuwa na uwezo wa kumzalisha mkewe watoto wengi. Ng'ombe hao pia walipewa fursa ya kuutandaza mchanga uliokuwa umewekwa kama kilima kaburini katika sehemu nyingi za boma la mwendazake ili kuzituliza roho za watu waliouawa na shujaa huyo aliyeaga. Iliaminika kuwa fahali hao walifanya hivyo ili

kumuandalia aliyeaga nafasi nzuri kule alikokuwa akielekea kwa mizimu (Anzumbu, Kakhai na Khiyanjila 2018).

Kutokana na mpito wa wakati, sherehe hii ya miviga ya *Shilembe* bado ipo na mtafiti alipata fursa ya kuzihudhuria sherehe tatu wakati mashujaa kutoka katika jamii ya Waisukha walipoaga dunia (Tazama kiambatisho D). Sherehe hizo zilifuata hatua zote za mchakato huo siku moja baada ya mazishi. Miviga ya *Shilembe* ya kwanza ilifanyiwa mwenzake Meja Nandi kutoka katika nasaba ya Vasalwa, Mulanda mnamo tarehe 5/9/2018 (Taz. Kiamb. D, P8). Sherehe ya pili ilifanyiwa mwenzake Elisha Shitamba kutoka katika nasaba ya Vashitaho, sehemu ya Uwanja Ndege tarehe 3/10/2018 (Taz. Kiamb. D, P10). Sherehe ya tatu ilifanyiwa katika boma la mwenzake Mukabwa Lwoyelo kutoka katika nasaba ya Vamilonje, sehemu ya Mulanda tarehe 4/1/2019 (Taz. Kiamb. D, P9). Fahali waliletwa kaburini pa wenzao hao na kikundi cha wanajamii na fanani na washiriki wengine kutoka katika jamii ya Waidakho wanaoienzi sherehe hii kama vile Mheshimiwa Bonnie Khalwale miongoni mwa wanajamii wengine na mashabiki mashuhuri walihudhuria.

Miviga ya *Shilembe* imeendelea kujinyumbua na kubadilika kwa vile mashujaa wengi waliokuwa na ushujaa wa kuwaua maadui kama Wazungu na Wanandi, hawaruhusiwi na sheria kwa hivyo sherehe hiyo imebadilika na mashujaa sasa ni fahali. Ingawa sherehe hii bado ipo lakini siku hizi uporaji wa ng'ombe uliohusishwa na jamii ya Wanandi haupo tena. Sherehe hii sasa inajulikana kama *Mchezasili wa Mayo* na inafanywa kama sanaa za maonyesho siku za wikendi au kila kunapokuwa na sikukuu yoyote nchini Kenya. Fahali

hupiganishwa na fursa hutolewa kwa watu wa nasaba mbalimbali katika jamii hii kujigamba.

Tafiti za awali zinaonyesha kuwa sherehe za kupiganisha fahali hufanywa katika jamii mbalimbali kama mbinu ya kutoa burudani na shughuli ya mazishi tu. Hata hivyo, katika majigambo ya Waisukha yanayoghaniwa na fanani wajigambi na watambaji wakati wa miviga ya *Shilembe na Mchezasili wa Mayo*, huwa kuna jumbe ambazo hubebwa na majigambo hayo. Vipashio vya lugha vinavyobeba ubabedume hudhihirika. Majina ya fahali, vishazi na vitenzi hutumika katika majigambo hayo na huwa yamesheheni sifa anuwai za ubabedume. Haya ndiyo yaliyomchochea mtafiti kuchunguza aina ya lugha inayotumiwa na wasanii katika kujigamba kwa mtazamo wa Kisemantiki. Uhakiki wa maandishi umetoa mwanya kuwa sherehe hizi katika jamii nyingi hazijikiti katika kufafanua jumbe zilizo katika majigambo hayo. Jambo hili ndilo lililomsukuma mtafiti kuchunguza ubabedume unavyosawiriwa katika majigambo ya miviga ya *Shilembe na Mchezasili wa Mayo* miongoni mwa Waisukha.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Utafiti huu unachunguza masuala ya kisemantiki katika majigambo ya miviga ya *Shilembe na Mchezasili wa Mayo* jinsi inavyodhihirika katika vipashio vya lugha. Miviga ya sherehe za *Shilembe na Mchezasili wa Mayo* zimekuwa sehemu za utamaduni wa Waisukha katika kutimiza majukumu tofautitofauti ya kijamii kama vile mazishi na burudani. Waisukha wengi wameshiriki sherehe hizi kama burudani tu ya kucheza na kughani majigambo pamoja na kushindana huku wakicheza ngoma ya 'Isukuti'. Ingawa majigambo hayo yanatumika kama burudani tu, husheheni jumbe fulani tofautitofauti

kwa wanajamii. Mojawapo ya jumbe hizo zinazowasilishwa kwa wanajamii ni suala la ubabedume linalodhihirika katika sherehe hizi kupitia kwa majigambo yanayotambwa wakati huo. Majigambo hayo yanasheheni ujumbe huu kupitia vipengele mbalimbali vya lugha kama vile nomino, vishazi na vitenzi. Hali hii ndiyo iliyomchochea mtafiti kuchunguza jinsi ubabedume unavyosawiriwa katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha. Haya yalitekelezwa kwa kuvichunguza vipashio mbalimbali vya lugha kwa kutumia mtazamo wa Kisemantiki. Utafiti ulilenga kuhakiki na kupambanua jinsi vipashio vya lugha katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha husawiri ubabedume. Ili kufikia lengo hili, utafiti ulidhihirisha wazi namna vipashio vya lugha hususan nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* husawiri ubabedume, ulihakiki tamathali za usemi zinavyosheheni ubabedume kwa mtazamo wa kisemantiki na kuchunguza nafasi ya lugha, historia na itikadi za Waisukha katika kujenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume wanapopiganisha fahali.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza ubabedume katika jamii ya Waisukha jinsi unavyodhihirika katika vipashio vya lugha vinavyosheheni majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Madhumuni mahsusi yalikuwa:

- i. Kubainisha namna vipashio vya lugha hususan nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* vinavyodhihirisha ubabedume.

- ii. Kuhakiki tamathali za semi zinazosheheni ubabedume kwa mtazamo wa Kisemantiki.
- iii. Kuchunguza nafasi ya lugha, historia na itikadi za Waisukha katika kujenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume wanapopiganisha fahali.

#### **1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Je, ni kwa namna gani vipashio vya lugha hususan nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* ya Waisukha hudhihirisha ubabedume?
- ii. Je, ni tamathali gani za semi zinazosheheni ubabedume kwa mtazamo wa Kisemantiki?
- iii. Je, lugha, historia na itikadi za kijamii zina umuhimu gani katika kuchipua, kujenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume katika majigambo ya Waisukha wanapopiganisha fahali?

#### **1.5 Sababu ya Uteuzi wa Mada ya Utafiti**

Majigambo ni mojawapo ya vipera vya maigizo ya Fasihi Simulizi ambayo yanadhihirisha utata na uchangamano kutokana na fasili mbalimbali zinazotolewa kueleza dhana yake kama ilivyo dhana ya kimsingi ambayo ni Fasihi Simulizi kwa vile hutegemea fanani katika jamii husika. (Wanjala, 2011 na Ndumbaro, 2013). Hivyo, ni vigumu kueleza mipaka ya majigambo kimaumbo kwa vile hujifaragua na kujinyambua kimaumbo. Finnegan (2012) anasema kuwa Fasihi Simulizi hutegemea msanii ambaye huiumba kwa maneno katika tukio maalum. Hoja muhimu katika mawazo ya Finnegan

ambayo iliuchochea utafiti huu ni kwamba ubunifu wa Fasihi Simulizi hutegemea tukio maalum ambalo katika utafiti huu ni miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* wakati wa kupiganisha fahali. Sababu ya kwanza iliyopelekea uteuzi wa mada ya utafiti ni;

- i. Upekee wa majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* katika jamii ya Waisukha.
- ii. Suala la utafiti huu lilichaguliwa kwa misingi kuwa, licha ya kuwepo kwa makongamano na utafiti kuhusu jinsia na lugha katika nchi za Magharibi, tafiti chache sana zimefanywa Barani Afrika, hususan katika jamii ya Waisukha katika muktadha huu.
- iii. Mapigano ya fahali katika jamii hutazamwa tu na kupuuzwa, kwa hivyo, tuliufanya utafiti huu kwa sababu tulitaka kuelewa dhima ya sherehe hii ya Waisukha.
- iv. Tuliufanya utafiti huu kwa minajili ya kufuzu na kupata shahada ya Uzamifu.
- v. Majigambo ni utanzu muhimu wa Fasihi Simulizi ya jamii ya Waisukha ambayo hutumiwa na jinsia zote. Kwa hivyo, iliyo muhimu katika majigambo yao ni dhana ya lugha ambacho ni kitambulisho cha wanajamii hawa kwani husheheni na kuhifadhi historia yao.
- vi. Wataalam mbalimbali kama vile Mwita (1997); Wanjala (2011, 2015), Matinde (2015), Mung'ahu na Kobia (2016) wameshughulikia majigambo na miviga katika Fasihi Simulizi ingawa wachache wamehusisha miviga na ubabedume kwa kutumia mtazamo wa Kisemantiki. Ni muhimu basi kuchunguza majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha ili kudadavua matumizi yake hususan dhima yake kwa mwanamume Mwisukha.

vii. Utafiti huu ulitiwa mshawasha na ukweli kuwa suala la ubabedume katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika halijatafitiwa kwa kina (Matinde 2015). Tasnifu hii ni rejea muhimu katika usomi na vilevile ufundishaji wa Isimu, Fasihi Simulizi, Isimu-Jamii, Isimu-Amali na Uchanganuzi wa matini hususan katika harakati ya kubainisha namna jamii husetiri utamaduni, itikadi, mila na desturi yao katika matini au usemi katika miktadha mahsusi ya kijamii.

### **1.6 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulishughulikia uchanganuzi wa ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha. Utafiti ulifanywa katika eneo bunge la Shinyalu katika kaunti ya Kakamega na sehemu maalum zilizotafitiwa ni; wadi za Muranda, Uwanja Ndege, Ilala, Museno, Khayega na Shinyalu. Uchanganuzi ulihusisha masimulizi na utendaji wa fanani katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* kutoka katika jamii ya Waisukha kwa kuchunguza vipashio vya lugha Kisemantiki. Utafiti huu ulikuwa wa Fasihi, utanzu wa Fasihi Simulizi unaojulikana kama maigizo, vipera vya miviga na majigambo. Mikakati iliyotumiwa kufasili data hii ilikuwa ni Isimu katika ngazi ya Kisemantiki na vilevile uchunguzi wa vipashio vya lugha hususan nomino, vishazi na vitenzi.

### **1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ni muhimu kwani ulisaidia kukusanya majigambo kumi na sita ya Waisukha kutokana na masimulizi ya fanani ili kuweza kurithisha kwa vizazi vijavyo vya jamii hii. Utafiti ulichochea na ukweli kuwa suala la ubabedume katika fasihi simulizi ni muhimu. Suala la upiganishaji fahali halijathaminiwa na baadhi ya wataalam. Matokeo



ya utafiti huu yatakuwa tunu muhimu katika tahakiki zilizoko kuhusu ubabedume kwa kuuweka wazi utamaduni wa Waisukha ambao haujawekwa wazi kimaandishi na wataalam wengi. Utafiti huu ulikusanya majigambo kumi na sita; kwa hivyo utafiti huu unatoa mchango katika hali ya kuweza kuhifadhi mojawapo ya tanzu za Fasihi ya Waisukha kwenye kiwango cha othografia au kimaandishi. Ni muhimu kutaja kuwa majigambo hutoa mafunzo muhimu kwa wanajamii kupitia kwa lugha hususan mila, itikadi, desturi, historia, utamaduni miongoni mwa mafunzo mengine.

Matokeo ya utafiti huu ni rejeleo muhimu kwa vile yatatumika kama malighafi mwafaka kuhusu tahakiki zilizoko zinazojikita katika ubabedume katika Fasihi ya Kiafrika. Hali hii itakuwa muhimu kwa sababu lugha ya mtu ni kitambulisho chake kwa hivyo, haya yataweza kudhihirisha bayana namna ambavyo mila, itikadi, utamaduni na historia ya Waisukha hujenga, hushamirisha na kuhalalisha mahusiano ya ubabedume kupitia kwa majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*.

Utafiti huu unatazamiwa kuwafaidi wanafunzi wa Kiswahili katika shule, vyuo na ndaki mbalimbali.

### **1.8 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti uliongozwa na nadharia mbili zilizojumuisha nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (Fairclough na Wodak 1990) na nadharia ya Uwezo-Uume (Izugbara 2005). Utafiti huu ulitumia nadharia mbili kwa sababu kulikuwa na haja ya kuonisha taaluma ya Isimu na Fasihi Simulizi kwa kuzingatia vipengele vya lugha ambavyo ni nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo ya Waisukha. Aidha, uhakiki wa tamathali za usemi katika majigambo hayo kwa mtazamo wa kisemantiki ulitulazimu kutumia nadharia zaidi

ya moja. Kimatumizi, nadharia ya Uwezo-Uume ina mihimili ambayo kwa mujibu wa utafiti huu inachangiana na kukamilishana na mielekeo ya nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi kama ilivyodhihirika nyanjani.

### **1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi**

Nadharia ya kwanza iliyotumika katika utafiti huu imekitwa katika nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ambayo pia kwa ufupisho ni UCHAMAWADI (Choge, 2018). Dhana ya diskosi imetumiwa na wataalam mbalimbali kurejelea maana tofauti tofauti. Nadharia hii iliasisiwa mnamo mwaka wa 1990 na Teun Van Dijk, Norman Fairclough, Theo Van Leeuwen na Ruth Wodak. Uwanja ambao unashughulikiwa na nadharia hii unakua kwa kasi sana hususan katika uchunguzi wa lugha. Nadharia hii hutazama usemi kama aina ya kaida au desturi za kijamii (Fairclough na Wodak, 1997, uk. 258). Miongoni mwa wachangiaji mashuhuri wa nadharia hii ni pamoja na Fairclough (1992, 1995). Gee (1990), Teun van Dijk (1993, 1999) na Wodak (2001).

UCHAMAWADI si nadharia moja bali huchukuliwa kama njia iliyo na mielekeo au mitazamo tofautitofauti na mikakati tofauti ya kuchunguza uhusiano baina ya matumizi ya lugha na muktadha wa jamii. Mihimili ambayo hurejelewa zaidi ni ile iliyo na mawazo ya Van Dijk, Fairclough na Wodak (1997). Hata hivyo, mawazo na maoni ya wataalam wengine yamerejelewa ili kuchangia yale ya wataalam hawa. UCHAMAWADI ni nadharia ambayo huangazia matatizo ya kijamii. Nadharia hii haiangazii tu lugha na matumizi yake bali pia humulika sifa za kiisimu za kijamii na kitamaduni hususan dhana ya ukosefu wa usawa katika jamii na ubaguzi wa rangi miongoni mwa masuala mengine

(Van Dijk, 1993). Huweza kuchanganua matini au usemi kwa kina ili kuweza kubainisha mahusiano ya kimamlaka ambayo huzua matatizo ya kijamii. Uhusiano wa kimamlaka hutokana na usemi, UCHAMAWADI hueleza uhusiano wa kijamii uliopo na namna uhusiano huo hujitokeza katika usemi. Kwa vile usemi huhusisha jamii na utamaduni, hali hii ina maana kwamba matumizi ya lugha huchangia mabadiliko katika jamii na utamaduni wa jamii husika pamoja na uhusiano wa kimamlaka. Usemi hujikita katika itikadi na hii ina maana kwamba itikadi huvyazwa na usemi, jambo linalopelekea usemi kuweza kuchanganuliwa kwa kina zaidi kwa kujikita katika jinsi usemi huo unavyofasiriwa, unavyopokelewa na athari ya usemi huo katika jamii. Kwa vile usemi ni historia, ufasiri wa usemi hutegemea muktadha wa historia. Nadharia ya UCHAMAWADI hujikita katika masuala mengine yasiyo ya Kisimu kama vile itikadi, utamaduni na jamii (Fairclough na Wodak, 1997).

Kulingana na UCHAMAWADI, usemi ni mchakato au shughuli ya kijamii inayohusisha mambo mengi yanayomwangazia binadamu kwa vile yeye ndiye pekee aliye na uwezo wa kusema. Fairclough ndiye mtaalam tajika aliyeweza kuyachukua mawazo ya Karl Marx (1859) kuhusu mitazamo ya kijamii inayosisitiza umuhimu wa mbinu za uzalishaji. Kwa mujibu wa mtaalam huyu, jukumu la UCHAMAWADI ni kubaini jinsi kutokuwepo kwa usawa na vilevile mivutano ambayo ni mifumo ya kibepari ya uzalishaji mali hudhihirika katika usemi au matini (Fairclough 1989, 1995). Katika hali hii, mtazamo ni dhana muhimu sana kwa vile Teun Adrian Van Dijk anachangia kwa kueleza kuwa mtazamo una dhima ya kusaidia katika kuelewa na kufasiri matini na usemi (Van Dijk 1993, 1996 & 2001). Ni muhimu tuelewe mitazamo ambayo hutokana na shughuli za

kijamii ili tuweze kuelewa ukosefu wa usawa wa kijamii. Mitazamo na mielekeo hii ndiyo huchangia namna ulimwengu hufasiriwa.

Van Dijk (1993) alifanya utafiti kule Uingereza na alitumia mfano wa jinsi ubaguzi wa rangi unavyoweza kuathiri mazungumzo dhidi ya mtu mweupe na mweusi. Kulingana na Van Dijk, mitazamo hiyo ndiyo huzua mielekeo tofauti tofauti akilini mwa watu. Hali hii ndiyo huonyesha upendeleo kama ubabedume, kiburi na dharau kutegemea mielekeo na mitazamo iliyomo akilini. Nadharia hii huchanganua uhusiano wa lugha na ruwaza za kiuwezo zinazozua ukosefu wa usawa kijamii. Kwa mantiki hii, nadharia ya UCHAMAWADI huchanganua muundo ulio wazi na usio wazi wa mahusiano ya kimamlaka, kiubaguzi, kiuwezo na kiutawala ambayo hudhihirishwa na kushamirishwa na lugha.

Nadharia ya UCHAMAWADI, ina mihimili ifuatayo:

- i. Huangazia matatizo ya kijamii. Haiangazii tu lugha na matumizi yake bali pia sifa za kiisimu za kijamii na utamaduni. Huchanganua usemi kwa kina ili kuonyesha mahusiano ya kimamlaka ambayo husababisha matatizo ya kijamii.
- ii. Uhusiano wa kimamlaka hutokana na usemi. Hueleza uhusiano wa kijamii na namna unajitokeza katika usemi.
- iii. Huhusisha jamii na utamaduni. Matumizi ya lugha huchangia mabadiliko katika jamii na utamaduni wa jamii hiyo pamoja na uhusiano wa kimamlaka. Usemi hushughulikia itikadi. Itikadi huvyazwa katika usemi. Haitoshi kuchanganua tu

usemi bali pia ni muhimu kuchanganua namna usemi hufasiriwa, hupokelewa na athari ya usemi huo katika jamii husika.

- iv. Usemi ni historia. Ufasiri wa usemi hutegemea muktadha wa historia. Kutokana na hili, nadharia ya UCHAMAWADI hutegemea masuala mengine yasiyo ya Kiisimu kama vile utamaduni, jamii na itikadi.

#### **Dhima ya Nadharia ya UCHAMAWADI katika Utafiti huu**

- i. Huangazia matatizo ya kijamii. Haiangazii tu lugha na matumizi yake bali pia sifa za kiisimu za kijamii na kitamaduni. Mtafiti anayejikita katika nadharia hii anafaa kutambua kuwa katika uchanganuzi wake hawezi kuangazia tu upande mmoja bali anastahili kuwa na jicho pevu ili aweze kuyaona yaliyo ndani zaidi kama vile uhakiki wa vipasiho vya lugha katika majigambo ya Waisukha. Mtafiti akifanya hivyo atapata fursa ya kuchimbua maana iliyosetiriwa ndani ya nomino na vishazi ili kuweza kudhihirisha ubabedume uliomo. Nadharia hii inasisitiza sifa za kiisimu za kijamii na kitamaduni kwa vile kila jamii ina utamaduni wake na hakuna njia inayofanana na nyingine katika muktadha huo. Madhumuni ya kwanza ya kubainisha namna vipashio vya lugha katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* yalifaidi kutokana na mhimili huu kwa sababu kuna kule kuhusisha Isimu na Fasihi Simulizi. Nadharia ya UCHAMAWADI ina azma ya kuwahimiza watafiti kuwa makini katika uteuzi wa lugha kwa sababu lugha ina dhima tofautitofauti katika jamii. Matumizi ya vipashio vidogo vya lugha kama msingi wa utangulizi umeshadidiwa na Fairclough (1992) anayehoji

kuwa mchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni sharti aanze kwa kuvichanganua vipengele vya chini (vidogo) vinavyopatikana katika matini kama vile msamiati, nomino na vishazi na aendelee hadi kwa vipengele vikubwa ambavyo matini huchota kwayo kama vile semantiki na pragmantiki. Umuhimu wa mwelekeo huu ni kuwa mtafiti hupata fursa ya kuvichagua vipengele vya Kiisimu anavyohitaji kuangazia kulingana na maswali ya utafiti, suala la utafiti au kichocheo cha utafiti husika (Fairclough 2013). Nadharia hii ni mwafaka kwa vile inaongezea kuwa kuangazia vipengele vya lugha pekee hakutoshi kwa sababu matini huchota kutoka kwa jamii na wanaotoa matini. Lengo kuu la UCHAMAWADI ni kushughulikia matini na muktadha ili kutatua matatizo ya kijamii (Walsh 2001).

- ii. Uhusiano wa kimamlaka hutokana na usemi. Mhimili huu huweka wazi uhusiano wa kijamii na namna unavyojitokeza katika usemi. Kwa mujibu wa nadharia hii, uhusiano wa kimamlaka hautokei tu katika ombwe tupu bali hubuniwa na usemi au mazungumzo ya wanajamii husika. Nadharia hii ya UCHAMAWADI ni mwafaka katika utafiti huu kwa vile lengo kuu ni kuchunguza ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mayo* ya Waisukha kwa mtazamo wa Kisemantiki. Mhimili huu uliafiki lengo hili kwa vile ubabedume ni uhusiano wa kimamlaka katika jamii na majigambo ni usemi. Nadharia hii yasisitiza umuhimu wa kuchunguza na kuhakiki usemi wowote ule kwa makini ili kutambua ni vipengele vipi vya kimamlaka vilivyomo. Nadharia ya UCHAMAWADI pia iliafiki matakwa ya madhumuni ya pili kwa vile yalihatiji uhakiki wa tamathali za semi zinazosheheni ubabedume ulio na uhusiano wa kimamlaka katika jamii

ya Waisukha kwa mtazamo wa kisemantiki na kuzua maana mbalimbali katika tamathali hizo za usemi kama jazanda na chuku.

- iii. UCHAMAWADI huhusisha jamii na utamaduni. Nadharia hii ina azma ya kuwahimiza wahakiki waweze kuzingatia utamaduni pamoja na jamii husika katika uchanganuzi wao. Lugha ya mtu ni kitambulisho chake, kwa hivyo nadharia hii inadhihirisha kwamba matumizi ya lugha huchangia mabadiliko katika jamii husika na utamaduni wa jamii hiyo ikiwemo uhusiano wa kimamlaka. Mhimili huu uliusaidia utafiti huu katika kuvichunguza vipengele vingine kama vile itikadi kwa vile haitoshi kuchanganua tu usemi bali ni bora kuchanganua namna usemi hufasiriwa, hupokelewa na athari ya usemi huo katika jamii husika. Haya yaliafiki madhumuni ya tatu ambayo yalijalizwa na nadharia ya Uwezo-uume.
- iv. Usemi ni historia. Ufasiri wa usemi hutegemea muktadha wa historia. Kutokana na nadharia ya UCHAMAWADI, ni wazi kuwa hujikita katika masuala mengine yasiyo ya Kiisimu kama utamaduni, jamii na itikadi. Nadharia hii inasisitiza kuwa, historia ya jamii fulani ni muhimu irejelewe ili kuweza kuchanganua masuala ya diskosi kwa urahisi. Masuala ya kihistoria kuhusu jamii ya Waisukha yamebainika wazi katika utafiti huu na yameweza kuusaidia utafiti huu kumwelewa mwanamume Mwisukha kupitia kwa usemi wa majigambo ambayo yana historia ndefu inayodhihirika kupitia kwa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Kulingana na Fairclough (1995) diskosi inafaa kumsaidia mchanganuzi kubainisha kitendo fulani cha kijamii kutoka kwa mwelekeo fulani.

Hivyo basi, ikiwa usemi ni historia, majigambo ya Waisukha pia ni tofauti na majigambo ya jamii nyingine. Mhimili huu ulikuwa faafu kwa vile ulimsaidia mtafiti kuchanganua suala la ubabedume kwa kujikita katika nasaba za Waisukha.

Nadharia ya UCHAMAWADI pia ilitumika na Owala (2014) katika tasnifu yake ya “Uchanganuzi wa Matini Zilizoteuliwa za Ugaidi katika Gazeti la Taifa Leo la Kenya, kati ya Oktoba 2010 na Novemba 2011.” Owala anaeleza kwamba, mchanganuzi yeyote wa usemi anastahili kufanya makini katika uteuzi wa lugha; vyanzo vya habari na nafasi ya uwasilishaji wa usemi katika kuripoti habari za ugaidi ili kupunguza mwegemeo na athari hasi zinazosababishwa na mwegemeo huo. Nadharia ya UCHAMAWADI ilimwezesha mtafiti huyo kuchunguza jinsi uteuzi wa lugha unaweza kuwa na athari mbalimbali kwa wasomaji wa habari za ugaidi. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba kuna haja ya kufanya makini katika uteuzi wa lugha; vyanzo vya habari na nafasi ya uwasilishaji wa usemi katika kuripoti habari za ugaidi ili kupunguza mwegemeo na athari hasi zinazosababishwa na mwegemeo huo. Uchanganuzi wa mtaalam huyu uliusaidia utafiti huu kwa vile kulikuwa na haja ya kuichunguza lugha iliyotumiwa katika majigambo ya Waisukha kwa kina ili kuweza kuteua vipashio mbalimbali vya lugha vilivyosheheni ubabedume.

Mihimili hii imeafiki utafiti huu kwa njia kadha wa kadha. Wahakiki wengi huchukulia masuala ya ushairi hasa majigambo kama yaliyo magumu kuchanganua. Nadharia hii imetoa mwelekeo jinsi uchanganuzi wa diskosi unafaa kufanywa kwa umakini. Katika hali hii, ninaona majigambo na usaili wa fanani na washiriki katika sherehe za *Shilembe*



na *Mchezasili* wa *Mayo* katika utafiti huu kama vipera vya diskosi. Nadharia hii pia ilitumika katika kufafanua vipashio vya lugha ambavyo vinasawiri ubabedume. Kwa kuongozwa na nadharia hii ya UCHAMAWADI, mtazamo wa Kisemantiki umebaini taashira mbalimbali za ubabedume katika majigambo ya Waisukha.

Kabla ya kuasisiwa kwa nadharia hii, uchunguzi wa lugha na jinsia ulianza katika nchi za Kimagharibi na tamaduni zao katika miaka ya katikati mwa 1970 (Mills & Mullany 2011). Wanaisimu walichunguza lugha kimuundo bila kuzingatia matumizi na uamilifu wa lugha katika jamii. Umilisi wao ulikitwa katika umilisi wa wazawa wa lugha (Chomsky, 1957), uhusiano baina ya lugha na muktadha (isimu amali). Levinson (1983) anachangia hoja hii kwa kudai kuwa, kwa kuzingatia umilisi wa kipragmatiki, sentensi na vipashio vya sentensi vilichukuliwa kama viambajengo vya msingi katika uchanganuzi wa lugha. Nadharia ya UCHAMAWADI hutambua uamilifu wa lugha katika jamii, Fairclough na Wodak (1997) na umuhimu wa lugha hukitwa katika miktadha ya matumizi (Wodak, 2000, Benke, 2000). Kiambajengo muhimu ni matini au usemi kwa vile ndicho kipashio muhimu cha mawasiliano. Kwa mantiki hii, UCHAMAWADI ni nadharia ambayo huchanganua muundo ulio wazi na usio wazi wa mahusiano ya kimamlaka, kiubaguzi, kiuwezo na kiutawala ambayo hudhihirishwa na kushamirishwa na lugha.

Mbali na nadharia ya UCHAMAWADI kuweza kuangazia matatizo ya kijamii, inaangazia pia lugha, matumizi yake pamoja na sifa za Kiisimu za kijamii na kitamaduni. Viambajengo vya lugha hususan vya Kisemantiki vilichanganuliwa na kuhakikiwa ili kuweka wazi itikadi, historia na mielekeo ya Waisukha inayotawala ruwaza za kiuwezo

katika mitagusano na utangamano wa wanajamii. Nadharia ya UCHAMAWADI ina jukumu la kuweza kuchanganua usemi kwa kina ili kudhihirisha mahusiano ya kimamlaka ambayo husababisha utofauti wa kijinsia kama vile ubabedume katika jamii. Uhusiano huu hutokana na usemi kama ilivyodhihirika katika majigambo ya Waisukha. UCHAMAWADI hueleza uhusiano wa kijamii na jinsi uhusiano huo unavyojitokeza katika usemi ndiposa majigambo ya Waisukha yalikuwa na dhima ya kuusawiri ubabedume katika jamii hiyo. Usemi huhusisha jamii na utamaduni, kwa hivyo, majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* yalikuwa muhimu katika kumwelewa mwanamume Mwisukha na jinsi ubabedume unavyodhihirika katika jamii hiyo. Jambo hili linaonyesha kuwa lugha na matumizi yake huchangia mabadiliko katika jamii na utamaduni wa jamii husika pamoja na uhusiano wa kimamlaka.

Usemi pia hujikita katika masuala ya itikadi. Kwa vile itikadi huvyazwa katika usemi, kuchanganua tu usemi hakutoshi bali kunahitaji ufasiri, namna usemi huo unavyopokelewa na athari yake katika jamii. Haya ndiyo yaliyotuelekeza katika kuchanganua masuala ya itikadi kwa kurejelea miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* katika sherehe ya kupiganisha fahali. Kuna mhimili mwingine unaodai kuwa, usemi ni historia, kwa hivyo, UCHAMAWADI hutegemea masuala mengine yasiyo ya Kiisimu kama vile itikadi, utamaduni na jamii. Katika muktadha huu, utafiti huu uliweza kuhakiki ubabedume unavyosawiriwa katika majigambo ya Waisukha kwa kuangazia itikadi katika miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*, hivyo kuweka wazi utamaduni wa jamii ya Waisukha. Kwa hivyo, usemi kwa mtazamo wa UCHAMAWADI ni aina ya

shughuli ya kijamii, kama ilivyokuwa katika sherehe hizo mbili miongoni mwa Waisukha.

Madhumuni makuu ya nadharia hii ya UCHAMAWADI yanayodhihirika bayana ni kubainisha na kuweka wazi uhusiano wa kimamlaka kama ilivyojitokeza katika ubabedume wa mwanamume Mwisukha katika miviga ya sherehe ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Ndiposa Fairclough aliweza kuchukua mwelekeo wa Karl Marx (1859) katika Williams (1978) kuhusu mivutano ya kijamii (Fairclough na Wodak, 1997). Huu ndio mtazamo unaochangia mbinu za uzalishaji. Kulingana naye, kazi ya UCHAMAWADI ni kuweza kutambua namna ukosefu wa usawa na mivutano ambayo ni mifumo ya kibepari ya uzalishaji mali hujidhihirika katika usemi (Fairclough 1989, 1995). Haya yalijitokeza wazi katika majigambo ya Waisukha yaliyosheheni ubabedume mwingi na namna wanawake wanavyowategemea ili kuzalisha mali kama vile mifugo hususan ng'ombe katika jamii hii.

### **1.8.2 Nadharia ya Uwezo-Uume**

Nadharia ya Uwezo-Uume iliasisiwa na Robert Bly (Wells & Holland, 2001) na kuendelezwa na Izugbara mnamo mwaka wa 2005. Nadharia hii hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Asili ya nadharia hii hufungamanishwa na umiliki wa dhakari (wanaume). Izugbara anaeleza kuwa dhakari hutumiwa kama chombo cha kumshusha hadhi mwanamke. Walsh (1997) anasema kuwa uume huhusishwa na uwezo wa mwanamume kuwa na mafanikio kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Mwanamume hazaliwi na uume kama sehemu ya viungo vyake bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni anamokulia.

Nadharia hii imejengeka katika misingi kwamba utamaduni ni dhana muhimu na ni uti wa mgongo katika ujenzi na matumizi yake kutegemea jamii husika kwa vile, kila jamii ina utamaduni wake. Nadharia hii ina mihimili minne mikuu. Nayo ni;

- i. Kwanza kabisa ni itikadi za kijamii, ambazo huongoza fikra, mitazamo na mielekeo ya wanajamii. Teneti hii ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile ilisaidia katika kutathmini jinsi jamii ya Waisukha huratibu mahusiano ya kijinsia katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* na kuweza kusawiri ubabedume kupitia kwa majigambo yanayoghaniwa na fanani.
- ii. Pili, ni utamaduni ambao huakisi ujumla wa maisha ya jamii pamoja na mahusiano na matarajio ya jamii kuwahusu. Utamaduni wa jamii hujikita katika lugha, imani na desturi ambazo hutamalaki katika mfumo mzima wa jamii.
- iii. Tatu, teneti hii inaelezea kuhusu jinsi majukumu hugawanywa kiuana. Kuna yale ambayo yametengewa jinsia ya kike na mengine jinsia ya kiume. Mgawanyo huu hudhihirisha namna mamlaka na uwezo hugawanywa kijinsia.
- iv. Nne, ni sifa angama za uwezo-uume. Hizi ni sifa ambazo ni sharti mwanamume awe nazo ili kuweza kujenga, kudumisha na kudhihirisha ubabe. Sifa hizi ni kama vile; uvumilivu, uwezo, kutoogopa, kuthubutu, ukware miongoni mwa sifa nyingine.

Mihimili ya nadharia hii ilikuwa muhimu kwa vile iliungoza utafiti huu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data ili kufikia lengo la utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu ulilazimika kuifidia nadharia hii kwa kuioanisha na nadharia ya UCHAMAWADI ili

kuweza kuyachanganua majigambo ya Waisukha kwa kina zaidi kwa kutumia mtazamo wa kisemantiki.

**Mihimili ya nadharia ya Uwezo-uume iliyotumika katika utafiti huu:**

- i. Mihimili wa pili unasisitiza kuhusu utamaduni ambao huakisi ujumla wa maisha ya jamii pamoja na mahusiano na matarajio ya jamii kuwahusu. Mihimili huu unaweza kuunganishwa na mhimili wa kwanza unaoeleza kuwa itikadi za kijamii ndizo ambazo huongoza fikra, mitazamo na mielekeo ya wanajamii pamoja na teneti ya nne inayoangazia sifa angama za uwezo-uume. Mihimili hii iliusaidia utafiti huu katika kuyashughulikia madhumuni ya tatu. Kutokana na mihimili hii, nadharia ya Uwezo-uume inasisitiza umuhimu wa kuzichunguza itikadi, historia na lugha za jamii husika ili kufahamu ubabedume unavyojengwa, kuendelezwa na kudumishwa. Katika nadharia hii, ni wazi kuwa huwezi kushughulikia jamii yoyote ile bila kufahamu kwanza utamaduni na itikadi za wanajamii kwa vile lugha ni utamaduni na kitambulisho cha mwanajamii.
- ii. Nadharia ya Uwezo-uume ina azma ya kuwahimiza watumizi wake kuteua utamaduni wa jamii husika kwa kurejelea historia yake na lugha yake ili kuweza kufuatilia asili ya mielekeo, mitazamo na falsafa za jamii husika. Nadharia hii ilikuwa mwafaka katika utafiti huu kwa vile mihimili iliyotajwa iliwezesha utafiti huu katika kubainisha namna ubabedume hukuzwa, kupitia kwa majigambo yanayoghanwa katika miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Ubabe huo huendelezwa na kushamirishwa na mahitaji ya utamaduni wa jamii ya Waisukha

kwa kuchunguza historia yao na asili ya miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili* wa Mayo. Mihimili hii ilisaidia katika kuchunguza sifa angama za uwezo uume kama vile mhimili wa nne unavyopendekeza. Hatua hii ilikuwa muhimu sana kwa vile nadharia hii humulika sifa kama vile mwanamume kuwa na uvumilivu, uwezo, kutoogopa, kuthubutu, ukware miongoni mwa sifa nyingine. Mtafiti wa masuala ya ubabedume anahitajika kuzifahamu sifa hizi ili azihakiki vilivyo. Nadharia ya Uwezo-uume inatoa mwelekeo bora kwa wanaume katika jamii kuchukua nafasi yao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Nadharia ya Uwezo-uume pia ilitumika na Matinde (2015) katika tasnifu yake ya “Uchanganuzi wa Ubabedume katika Majigambo (Amabaiko) ya Abakuria”. Matinde anaeleza kwamba, ubabedume hujitokeza katika mahusiano mbalimbali ya kijamii kama vile; unyagoni, jandoni na arusini miongoni mwa mengine. Nadharia ya Uwezo-uume ilimwezesha mtafiti kuchunguza ukuzaji na uendelezaji wa ubabedume kupitia kwa majigambo ya sherehe mbalimbali za jamii ya Abakuria. Mihimili hii imeafiki tu utafiti huu kwa kuangazia madhumuni yetu ya tatu pekee. Katika mahusiano mbalimbali ya kijamii, wanaume wana sifa mbali mbali ambazo huwakweza kama vile ukakamavu, uvumilivu, ukware na kuthubutu. Kwa upande mwingine, kuna zile sifa ambazo huidhalilisha jinsia za kike kama vile uoga, kutohubutu mambo na kadhalika. Mahusiano hayo hutegemea mila na desturi za jamii husika. Nadharia hii iliufaidi utafiti huu katika kutambua umuhimu wa kuangazia masuala ya historia na itikadi za kijamii ili kuchipua, kujenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume katika majigambo ya Waisukha

wanapopiganisha fahali katika miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Nadharia hii ina azma ya kueleza ni kwa nini wanaume wanamiliki uwezo dhidi ya wanawake.

### **1.9 Hitimisho**

Sura hii kwa ujumla imeshughulikia mambo ya kiutangulizi ambayo ndiyo msingi wa tasnifu nzima. Mambo haya ni pamoja na usuli wa utafiti unaohusiana na historia ya *Shilembe* na *Mayo* kwa kurejelea upiganishaji fahali na usawiri wa ubabedume katika majigambo ya miviga ya sherehe hizi katika jamii nyingine. Suala la utafiti ambalo linahusu ubabedume miongoni mwa Waisukha na namna unavyodhihirika katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Mengine yaliyoshughulikiwa ni malengo na maswali ya utafiti, sababu ya uteuzi wa mada, upeo wa utafiti, umuhimu wa utafiti na misingi ya nadharia. Kwa hivyo, hii ni sura ambayo inabainisha kile ambacho mtafiti alilenga kutekeleza.

## 1.10 Maelezo ya Istilahi

**Animonimu** : Njina au majina ya wanyama.

**Anthroponemia** : Ni utanzu unaoshughulikia anthroponimu.

**Anthroponimu:** Ni jina au majina ya watu.

**Fanani** : Msimuliaji wa kisa katika majigambo ya Waisukha.

**Fanani Mjigambi:** Fanani anayejigamba katika majigambo.

**Fanani Mtambaji:** Fanani anayesimulia kisa katika majigambo.

**Itikadi** : Dhana hii imetumika kurejelea sheria na imani zinazoongoza mfumo wa maisha ya Waisukha kwa kuangazia misingi yao ya kiuchumi, kisiasa, kiutawala na hata kitamaduni.

**Majigambo** : Ni aina ya ushairi unaotolewa kwa kalima au kughaniwa badala ya kuimbwa. Ni maigizo yanayotoa mwanya kwa Waisukha kujisifu na kujitapa kwa sababu ya matendo fulani ya kishujaa au mafanikio katika nyanja fulani za kimaisha. Ni sanaa ya ushairi ambayo hutumia uteuzi maalum wa maneno ili kuibua hisia za uchungu au furaha kwa wasikilizaji katika jamii ya Waisukha.

**‘Master key’** : Katika utafiti huu, dhana hii imetumika kurejelea dhakari ilivyo na majukumu mengi ya kiuwezo kama vile uwezo wa kufungua milango



mingi ya wanawake yaani uwezo wa mwanamume wa kuoa zaidi ya mke mmoja.

**Mayo:** Sherehe ya *Shilembe* inayofanywa kisanaa katika jamii ya Waisukha.

**Mfumo-dume:** Mfumo wa muundo wa kijamii ambao mwanamume anapewa nguvu na uwezo zaidi dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za maisha; kuitawala, kiuchumi, kidini, kisiasa na kijamii.

**Mtazamo wa**

**Kiisimu** : Unatumiwa kurejelea usawiri wa ubabedume kwa kujikita katika uchanganuzi wa vipashio vya lugha kama vile jazanda, istiara, takriri, tanakali za sauti kwa kujikita katika mtazamo wa Kisemantiki.

**Onomastiki** : Ni taaluma inayoshughulikia majina kwa jumla.

**Osama** : Kwa mujibu wa utafiti huu, fahali kutoka nasaba fulani hupewa jina Osama kama yule aliyehusika na mashambulizi ya kigaidi ili kudhihirisha ushujaa wa hali ya juu.

**Shilembe** : Sherehe inayofanywa na Waisukha hasa kwa wafu waliokuwa mashujaa au aliyemuua mtu katika jamii hii. Mtu aliyeuawa alifaa kuwa Mzungu au Mnandi kwa vile alikuwa adui. Huhusisha fahali wawili ambao huletwa siku moja baada ya mazishi na huongozwa na wazee wateule.

**Spana** : Katika utafiti huu kifaa hiki kimetumika kijazanda kurejelea matumizi anuwai ya dhakari kama vile kubikiri na kupachika mimba. Jambo linalompa mwanamume mamlaka dhidi ya mwanamke.

**Tsinziga** : Hizi ni pembe za fahali ambazo hutumika wakati wa upiganishaji fahali. Katika utafiti huu, dhana hii imetumika kurejelea kunolewa kwake na kufananishwa na kusimika kwa dhakari ya mwanamume.

**Tsichirishi** : Ng'ombe wa kiume wanaotumiwa katika kupigana wakati wa Mchezasili wa *Mayo* au miviga ya *Shilembe*.

**Ubabedume**: Matumizi ya nguvu dhidi ya watu wengine. Hujengwa na kushamirishwa na sifa kama vile; ujasiri au ushujaa, uwezo wa kutawala, uhuru, ukware, ushindani, mamlaka, kuthubutu, nguvu na mamlaka ya kuamuru na kuongoza.

**Uchunzaji-Shiriki**: Ni mbinu ya utafiti inayojumuisha kushiriki, kushuhudia na kuhoji fanani, washiriki na wasailiwa wakati wa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*.

## **SURA YA PILI**

### **UHAKIKI WA MAANDISHI**

#### **2.1 Utangulizi**

Sehemu hii ilijadili tahakiki za maandishi mbalimbali yanayohusiana na ubabedume na hasa itikadi, historia na ujenzi wa ubabedume kijumla pamoja na suala la majigambo, miviga na taaluma nyingine. Mtindo uliotumiwa ni ule wa kujadili mada mbalimbali zinazohusiana na ubabedume. Vipengele vitatu vilishughulikiwa mathalan: mikakati ya kiisimu inayotumiwa kuibua ubabedume katika lugha ya majigambo, taashira za ubabedume katika majigambo na dhima ya majigambo katika ujengaji wa ubabedume.

#### **2.2 Dhana ya Ubabedume**

Kwa ajili ya tasnifu hii, kuna haja ya kuweka wazi maana ya ubabedume kama inavyoelezwa na wataalamu mbalimbali na kufikia mwafaka wa yale yanayorejelewa tunapozingatia ubabedume. Maandishi mbalimbali yanayohusiana na ubabedume yanaonyesha kuwa kuna utata katika kijejezi cha ubabedume. Utata huo unatokea kwa sababu ya mielekeo na misimamo mbalimbali ambayo ina athari kubwa dhidi ya maoni ya watu (Hoffman 1998). Ingawa hivyo, kwa ajili ya utafiti huu, itakuwa ni bora kueleza kile tunachomaanisha kila tunapotaja neno “ubabedume.”

Maana ya awali ya ubabedume ni ile ya Oxford (1948) katika Matinde (2015) aliyeeleza kuwa ubabedume ni hali ya kuwa na sifa za jinsia ya kiume kama vile utanashati, ujamali na ushujaa. Hali hii inaweza kuchukua mifumo mbalimbali kutegemea na utamaduni wa jamii husika. Maelezo haya yamenakiliwa kuonyesha kuwa dhana ya ubabedume

imekuwa ikibadilika kutegemea mielekeo mipya inayojiri kuhusiana na swala hili. Onyango (2011) anaeleza kuwa dhana ya ubabedume ilianza kutumika hata kabla ya ukoloni. Anaongezea kuwa, dhana mbalimbali za Fasihi Simulizi kama vile, vitendawili simulizi, vitanzandimi na nyimbo zilimsawiri mwanamume kama shujaa, mwenye hadhi na mamlaka zaidi ya mwanamke. Mtaalam huyu anadokeza kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya nyimbo na mahusiano ya kiuwezo.

Kwa hivyo, katika jamii nyingi nchini Kenya, nyimbo zilitungwa kumtukua mwanamume hasa kuhusu nafasi yake ya utawala na pale ambapo nyimbo zilitungwa kuhusu mwanamke zilidokeza sura hasi ya mwanamke. *Kamusi ya Karne ya 21* (2015) inaeleza ubabedume kama ujanja na hila za kutumia nguvu, ugangwe au tendo la dhuluma na maonevu.

Kulingana na Walsh (1997), katika jamii za Kiafrika, ubabedume huhusishwa na uwezo wa mwanamume kuwa na mafanikio kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Aidha, anaeleza kuwa mwanamume hazaliwi na ubabedume kama sehemu ya viungo vyake vya uzazi bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni anamokulia.

Choti (1998) anaeleza kuwa ubabedume ni hali ya mwanamume kuchorwa kama binadamu mwenye nguvu tofauti kabisa na mwanamke, anaongezea kwa kusema kuwa mwanamume huangazwa kwa mtazamo chanya ilhali mwanamke huangazwa kwa mtazamo hasi. Ingawa hivyo, utafiti wake ulijikita katika jinsia ya kike. Maelezo ya Oxford kwa hivyo yanaonekana kupitwa na wakati. Hata hivyo, bado ni msingi muhimu na pahali mwafaka pa kuanzia maelezo na ufafanuzi wa dhana ya ubabedume.

Matinde (2006) katika utafiti wake kuhusu usawiri wa mwanamume katika nyiso za jando za Abakuria, anabainisha jinsi matarajio, mitazamo na mielekeo ya jamii huchukua nafasi muhimu katika kuratibu majukumu kiuana na kutathmini thamani ya kila jinsia. Mtaalam huyu amedhihirisha kuwa jamii ya Abakuria humsawiri mwanamume kwa njia chanya tofauti na mwanamke, kama anavyodai Choti. Vilevile, nyiso za jando za Abakuria hudhihirisha uwezo mkubwa alio nao mwanamume katika nyanja mbalimbali za kijamii kama vile, sheria, siasa, utawala, uchumi na mamlaka juu ya maamuzi na maafikiano katika jamii.

Wanjala (2011, 2015) akiunga mkono mawazo ya wataalam hawa anadhihirisha wazi jinsi nyiso za jando za Wabukusu zinavyomsawiri mwanamume Mbukusu kwa kumpa sifa za ushujaa. Anaeleza kuwa tohara ni muhimu katika jamii hii kwa vile ni ishara ya uwezo na uhalalisho wa ushujaa na ukali katika kutetea jamii yake. Anasisitiza kuwa baada ya tohara kijana wa kiume huruhusiwa kuingia katika kundi la watu wazima na kwamba tohara ilikuwa sharti muhimu katika kuoa au kuolewa. Maoni haya yanaonyesha jinsi ubabedume ni suala tata.

Kwa upande mwingine, ubabedume katika utafiti huu umedhihirishwa na vipashio vya nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo yanayoghaniwa na fanani watambaji na fanani wajigambi. Majigambo hayo hutaja majina mbalimbali ya watu mashuhuri, wanyama, ndege na hata dhana nyingine katika mazingira zinazorejelea ubabedume. Hali hii inarejelea taaluma ya Onomastiki hususan anthroponemia na animonimu.

Kamusi za Merriam-Webster na Wikipedia zinafafanua Onomastiki kama taaluma inayohusu majina ya watu, wanyama na mahali. Maelezo haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu utafiti huu ulijikita katika kuyahakiki majina wanayopewa wanyama-fahali wanaotumiwa katika majigambo ya sherehe ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* wakati wa upiganishaji wa fahali. Utafiti wetu umebaini jinsi majina ya watu kama Mike Tyson, ndege kama vile bundi na Eminyi, majina ya majazi kama vile spana na master key miongoni mwa mengine hupewa fahali wanapopiganishwa kutegemea nasaba mbalimbali na hali hii husawiri ubabedume katika jamii ya Waisukha. Tamathali za semi zinazotumika katika majigambo hayo hubeba sifa mbalimbali za kiubabe mathalan chuku inayorejelea Wavulana wa ukoo fulani katika jamii hii kuwa na urefu wa futi tisa (Taz. Jigambo la 11 Kiamb. B).

Crystal (1987) anahoji kuwa Onomastiki ni sayansi maalum inayochunguza au kutalii majina ya viumbe. Taaluma hii hutambulisha majina ya watu, wanyama na mahali. Mawazo haya yanakaribiana na ya TUKI (2004) wanaoeleza kuwa istilahi nomino inatokana na neno la Kilatini linalojulikana kama 'nomen' lenye maana ya neno la kutaja kitu. Maelezo haya ni msingi muhimu katika tasnifu hii kwa sababu imeshughulikia jinsi ambavyo nomino mbalimbali katika majigambo ya Waisukha husawiri ubabedume. Tafiti mbalimbali zimeshughulikia taaluma ya Onomastiki na kueleza umuhimu wa majina katika jamii mbalimbali.

Aswani (1993) alichunguza kipengele cha anthroponimu katika lugha ya Kiluhya. Aliziainisha anthroponimu katika vikundi vitano vya: tabia, mazingira, matukio, maumbile na vitu vya kawaida. Ameonyesha mfumo unaofuatwa na Waluhya katika

kuunda anthroponimu na namna ambavyo anthroponimu hizi zinaweza kuchanganuliwa kiisimu. Kwa mfano, alitaja anthroponimu khandu yenye maana ya ‘kijitu’ na kutoa antonimi yake ambayo ni kundu na iliyo na maana ya ‘jitu’. Aswani anaonyesha kuwa majina ya watu hutokana mathalan na mazingira au tabia. Hali hii ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile fahali katika majigambo ya Waisukha hupewa majina kutoka katika mazingira ya jamii yanayosawiri ubabedume. Utafiti wake ni muhimu kwa vile alihusisha fasihi na isimu. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na tasnifu hii kwa sababu yeye alishughulikia anthroponimia katika lahaja kumi na saba za Kiluhya ilhali utafiti huu unachunguza namna ubabedume unavyosawiriwa katika majigambo ya Waisukha kupitia kwa anthroponimia wanazopewa fahali, vishazi na vitenzi vinavyotumiwa wakati wa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Dhana ya anthroponimia katika kazi yake iliwekea utafiti huu msingi bora kuhusu maana ya majina kama ilivyo katika majigambo ya Waisukha.

Choge (1997) alitafitia anthroponemia asilia za Kinandi kwa mtazamo wa kisemantiki. Anafafanua anthroponimu kama jina au majina ya watu ilhali animonimu ni jina au majina ya wanyama. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba maana za anthroponimu za Kinandi zinapatikana katika utamaduni wa Wanandi. Katika utafiti wake ametumia anthroponimu za kijazanda. Kwa mfano, badala ya kutaja nyoka kwa kutumia animonimu yake halisi, anatumia kifungu jina ‘mnyama mrefu’. Mtaalam huyu anasema kuwa sababu maalum ya kutumia jazanda hii ni kuondoa ule ukali ambao ungeletwa na matumizi ya leksia ndara au eren zilizo leksia halisi za kurejelea nyoka katika Kinandi. Huu ni mchango kwa utafiti huu kwa sababu madhumuni ya pili ya utafiti huu yalilenga

kubaini jinsi tamathali za usemi kama vile jazanda husawiri ubabedume kwa mtazamo wa kisemantiki. Kulingana na utafiti wake, anthroponimu ni kipengele cha isimu ambacho kinaweza kuhakikiwa sifa zake za kisemantiki. Anahoji kuwa uchunguzi wa awali juu ya anthroponemia unaonyesha kuwa anthroponimu za Kiafrika zimechunguzwa kwa mikabala kama vile ya kianthropolojia, kihistoria na kifalsafa. Utafiti wa mtaalamu huyu ni rejea muhimu katika tasnifu hii kwa sababu, utafiti huu ulichunguza anthroponimu zinavyosawiri ubabedume kwa mtazamo wa kisemantiki. Kazi yake ina mchango kwetu kwa vile ilitupatia mwelekeo wa kuchanganua majigambo kisemantiki. Kwa hivyo, utafiti huu ulijikita katika mtazamo wa kisemantiki na pia ulichunguza jinsi majina mbalimbali husawiri ubabedume katika jamii ya Waisukha kupitia kwa majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Ndiposa kazi yake ni rejea maalum katika utafiti huu. Ingawa kazi yake inatofautiana na yetu kinadharia na kimadhumuni, utafiti huu ulifaidika kutokana na utafiti wake kwa ajili ya kushughulikia taaluma ya Onomastiki kwa kutumia mtazamo wa kisemantiki. Vilevile, utafiti huu ulifaidika kutokana na maelezo yake ya dhana za anthroponimia na animonimu.

Okal (2012) katika makala yake alitafitia Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onomastiki na akajikita katika Uhakiki wa Mbinu zake katika Tafsiri. Anaeleza kuwa taaluma hii inakua na kuzagaa kote ulimwenguni kwa sababu kuna nguvu katika majina wanayopewa watu fulani. Kulingana na uchunguzi wa mtaalam huyu, anaeleza kuwa kitengo kinachoshughulikia majina ya watu hujulikana kama anthroponomastiki au anthroponimu. Anahoji kuwa, kila kiumbe hupewa majina na binadamu ili kurahisisha mawasiliano. Kulingana na Okal, wanaisimu mbalimbali wanadokeza kuwa neno



linalotumiwa kutaja kiumbe hudhukuriwa aghalabu na wanaisimu wengi kama nomino. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba tafsiri ina mchango mkuu katika taaluma ya Onomastiki kwa vile ina uwezo wa kuzalisha taaluma zingine. Kazi ya mtaalam huyu ilikuwa faafu katika utafiti wetu kwa vile mtaalam huyu anasisitiza kuwa sababu ya kiumbe chochote kile kupewa majina ni kurahisisha mawasiliano, jambo lililousaidia utafiti huu kupata mwanya wa kuchunguza namna ambavyo vipashio vya lugha mathalan nomino katika majigambo ya Waisukha husawiri sifa za kiubabe.

Msingi wa maelezo ya wataalam hawa yaliufaa utafiti wetu kwa vile ulitusaidia katika kuhakiki na kupambanua vipashio vya lugha mathalan nomino katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha ili kusawiri ubabedume. Taashira hizi zilibainika kupitia kwa majigambo mbalimbali yaliyosheheni sifa za ubabedume kama vile ushujaa kupitia kwa majina ya majazi ama lakabu yaliyopewa fahali walipokuwa wakipigana kama vile Spana, *tsinziga*, bundi, Emini, Osama, 'Master key' na Mike Tyson miongoni mwa mengine. Kwa kurejelea majina haya, kwa mfano kila mtu ulimwenguni anajua jinsi Osama alivyokuwa shujaa katika masuala ya ugaidi na ndiposa ubabedume katika jamii ya Waisukha umesawiriwa kupitia kwa majina kama haya yanayojulikana kama majina/animonimu.

Ubabedume pia ulidhihirika pale ambapo akina mama hawakuruhusiwa kuwepo karibu sana na sehemu hiyo ya upiganishaji fahali, hii ni ishara kuwa wanaume katika jamii hii wanamiliki madaraka kuliko wanawake.

### **2.3 Maana ya Majigambo**

Dhana ya majigambo kama ulivyo ubabedume ni tata. Dhana hii imezishughulisha kalamu nyingi na kuibua fasili tofauti tofauti. Cope (1968) ameandika kusanyo la mashairi ya Wazulu yanayoitwa “Izibongo” lenye maana ya sifa (wingi) na katika umoja humaanisha jina la ukoo. Kulingana na maelezo yake, anayeghani majigambo haya huitwa “imbongi”. Mashairi haya yamekitwa kwenye ujumla wa maisha ya Wazulu, hali inayodhihirisha kuwa kuyaelewa ni muhimu kuzama ndani na kuelewa mfumo wao wa kitamaduni na kijamii. Mashairi haya yanaakisi maiha ya kijamii na mazingira yalimotungwa, mathalan mito, milima, misitu na mabonde. Ndani mwa mashairi haya ng’ombe hutajwa sana kwa vile ni mifugo muhimu katika maisha ya Wazulu. Ingawa kazi hii inatofautiana na utafiti wetu kinadharia na kimadhumuni, ilitufaa katika kubainisha majigambo ya Waisukha na mfumo wa kijamii, itikadi na utamaduni wa jamii ya Waisukha kama malighafi muhimu ya kudhihirisha mahusiano ya kiuwezo na mamlaka katika jamii ya Waisukha.

Kunene (1971) alifanya utafiti kuhusu majigambo ya Abasotso, kazi ya mtaalam huyu imejikita sana katika vitendo vya kishujaa kama malighafi muhimu ya majigambo aliyoyahakiki. Katika majigambo ya Abasotso, huwa kuna uamilifu wa kutukuza vitendo vya kishujaa, ujasiri, ushupavu, uhodari, weledi na umahiri katika vita. Mtaalam huyu anahoji kuwa hali kama hizi zilitokana na vita vya mara kwa mara, safari za usasi, mapambano ya mara kwa mara na wanyama pamoja na hatari nyinginezo. Kunene anadhukuru kuwa mazingira yaliyojaa uhasama huwa ni mchango mkubwa sana kwa majigambo. Kazi ya Kunene ilikuwa faafu katika utafiti huu kwa vile ilitusaidia

kutathmini jinsi vipashio vya lugha na tamathali za semi husawiri ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* miongoni mwa Waisukha. Katika kazi yake, Kunene anadhihirisha mbinu mbalimbali mathalan; taswira, usambamba, takriri-konsonanti na tanakali za sauti.

Chacha (1997) akiyaunga mkono mawazo ya Kunene anaeleza kuwa asili ya majigambo ya Batsotso ni vitendo vya kishujaa kama vile uhodari, ushupavu na umahiri wa vita. Inawezekana kuwa mazingira yaliyojaa vitendo vya uhasama ndiyo yaliyochangia katika matumizi ya majigambo.

Hodza (1979) alitafitia jamii ya Washona. Ameelezea aina mbalimbali ya majigambo ya jamii hii kama vile; majigambo ya nasaba, majigambo ya kibinafsi na majigambo ya majivuno. Aliyachambua majigambo hayo kifonolojia na kimofolojia. Katika kazi yake, ameelezea kuwa majigambo haya ni sehemu muhimu ya utamaduni, mila na itikadi za Washona. Kazi yake ilikuwa mwafaka kwa utafiti wetu kwa vile utafiti wetu ulihusisha vipashio vya lugha kimofolojia, kisintaksia na kisémantiki. Utafiti wake uliusaidia utafiti huu hasa katika kuchanganua majigambo kinasaba kutegemea nasaba mbalimbali za Waisukha.

Nchini Kenya, ubabedume umedhihirika katika jamii mbalimbali kama vile, katika jamii ya Abakuria kuna majigambo ya wanawake na wanaume ambayo Matinde (2015) anayaita ‘Amabaiko’. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa jinsia ya kiume imesheheni ubabe. Katika jamii ya Waswahili, kwa mfano katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ubabedume umedhihirika kupitia kwa jamii ya Wagalla kuweza kumwomba

Fumo Liyongo mbegu yake miongoni mwa jamii nyingine. Mifano hii inaonyesha ushujaa na ubabe miongoni mwa jinsia ya wanaume (Mung'ahu na Kobia, 2016).

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa vivugo (majigambo) ni ghani la kujisifia. Anaongezea kuwa kwa kawaida hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe. Anasema kuwa kivugo hutungwa kwa ufundi mkubwa kwa kutumia mbinu kama jazanda, chuku, sitiari, vidokezi, ishara, takriri na wakati mwingine hata vina. Maelezo ya Mulokozi pia yalikuwa ya manufaa katika utafiti wetu kwa kuhakiki tamathali za semi kama vile jazanda na chuku katika majigambo ya Waisukha kwa mtazamo wa Kisemantiki.

Kulingana na Mwita (1997), majigambo ni sanaa ya unenaji iliyo na utendaji ambayo kwayo mtu hujinaki kwa kutangaza sifa zake. Anahoji kuwa majigambo ni sanaa ya ushairi ambayo hutumia uteuzi maalum wa maneno ili kuibua hisia zinazowaathiri wasikilizaji na kuwafanya wahisi uchungu au furaha. Anasisitiza kuwa kwa vile majigambo hutaja watu, mahali, makabila, koo mbalimbali, matukio maalum, mila na imani za jamii husika, inabidi historia na maarifa ya kiethnografia ya jamii tajwa zieleweke vyema kabla ya kuelewa majigambo hayo. Kauli za mtaalam huyu zilikuwa mwafaka kwa utafiti huu kwa vile katika majigambo ya Waisukha, fanani mjigambi huteua maneno maalum ya kutumia ili kuibua hisia kwa watazamaji au hadhira. Fanani hao hujinaki na kutangaza sifa zao kwa niaba ya wafu katika *Shilembe*. Semi za fanani hao ndizo zilizotusaidia katika uchanganuzi wa kazini yetu. Mtaalam huyu alituelekeza kutambua kwamba mbinu ya kiethnografia ni muhimu katika kukusanya data ya majigambo kutoka kwa majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*.

Jambo hili lilikuwa la manufaa sana kwa vile mtafiti aliweza kwenda kuishi na watafitiwa na kukusanya data ya kimsingi. Wamitila (2003) anachangia kwa kueleza kuwa majigambo ni aina ya maghani yanayohusu kujisifu au sifa. Aghalabu huhusu kutongoa utungo wa kujisifu kuhusiana na kitendo fulani, ushujaa, urijali au matendo muhimu. Anaongezea kuwa majigambo haya ni maigizo ambayo yanaonyesha kujigamba kwingi kwa mtu ambaye labda ni shujaa au ametenda mambo ya kishujaa au yenye uzito fulani. Mtaalam huyu anadai kuwa watu wanaopatikana katika majigambo ndio watambaji au wasimuliaji wa majigambo yenyewe. Kwa hivyo, ni kawaida ya majigambo kuwa na lugha nzito iliyojaa tamathali zenye taswira au picha za undani na yenye hisia na mawazo mazito. Anasema kuwa mtambaji au fanani anaweza kujitapa kwa jambo lolote. Wanjala (2011) anasema kuwa majigambo ni maigizo yanayotoa mwanya kwa wahusika kujisifu kwa sababu ya matendo fulani ya kishujaa au mafanikio katika nyanja fulani za maisha.

Sifa za majigambo zimefafanuliwa na Wanjala kama zifuatatazo:

Kwanza, wahusika huigiza kwa kutumia lugha nzito ya tamathali, picha na taswira zenye mawazo mazito. Pili, huwa na matumizi ya chuku. Tatu, majigambo husaidia kuelimisha, kuadilisha na kuhifadhi mila na kuzipokeza kwa vizazi vipya. Nne, majigambo hujitokeza katika sherehe mbalimbali tohara (*khubita* na *khulonga* katika jamii ya Wabukusu), mazishi na maonyesho ya kisanaa. Kazi ya Wanjala ni msingi bora kwa utafiti wetu kwa vile tulipata mwanya wa kuyahakiki majigambo kwa kujikita katika tamathali za usemi kama jazanda na chuku. Sifa hizi pamoja na mawazo ya wataalam hawa yalikuwa msingi mwafaka kwa utafiti huu.

Matinde (2015) alifanya utafiti kuhusu Uchanganuzi wa Ubabedume katika Majigambo ya Abakuria. Alitafitia sherehe kama vile tohara, arusi na ukeketaji. Anaeleza kuwa , majukumu mbalimbali wanayopewa watoto wavulana na wasichana katika jamii hii husaidia katika kujenga ruwaza mbalimbali za kihusiano zinazosababisha wanaume kusawiriwa kama walio na mamlaka juu ya wanawake. Jambo hili liliusaidia utafiti huu katika kuyatalii majukumu wanayopewa wasichana na wavulana Waisukha ili kupata msingi kuhusu usawiri wao wa ubabedume (Taz. Kiamb. E Maswali; 9, 10 na 11) Matokeo ya utafiti wake ni kuwa vipashio vya lugha, uwezo, historia, imani na itikadi za mfumo-dume hujenga, hushamirisha na kuhalalisha ubabedume katika jamii ya Abakuria. Mtafiti huyu alitumia nadharia mbili; ya Uwezo-Uume na pia Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ambao utafiti wetu unauita Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (UCHAMAWADI) kama anavyodai Choge. Utafiti huu unakaribiana na utafiti wetu ila malengo yake ya utafiti ni tofauti na yetu. Aliyachanganua majigambo ya Abakuria ilhali utafiti huu uliyachanganua majigambo ya Waisukha. Matinde alitumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi iliyo sawa na nadharia yetu ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ila aliuchukua mkabala wa Usemi, mtazamo wa kihistoria uliopendekezwa na Wodak (1996 na 1999). Utafiti wake ulipeana mwanya kwa utafiti wetu kwa vile ulitusaidia katika kutambua namna ya kuweza kutumia nadharia mbili kwa ajili ya kujengana na kukamilishana ili kuzua mwingilianotaaluma.

Wataalam hawa wote wanashabihiana katika kutoa maana kwa vile wote wanaelezea kuwa majigambo huhusika na matendo ya kishujaa katika jamii mbalimbali za Kiafrika. Katika muktadha huu, mawazo ya Wamitila (2003) na Wanjala (2011) na Matinde (2015)

yaliufaa sana utafiti huu kwa vile, mathalan Wanjala anafafanua kuwa majigambo hayahusu tu ushujaa bali hujikita katika kudhihirisha mafanikio katika nyanja fulani za maisha. Wamitila anaongezea kuwa kuna matumizi ya lugha kisanaa katika lugha ya majigambo. Hali iliyodhihirika katika majigambo ya Waisukha hasa tulipoangazia kipengele cha kiisimu; kisemantiki. Matinde anashadidia kwa kusisitiza umuhimu wa kufahamu historia ya jamii fulani ili kuweza kuyachanganua majigambo vizuri. Lililo muhimu katika mawazo hayo ni ile hali ya majigambo kuweza kutoa mwanya kwa wahusika kujisifu kwa sababu ya matendo fulani ya kishujaa na matumizi ya lugha kisanaa, hali iliyobainika wazi katika majigambo ya Waisukha katika miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* fahali walipokuwa wakipigana huku fanani wakijigamba.

Kutokana na tafiti mbalimbali ambazo tumezipitia, ni wazi kuwa mada hii haijafanyiwa utafiti, hususan jinsi utanzu wa majigambo husawiri na kudumisha ubabedume katika jamii ya Waisukha kwa kushughulikia miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Ingawa hivyo, maandishi mengi tuliyoyadurusu yalitusaidia pakubwa katika kuuwekea utafiti huu kitovu na pia katika kukusanya na kuchanganua data kulingana na malengo yetu ya utafiti. Kazi za wataalam hawa zimekuwa nguzo kuu kwa utafiti wetu kwa vile zimetusaidia kubaini ni yepi yamefanywa na watafiti wengine wa awali ili kujua mwelekeo ambao utafiti wetu ungefuata na kutuwezesha kuliziba pengo lililoachwa na watafiti watangulizi.

#### **2.4 Tafiti zilizofanywa kuhusu ubabedume**

Sehemu hii imebainisha wazi kazi mbalimbali ambazo zimedhihirisha umuhimu wa itikadi na tamaduni za jamii mbalimbali katika jitihada zao za kujenga na kudumisha

ubabedume. Baadhi ya kazi hizi zimeshughulikia jamii za Waswahili ama Waisukha lakini kwa malengo tofauti na nyingine zimeshughulikia jamii nyingine kwa lengo tofauti na utafiti huu.

Itikadi ni mfumo wa fikra na imani katika jamii ambazo kwa njia moja au nyingine hutawala hali na muktadha mahsusi katika kipindi fulani cha kihistoria na huendelezwa na tabaka au kundi fulani lenye uwezo katika nyanja kama vile kiuchumi, kisiasa, sanaa, dini na sayansi (Ssettuba 2002). Coward & Ellis (1977) wakiunga mkono kauli hii wanaeleza kuwa itikadi ni mfumo changamano na wenye ukinzani na ishara kama usemi, taswira na visasili ambavyo kwayo tunajihisi katika mahusiano na wengine katika jamii tunamoishi. Itikadi ni dhana ambayo haiwezi kutenganishwa na ubabedume. Itikadi hubainika katika ugawaji wa majukumu kiuana.

Kulingana na Kirsten na Svensson (1988), majukumu yanayohitaji nguvu nyingi na yenye thamani hutengewa jinsia ya kiume ilhali yale madogomadogo na yanayohitaji nguvu kadri huachiwa wanawake. Mwanamume ndiye humiliki fahali wanaotumiwa katika upiganaji na kwa hivyo amepewa majukumu yote muhimu na ya hadhi yanayoandamana na ufugaji wa ng'ombe. Thamani ya fahali katika jamii ya Waisukha huenda sambamba na thamani inayoandamana na umenke au jinsia ya kiume.

Katika misingi ya ndoa, Kirsten na Svensson wanabainisha uwezo na madaraka makubwa anayomiliki mwanaume kwani ndiye aliye na jukumu la kupeleka mahali kwa kina mkewe. Kwa mfano, katika jamii ya Abakuria, kulingana & Matinde (2015), wasichana walijumuishwa katika hirimu ya vijana wa kiume waliotahiriwa hadi pale walipoolewa.



Baada ya kuolewa, msichana alijiunga na hirimu ya mumewe. Hali inayobainisha kuwa mwanamke ni milki ya mwanaume. Mwita (1997) anaeleza kuwa mvulana Mmaasai akitaka kuo, hata akikosa ng'ombe hujigamba kuwa, bora ana mkuki. Haya yanatudokezea sifa za kishujaa wanazozimiliki wanaume.

Kirsten & Svensson katika kumchora mwanaume wanapambanua maleba na mavazi ya wanaume, hali inayomsawiri akiwa kama mkakamavu, shupavu na shujaa. Kwa mfano katika baadhi ya michoro, kuna picha ambazo zinaonyesha mwanaume akiwa amejifunga kipande cha ngozi ya chui au simba. Kwingineko huchorwa akiwa na rungu, mkuki, ngao na sime, ambazo ni zana za kivita, hali hii ni ishara tosha kuwa ana jukumu la kulinda, kutetea na kupigania jamii yake. Kutokana na hali hii, ni wazi kuwa mila na desturi za Waisukha na Waswahili kwa jumla ni nguzo kuu katika kuuwekea msingi, kuujenga na kuukuza ubabedume. Matinde (2015) akikubakiana na mawazo ya Kirsten na Svensson (1988) anasema kuwa wajibu mkubwa wa mwanaume wa Wakuria ni kulinda jamii kutokana na maadui...mashambulio ya kupora ng'ombe kutoka kwa maadui wao yalichukuliwa kama suala la kawaida na muhimu. Vita na uvamizi huu ni matukio yanayodhihirisha ujasiri na ushujaa.

Kazi hii imejikita zaidi katika utamaduni, imani, mila na desturi, itikadi na falsafa pamoja na mitazamo ya Waswahili, hali ambayo ni tofauti na utafiti wetu. Ingawa hivyo, kazi hii iliufaa utafiti huu katika kuonesha historia na hali ya maisha ya jamii ya Waisukha kwa jumla. Ulikuwa mchango mkuu katika kutathmini namna ambavyo ubabedume husawiriwa, hukuzwa na kudumishwa kupitia kwa historia ambayo ni sehemu muhimu ya fasihi.

Baadhi ya wataalam miongoni mwao wakiwemo Mitchell na Coltrane (2005) wakiunga mkono mawazo ya Weiss (1910) wanaelezea umuhimu wa historia na utamaduni wa jamii katika kuweka msingi, kujenga na kukuza uwezo wa jinsia ya kiume. Wataalam hawa wanakubaliana kuwa, familia ni asasi muhimu katika uzalishaji na ukuzaji wa thamani za kijinsia. Ni katika familia ambapo wavulana huweza kutambua fadhila za hadhi yao ambazo huwapa uwezo na mamlaka katika jamii. Hata hivyo, kazi ya wasomi hawa inatofautiana na utafiti huu kwa misingi ya nadharia na mielekeo yake na kuwa jamii lengwa yao ilikuwa Abakuria. Ingawa hivyo, kazi ya wasomi hawa ilitufaa sana katika kuelezea mchango wa utamaduni katika kujenga na kukuza ubabedume. Kazi yao ilikuwa mchango muhimu wakati wa uchanganuzi wa data ya fasihi imulizi kwa kutumia mtazamo wa kiisimu, semantiki.

Naye Hanke (1998) anabainisha jinsi ambavyo runinga huchangia kupitia kwa picha na mazungumzo katika kukuza ubabedume. Mawazo haya yameshadidiwa na Matinde (2015) ambye alifanya utafiti kuhusu uchanganuzi wa ubabedume katika majigambo ya Abakuria. Matokeo yake yalikuwa kwamba majigambo ya Abakuria huakisi na kushamirisha mfumo-dume. Utafiti wa wataalam hawa ulikuwa mchango mkuu katika utafiti huu kwa vile ulituwekea msingi wa dhana ya ubabedume katika jamii. Tafiti hizi zote zinadhihirisha wazi jinsi ambavyo utamaduni na mazingira huchangia katika kukuza uwezouume unaojengeka katika fahamu za wanajamii. Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke katika jamii na vilevile uhusiano kati ya mwanamume na mwanamume mwenzake. Katika muktadha huu, utamaduni wa Waisukha, kupitia kwa lugha, vitendo vya fanani na sherehe na miviga ya *Shilembe* na

*Mchezasili* wa *Mayo* ziliuwezesha utafiti huu kutambua umuhimu wa utamaduni na mchango wa mazingira katika kuukuza ubabedume.

## **2.5 Tafiti zilizofanywa kuhusu majigambo, miviga na taaluma nyingine**

Kama tulivyotaja, majigambo ni sehemu ya Fasihi Simulizi inayopatikana katika mgao wa ushairi. Ni sanaa semwa ambayo ni kielelezo cha fasihi katika jamii za Kiafrika. Inasikitisha kwamba Wazungu walipowasili, hawakutambua kuwa hiyo ilikuwa sanaa ya ushairi na hata wengine kama Burton wakadai kwamba Waafrika hawakuwa na tendi (Finnegan, 1970 na Knappert, 1979). Majigambo yaliyohakikiwa ni yale ya kisimulizi. Kwa sababu ya kule kutoandikwa kwa sanaa hii, maumbo au maneno yake hugeukageuka kutegemea na sherehe au wakati yanapokaririwa. Wanjala (2015) anakubaliana na kauli hii anaposema kuwa tanzu za Fasihi Simulizi hujinyambua.

Majigambo hutegemea uteuzi wa maneno na ubunifu wa fanani katika jamii husika. Msanii huwa na uhuru wa kuteua maneno, nahau, vifungu vya maneno, uradidi, mpangilio wa beti, kubadilisha ploti na kadhalika. Mwita (1997) alishughulikia majigambo ya Kikuria kwa kujikita katika mtazamo wa Kiisimu na alitumia nadharia ya Umuundo na Semiotiki. Matokeo ya utafiti wake yakawa, majina ya majisifu ni vipashio vya kimsingi katika majigambo. Majina hayo huundwa kwa vipengele mahsusni vya kifonolojia na kimofolojia yanayopatikana katika lugha ya Kikuria. Utafiti wake ulipeana mwanya kwa utafiti huu kwamba taaluma ya Isimu inaweza kuoanishwa na ya Fasihi Simulizi ili kuzua mwingilianotaaluma. Ingawa nadharia na malengo ya utafiti wa mtaalam huyu yanatofautiana na ya utafiti wetu, tulifaidika kwa kupata mwelekeo wa kuchunguza ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa

*Mayo* kwa kujikita katika mtazamo wa Kisemantiki, na pia ile hali ya kushughulika taaluma mbili katika kazi moja.

Majigambo ya Wajaluo kwa mujibu wa Wanjala (2011) hutokea wakati wa matanga. Wazee na vijana huwa wamebeba mikuki na ngao huku wanawake wakipiga mayowe. Msomi huyu anaeleza kuwa suala hili la kujigamba hutokea hasa kwa watu wenye umri mkubwa wanapokata kamba. Anaongezea kuwa, majigambo katika jamii ya Waha hususan katika sherehe za kulipa mahari yanaweza kutolewa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza huwa ni wakati wa kuuliza, kupokea au kupeleka mahali. Mawazo ya Wanjala kuhusu majigambo yanaonyesha kuwa ni vyema kuuelewa utamaduni wa jamii husika ili uweze kuyaelewa majigambo. Jambo hili lilikuwa nanga muhimu katika utafiti huu kwa vile lilitusaidia kuuelewa utamaduni, mila na itikadi za Waisukha ili kutuwezesha kuyaelewa majigambo yao.

Tafiti hizi ni msingi mwafaka kwa utafiti huu kwa vile utafiti wetu ulilenga kuchunguza ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* miongoni mwa Waisukha kwa kutumia mtazamo wa kiisimu. Miviga ni sherehe zinazofanywa katika jamii yoyote teule na hufungamana na tamaduni za jamii husika pamoja na matambiko ya aina yake. Tafiti nyingi zimeshughulikia miviga na kubainisha sifa zake.

Kulingana na Matei (2011), dhana ya miviga inarejelea sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalum cha mwaka. Mara nyingi, miviga kama vile jando hufanywa katika kipindi maalum baada ya mavuno. Miviga ya mazishi, kwa mfano, hufanywa kabla ya wakati fulani wa siku kutegemea imani ya jamii husika.

Miviga ya kuwapa watoto majina huadhimishwa muda fulani baada ya mtoto kuzaliwa. Matei alitusaidia kutambua jinsi dhana ya miviga inatofautiana kutegemea jamii husika. Kauli hii ilikuwa faafu kwa utafiti huu kwa vile miviga ya *Shilembe* na *Mayo* katika jamii ya Waisukha ni tofauti sana na miviga za jamii nyingine. Kwa mfano, katika jamii hii ya Waisukha, wakati wa miviga ya *Shilembe*, mashujaa watarajiwa hubeba mikuki, rungu na zana nyingine za vita na kupiganisha fahali katika kaburi la mfu. Hali hii hufanyika katika tukio maalum kama anavyosisitiza Matei.

Naye M’Ngaruthi (2008) anasema kuwa, miviga au mivigha ni sherehe maalum zifanywazo katika jamii katika vipindi au majira maalum ya mwaka. Sherehe za aina hii huandamana na nyimbo, uchezaji wa ngoma, ukariri na uimbaji wa mashairi, utegaji na uteguaji wa vitendawili na mafumbo, matumizi ya semi, sanaa za utendaji (uigizaji) na tambiko. Anaelezea kuwa, miviga mara nyingi hunuiwa wanajamii ambao ‘wanakomaa’ kutoka kwa kikundi kimoja hadi kingine. Tamasha za miviga pia hutendeka pale jamii inapopitia misukosuko ya kimaumbile au ya kibinadamu. Shughuli za miviga huweza kuandamana na mambo ya kisanaa pamoja na dua kwa Mungu au miungu. Wazo muhimu katika fasili za wataalam hawa ni kwamba miviga hufanywa katika kipindi maalum cha mwaka na huhusisha imani za jamii husika, jambo lililo muhimu kwa utafiti wetu kama nilivyokwisha kueleza.

Miviga inahusishwa sana na tamthilia pamoja na visakale na matendo ya kidini (Mulokozi, 1989). Barani Ulaya, tamthilia ziliweza kuhusishwa na miviga ya kidini katika jamii ya Wayunani au Wagiriki wa kale. Miviga hiyo iliambatana na maombi ya kuzaliwa, kuoza mpaka kufa na kubadili maumbile na kuwa binadamu tena. Kule India,

yaaminika kuwa chimbuko la miviga ni tamthilia zilizotokana na tenzi zilizoitwa Mahabharatana pamoja na miviga iliyoambatana na utendi wa tendi hizo katika mahekalu ya kidini. Barani Afrika, dhana ya mivigha ina ukuruba mkubwa na maigizo ya tamthilia yaliyopatikana Misri na yalihusu kufa na kufufuka kwa mungu wa Wamisri aliyejulikana kama Osiais.

Miviga katika jamii ni dhana ambayo haichukuliwi tu hivihivi kwa vile fasihi simulizi ina uhusiano mkubwa sana na dini. Huwezi ukatenganisha miviga, viviga vya jamii husika na dini. Beverline (2018) anaongezea kauli hii kwa kuunga mkono mawazo ya Were (1976) kwa kusema kuwa huenda ikawa sababu kuu inayoifanya jamii ya Waisukha kusemekana kuwa chimbuko lao ni 'misri'.

Wanjala (2015) alitafitia kuhusu miviga ya *embalu* katika jamii ya Babukusu. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba sherehe za tohara zimeratibiwa na ni matambiko yanayotokea kama drama. Sherehe hizi zinaafiki sheria na muundo wa tamthilia inayoanza kwa kuweka msingi wa mgogoro, kuukuza, kuuendeleza na hatimaye hufikia kileleni. Miviga hudhihirika pale ambapo kwa mfano, watahiriwa wanapowasili kwa wajomba, ng'ombe huchinjwa kama zawadi na *luliki* huwekwa shingoni kwa vile inaaminika kuwa hiyo ndiyo nyama iliyowasetiri wakiwa tumboni. Mtaalam huyu alishughulikia sherehe za *mwaka-kogwa*. Anafafanua kuwa sherehe hizi hufanywa visiwani Pemba na Unguja hasa eneo la Makunduchi lijulikanalo kama Kae Kuu ili kuukaribisha mwaka mpya. Huchukua takriban siku nne na ndugu wawili wawili kutoka Kaskazini na Mashariki humenyana kwa kutumia migomba. Mashabiki wa pande zote mbili hujiunga na wapiganaji na kusababisha uharibifu mkubwa wa ndizi katika eneo hilo. Vita hivi hutumiwa kama

ishara ya kuitakasa jamii na kuukaribisha mwaka mpya usiokuwa na kinyongo miongoni mwa wanajamii. Huu ulikuwa msingi faafu wa sherehe za miviga katika utafiti huu. Miviga ni muhimu katika utafiti huu kwa vile inaaminika kuwa kwa mfano miviga ya *Shilembe* inapofanyiwa katika makaburi ya wafu na fahali kuutandaza mchanga katika boma, husaidia roho ya mfu kupigana na roho za wanaume aliowaua ili aweze kupata kibali katika dunia ya mizimu (Kabaji, 2008).

Kwa mujibu wa Alembi (2002), miviga ya *Shilembe* katika jamii ya Wanyore huhusisha uharibifu wa mazingira yakiwemo ya migomba ya ndizi. Haya hutekelezwa siku ya mazishi ya mwanamume shujaa. Anaeleza kuwa wanaohusika hujipanga na fahali kwenye lango kuu na kufululiza mbio wakielekea upande wa nyuma ya nyumba kunakokuwa na migomba ya ndizi na mimea mingineyo. Migomba huawa inakatwa na kukanyagiwa chini pamoja na mimieaa mingine. Binadamu na fahali huhusishwa katika uharibifu huo. Uharibifu huu huashiria kupotea kwa mtu mashuhuri katika jamii hii. Baadaye, wahusika huelekea kaburini na kulitandaza kaburi la mwendazake aliyekuwa mwanamume mashuhuri katika jamii. Sifa ya kulitandaza kaburi na kutawanya mchanga kila mahali inasemekana kuwa muhimu kwa vile humpa shujaa nafasi ya kusameheana na watu aliowaua na pia inaaminika kuwa aliyeaga huandaliwa njia yake ya kuingia katika dunia ya pili.

Maandishi haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile yalipeana mwanya wa kulitafitia suala la miviga mintaarafu mila na tamaduni za jamii ya Waisukha kwa kujikita katika vipashio vya lugha kwa mtazamo wa Kisemantiki. Hii ni kwa sababu tafiti za awali zinaelekea kuegemea sana katika mtazamo wa Kiantropolojia, Kisosholojia na Kifalsafa.

## 2.6 Tafiti zilizofanywa kuhusu Waisukha

Kazi yoyote huwa inahusiana na mazingira ya kihistoria yanayomhusu mwandishi na jamii yake. Senkoro (1980) anaeleza kuwa historia ya jamii ndiyo chanzo na mwisho wa sanaa yoyote ile, ikiwemo fasihi. Fasihi na historia ni kama pande mbili za sarafu moja. Mawazo ya Senkoro yanawiana na ya wataalam wengine kama vile Firth (1890-1969) katika Choge (1997) wanapochangia kwa kusema kuwa lugha imeshehenezwa na utamaduni wa jamii husika. Wanashadidia kuwa ni vyema uchunguzi wa kipengele chochote kile cha lugha fulani uweze kufanywa kwa muktadha wa utamaduni unaosheheneza lugha inayochunguzwa. Kwa sababu hii, ilitubidi tuangalie historia ya Waisukha ili kuelewa Fasihi Simulizi yao kupitia kwa lugha inayotumiwa katika majigambo na miviga yao ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*.

Kulingana na Fasihi Simulizi ya Waisukha, yamkini koo zao hazikuwa na chimbuko moja. Kila moja inatoa kisa tofauti. Ingawa hivyo, kila moja inakubaliana kuwa Waisukha na Waidakho ni kama binamu. Inaaminika kuwa, chimbuko lao lilikuwa Misri, sawa na Waluhya wengine. Haijulikani wazi 'Misri' wanayoitaja ni nchi gani. Linalojulikana tu ni kuwa ilikuwa Kaskazini mwa Afrika Mashariki. Waisukha ni miongoni mwa Waluhya hawa; Wabukusu, Wanyala, Watachoni, Wakabras, Watsotso, Waidakho, Wamaragoli, Wawanga, Watiriki, Wanyore, Wakhayo, Wasamia, Wakisa na Wamarama. Waisukha wanapatikana katika Kaunti ya Kakamega, eneo bunge la Shinyalu. Waisukha wanapatikana katika eneo la Mashariki ya Kati ya Kakamega. Kwenye upande wa Mashariki, Waisukha wamepakana na Wanandi na kwenye upande wa Kaskazini, wamepakana na mji wa Kakamega. Waisukha wana koo nyingi



zinazoelekea kufanana na zile za Waidakho kama vile; Vakhayo, Vamilonje miongoni mwa koo nyingine, (Anzumbu 2018).

Dhana ya ukoo au nasaba ilikuwa muhimu sana katika jamii ya Waisukha kabla ya Ujio wa Wakoloni nchini Kenya. Katika enzi hizo, jamii hii iligawanywa kinasaba na hakukuwepo na hali ya mamlaka maalum ya kiofisi. Mwishoni mwa karne ya 19, kikihusisha kipindi cha ukoloni hadi wakati wa sasa, jamii ya Waisukha imepitia kipindi cha mabadiliko kijamii. Mifumo ya serikali kuu na ile ya kijamii imesababisha mabadiliko makubwa katika kiwango cha kijiji. Hata hivyo, nasaba za Waisukha ni takriban ishirini na saba. Nazo ni; Vayokha, Vitsende, Varuli, Vakhaiwa, Vamilonje, Vamakhaya, Vimalia, Vichina, Vamahalia, Vashitaho, Vakhulunya, Vakusi, Vakondi, Varimbuli, Vasulwa, Vaterema, Vasikhovu, Vakhombwa, Vatula, Vashilitsa, Valila, Vasakala, Vashilukha, Vashimutu, Vateheli, Vatsunga na Vasalwa. Kuna nasaba nyingine za jamii hii ambazo ni ndogo sana kiasi kwamba hujificha kwenye vivuli vya maeneo ya nasaba zile kubwa ambazo nimezitaja ingawa utambuzi wao bado upo Mifano ya hizi nasaba ndogo ni kama vile Vashiheli wanaopatikana katika eneo la ukoo wa Vatsunga.

Pia kuna nasaba ndogo ya Vakhonyi inayopatikana kwenye eneo la Vateheli na Vashikali kwenye eneo la Vitsende. Idadi kamili ya hizi nasaba ndogondogo katika jamii ya Waisukha bado si dhahiri (Were, 1976). Kinachotofautisha eneo la nasaba moja na nyingine huweza kuwa mto, njia au mahali palipojaa kidimbwi cha maji au nyua zinazoonyesha mipaka ya mashamba yao au vijiji vyao. Kila mpaka umejulikana wazi na wenye ukoo husika. Hali hii ni muhimu katika jamii ya Waisukha kwa vile kila ukoo

huwa na sifa zake bainifu zinazotofautiana na ukoo mwingine. Kwa mfano, ukoo wa Varuli umejulikana kama *viranyi* ambao ni weusi na wanafanya kazi ya uhunzi. Sanaa hii inahusishwa sana na mahali pao pa awali panapoitwa Samia kabla ya kuhamia walipo sasa. Ingawa hivyo, watu wachache sana katika ukoo huu ndio wanaoishughulikia sanaa hii.

Kwa upande mwingine, nasaba ya Vayokha inayojulikana kama *vashieni* au matabibu, ni ukoo unaosheheni sifa za kiganga na kwa hivyo wana nguvu za kutibu magonjwa mbalimbali. Katika hali hii, ukoo wa Vichina ambao unajulikana kama *valuvi* nao ulijishughulisha na kuvua samaki. Kwa hivyo waliifanya kazi ya uvuvi. Haya ni kwa mujibu wa masimulizi ya mmoja wa wasailiwa kutoka katika jamii hii, ukoo wa Vateheli (Shitekha 2018). Hata hivyo, anaeleza kuwa jambo lililo na mfanano katika jamii hii ni dhana ya miviga ya *Shilembe* na *Mayo* iliyo na misingi yake kule Misri ambako kunaaminika kuwa asili ya Waisukha (Were 1976).

Katika muktadha huu, historia ya Waisukha ni muhimu katika majigambo kwa vile ni mojawapo ya maudhui ambayo fanani anaweza kujinaki juu yake, kwa mfano, anayeonea fahari nasaba yake husimulia historia yake katika majigambo kwa kuyahusisha na historia ya kabila lolote. Nasaba za Waisukha pia ni muhimu kwa vile wao hujigamba kutegemea nasaba zao husika. Kuna zile nasaba ambazo ni mashuhuri katika majigambo na huheshimiwa na kupewa hadhi pamoja na fahali wao ilhali kuna wale wanaojigamba kwa kiasi na pia kuna wale wa hali ya chini. Lugha ni kipengele muhimu kwa vile hubeba utamaduni wa jamii husika. Khaemba (2013) ameshughulikia ubabedume na ujenzi wake katika miviga ya jamii ya Wabukusu. Alichunguza tohara, mafunzo kwa

vijana waliotahiriwa jandoni na sherehe inayofanywa siku tatu baada ya mazishi ya mzee mkongwe. Matokeo ya utafiti wake yalikuwa kwamba ubabedume ni dhana ambayo hujengwa na kuendelezwa na itikadi ambazo huikweza jinsia ya kiume na kuidhalilisha ya kike. Mtaalam huyu ameonyesha namna wanaume hutumia njia mbalimbali za unenaji kuchipua, kukuza na kuendeleza mamlaka yao katika jamii. Kazi ya Khaemba ni nguzo kuu katika utafiti huu. Ingawa alishughulikia utanzu tofauti wa Fasihi Simulizi katika jamii ya Wabukusu iliyo tofauti na jamii ya Waisukha, kauli zake zinazohusu ujenzi na udumishaji wa ubabedume zilikuwa mwafaka katika kuuwekea msingi utafiti huu. Majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* ya Waisukha yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile yalipeana fursa kwa mtafiti kutumia kipengele cha kiisimu ambacho ni semantiki na kuweza kubaini ubabedume unavyosawiriwa. Kwa hivyo, huu ulikuwa msingi bora katika utafiti huu.

## **2.7 Tafiti kuhusu kipengele cha kiisimu: kisemantiki**

Lugha kama mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na binadamu katika mawasiliano huchanganuliwa na taaluma ya isimu. Taaluma ya Isimu ina matawi mbalimbali kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Utafiti huu ulijikita katika mtazamo wa kisemantiki. Kulingana na Crystal (1987), semantiki au isimu maana ni utanzu wa isimu unaochunguza lugha. Habwe na Karanja (2004), wakiyaunga mkono mawazo ya Crystal wanaelezea kuwa isimu maana ni utanzu wa hutafiti maana za mofu, unaochunguza maana katika lugha ya binadamu. Utanzu huu hutafiti maana za mofu, maneno na tungo. Kutokana na fasili za wataalam hawa, ni wazi kuwa maana ni kipengele muhimu katika uchunguzi na uchanganuzi wa lugha ya mwanadamu. Maelezo ya dhana hii ni muhimu

katika utafiti huu kwa vile ulijikita katika kuchunguza vipashio vya lugha kama vile nomino, vishazi na vitenzi ili kubaini namna ubabedume unavyosawiriwa katika majigambo ya Waisukha. Aidha, utafiti ulichunguza tamathali za semi kwa mtazamo wa kisemantiki.

Mbiti (1967) anaeleza kuwa suala la maana ni muhimu sana katika lugha. Anahoji kuwa, karibu anthroponimu zote za Kiafrika zinabeba maana. Kulingana na mtaalam huyu, anthroponimu zinaweza kuakisi wakati, misimu, tukio au mahali alipozaliwa mtoto. Kwa mfano, katika jamii ya Wanandi, mtoto mvulana akizaliwa wakati kunaponyesha ataitwa Kiprop kutokana na nomino rop inayomaanisha ‘mvua’ au Kiprobon kutokana na kitenzi robon inayomaanisha ‘nyesha’ . Katika lugha ya Dholuo, anthroponimu hii huwa ni Akoth kurejelea msichana na Okoth kurejelea mvulana. Katika Kibukusu, anthroponimu hii ni Wafula kwa wasichana na Nafula kwa wavulana. Mbiti hakujikita katika utamaduni mmoja bali alishughulikia jamii mbalimbali. Kwa mfano alionyesha vile Wakamba na Washona wanavyowapatia watoto wao anthroponimu. Utafiti wake haukushughulikia uhakiki wa vipashio vya lugha katika majigambo bali ulijikita tu katika maana za anthroponimu. Hata hivyo, utafiti wetu ulichota dhana ya maana kutoka kwake na kutusaidia katika kuvihakiki vipengele vya lugha pamoja na tamathali mbalimbali za usemi mathalan chuku na jazanda kwa mtazamo wa kisemantiki.

Kibigo (2015) alitafitia Matumizi ya Ngeli miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kwa kuchunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi hao kutegemea mwaka wa masomo. Utafiti wake ulijikita katika vipengele vya kiisimu vya uainishaji ngeli kama vile imofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Matokeo ya utafiti wake

ni kwamba wanafunzi hao walikuwa na umilisi na utendaji kutegemea mambo mengi na athari mbalimbali kama vile athari ya lugha ya Sheng'. Ngeli ni msingi wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huo ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ulitusaidia kutambua jinsi uainishaji wa ngeli kisemantiki hujikita katika misingi ya maana. Kwa hivyo, utafiti wa mtaalam huyu unaonyesha umuhimu wa kutambua fahiwati mbalimbali katika tungo mbalimbali kama vile uchunguzi wa ubabedume katika majigambo ya Waisukha ulivyobainika kupitia kwa nomino na tamathali mbalimbali za semi.

Kerubo (2015) alishughulikia Uwazi na umaanisho: Usimbaji maana katika Ekegusii na Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa uchanganuzi wa misimbo mbalimbali ulidhihirisha tofauti za uteuzi wa kategoria za Semantiki ambazo ni za kileksika na kimuktadha. Maana zilizosimbwa zilibainisha maana kadha wa kadha. Tafiti hizi zilikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa vile vipengele vingine vya kiisimu ni msingi muhimu kwa taaluma ya Semantiki. Hali hii ilikuwa muhimu katika utafiti wetu ingawa ulijikita katika fasihi simulizi kwa kutumia mtazamo wa kiisimu.

Udurusu wa maandishi haya umekuwa wa manufaa katika utafiti huu kwa vile ulisaidia katika kuyapanua maarifa yetu kuhusu utanzu wa majigambo ya Waisukha katika upekee wake. Maandishi haya yametusaidia katika kubainisha tafiti ambazo zimefanywa na wengine ili kuupa utafiti wetu mkondo wa kuufuata na kuweza kuliziba pengo lililoachwa na watafiti wa awali.

## **2.8 Tafiti zilizofanywa kuhusu nadharia za utafiti huu**

Kulingana na Wanjala (2011), utafiti wa fasihi simulizi unaweza kuongozwa na nadharia moja au zaidi kutegemea malengo ya utafiti husika. Katika msingi huu, utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili za Uwezo-Uume (Izugbara, 2005) na nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (Wodak, 1996).

### **2.8.1 Nadharia ya Uwezo-Uume**

Nadharia ya Uwezo-Uume iliasisiwa na Robert Bly (Wells na Holland, 2001) na kuendelezwa na Izugbara mnamo mwaka wa 2005. Nadharia ya Uwezo-Uume hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jamii ya jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Dhana ‘mwanaume’ ipo kwa misingi ya kibiolojia ilhali “ubabedume” au “uanaume” hutokana na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii husika. Ubabedume huzaliwa na kukuzwa na utamaduni na pia huhalalishwa kwa njia, hali na nyakati tofauti za jamii husika. Chimbuko la nadharia hii hufungamanishwa na *dhakari* na wenye kuimiliki hujamiishwa katika jamii kama rasilmali yenye manufaa makubwa kwa jamii. Mwanaume huchukuliwa kuwa na nguvu, mwenye kuheshimiwa na kupewa hadhi katika jamii. Hivyo basi, mwenye dhakari siku zote hupewa hadhi ya juu na kuchukuliwa kuwa bora zaidi ya wale ambao hawana kiungo hiki (wanawake). Hali hii inatuelekeza kutambua kwamba, sura ya wanaume hujengwa kutokana na matarajio ya kiitikadi na kitamaduni kuwahusu. Haya ndiyo husababisha baadhi ya sifa zinazosisitizwa kama vile, ubabe, stahamala, ujasiri na ukatili katika kutenda bila kujali iwapo vitendo hivyo vitaleta maangamizi au vurugu katika jamii. Izugbara (2005:13) anafafanua:

*Umbo la dhakari la ubenuzi na hali ya kutokuwa na haya ikishirikishwa na uwezo wa dhakari kuwa ngumu, kubwa, thabiti na yenye nguvu wakati wa mchechemo ni dhihirisho kwa mawazo asili kuwa dhakari ina uwezo!...shahawa ambayo inatoa kipindi cha tendo la ngono huonekana kama sumu ambayo humdhoofisha mwanamke, Anasema kuwa dhakari imetawazwa na umuhimu wa uhai na ufu...matokeo muhimu huhusishwa na amali ya dhakari na upenyezi wake katika kupoteza ubikira na kutia mimba, hali hii huitawaza dhakari uwezo juu ya uhai na ufu...*

Walsh (1997) anaeleza kuwa udume hubainika bayana kwa misingi ya uhuru wa kijinsia, ushari, ushindani na uwezo wa kutawala, kuamuru na kuzuia. Aidha, anaongezea kuwa katika jamii za Kiafrika, udume huhusishwa na uwezo wa kutawala, kuamuru na kuzuia. Mihimili ya nadharia hii ni:

- i. Itikadi za kijamii huongoza fikra hivi kwamba utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria (Wells na Holland, 2001).
- ii. Utamaduni, lugha, imani na desturi zimewawezesha wanaume kuwa watawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilmali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini (Collins, 1971, Sokoloff, 1980).
- iii. Majukumu kugawana kiuana, wanaume wameweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu wa kiume kwa manufaa yao wakizingatia kwamba mwanamume alipewa mwanamke kama mwenzi kutoka kwa “Mungu wa kiume” (Ruether 1974).

- iv. Sifa angama za uume na maeneo ya ubabedume yanayojitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo (Chafetz, 1974 na Doyle, 1985).

Mihimili hii imejikita katika utamaduni, itikadi za jamii, mgawanyo wa mamlaka na uwezo wa kijinsia, mielekeo na matarajio ya kijamii kumhusu kila mwanajamii. Mihimili hii iliongoza utafiti wetu wakati wa ukusanyaji data na uchanganuzi wa data na kuusaidia kufikia azma yake. Nadharia hii ilikuwa mwafaka katika utafiti huu kwa vile utanzu wa majigambo husheheni taasubi za kiume zinazodhihirishwa na vipashio mbalimbali vya lugha. Inaaminika kuwa taasubi hizi huwa zimejikita kwenye utamaduni, mielekeo na matarajio ya kijamii, itikadi, mazingira, falsafa na sifa anuwai za kila jinsia kutegemea utambulisho wake katika jamii. Hata hivyo, utafiti huu ulitumia mihimili mitatu tu, mhimili wa kwanza wa itikadi, wa pili unaohusu utamaduni na wa nne unaoangazia sifa angama za uwezo-uume. Hali hii ilikuwa muhimu ili kuuwezesha utafiti kukidhi matakwa ya lengo la tatu kuhusu kuchunguza nafasi ya lugha, historia na itikadi za Waisukha katika kujenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume.

### **2.8.2 Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi**

Nadharia ya pili iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi iliyoasisiwa mnamo mwaka wa 1990. Waasisi wake ni pamoja na Teun van Dijk, Norman Fairclough, Gunther Kress, Theo van Leeruwen na Ruth Wodak. Msingi wa nadharia hii ni kazi mbalimbali za waasisi hawa. Nadharia hii ina misingi yake katika



sanaa ya Unenaji, Matumizi, Isimu Jamii, Isimu Matini na Isimu Amali au Isimu Pragmantiki. Dhana za itikadi, uwezo, mgawanyo msonge wa majukumu na uana ama jinsia huchukuliwa kama vibadiliki vya msingi katika ufasiri na ufafanuzi wa usemi au matini. Miruka (2014) alishughulikia Maumbo ya Fasihi Simulizi katika Mashairi Andishi ya Kiswahili. Mtaalam huyu ametumia mifano anuwai kama vile nyimbo, hadithi na nahau kuonyesha jinsi maumbo ya fasihi simulizi yanavyobainika katika fasihi andishi. Matumizi yake ya madondoo mbalimbali na uchanganuzi wake wa kina uliupatia utafiti huu mwelekeo wa kuyachanganua majigambo ya Waisukha kwa kina zaidi ili kuweza kubaini vipashio vya lugha vinavyobeba ubabedume. Matokeo yake yalikuwa kwamba kuna mwingilianomatini kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Ingawa utafiti wake ulikuwa na madhumuni tofauti na utafiti huu, kazi yake ina mchango maalum katika tasnifu hii kwa sababu mtaalam huyu anahoji kwamba usemi ni masimulizi yaliyohifadhiwa katika matini. Kauli hii inakaribiana na ile ya Fairclough (1993) anayeeleza kuwa matini ni lugha katika hali ya mazungumzo au maandishi kama inavyotumiwa katika muktadha wa usemi. Mawazo ya Miruka yalituongoza katika kuchunguza kwa kina dhana hizi: Diskosi na Makinifu ambazo ni dhana za kimsingi katika nadharia hii ya UCHAMAWADI.

#### **2.8.2.1 Dhana ya Diskosi**

Fairclough (1995) anatofautisha diskosi na lugha akieleza kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano ilhali diskosi ni njia ya kubainisha kitendo fulani cha kijamii dhidi ya mwelekeo fulani. Mills (1997: 2) anaeleza kuwa diskosi ni usemi, mazungumzo au mawasiliano kuhusu dhana fulani ilhali Halliday (1985) anatumia diskosi kurejelea matini.

Tafiti nyingi zimetumia dhana hii ya diskosi kurejelea mawasiliano simulizi na andishi. Matumizi ya lugha andishi na semwa huzua utofauti katika ufasili na ufasiri wa maana kwa vile hutegemea lugha inayotumiwa na miktadha husika (Cameron 2001). Haya yanarejelea uamilifu kwa sababu ya kazi ambayo lugha hutekeleza. Fairclough (2003) anadokeza kuwa uamilifu wa diskosi huweza kufasiriwa kwa njia mbili: kama kipengele cha maisha ya jamii na pia kama njia za kuiona dunia (Sunderland 2004). Foucault (1975) akiungwa mkono na Fairclough (1990) anahoji kuwa diskosi ni matendo yanayoratibu kile kinachosemwa. Utafiti huu, ulitumia ufasiri huu wa diskosi. Fairclough anachukulia diskosi kwa njia tatu: matini, zao la usemi na tendo la kijamii (Fairclough 1992). Hii ina maana kwamba tafiti anayetumia dhana ya diskosi hajikiti tu katika usemi bali pia hushughulikia matini wakati wa kuchanganua data kama ilivyodhihirika katika utafiti huu tulipoyarekodi majigambo, tukayafanyia ufasiri na tafsiri na hatimaye tukayachanganua.

#### **2.8.2.2 Maana ya ‘Makinifu’**

Nadharia hii ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi inasemekana kuwa *Makinifu* kwa vile inashikilia kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya itikadi na lugha ambao umejificha na matendo ya usemi au matini aghalabu hutumia vipashio vya lugha na kuviweka katika hali ya mazoea. Dhana ya umakinifu wa nadharia hii ndio huweka wazi itikadi katika diskosi na kudhihirisha taashira za kiuwezo na mamlaka (Fairclough 2015). Katika mchakato huo, huonyesha uhusiano kati ya lugha, itikadi na uwezo na kuweka wazi vipengele vilivyosetirika katika jamii. Dhana ya umakinifu inatuelekeza kutambua kuwa nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi haichukulii tu diskosi kijuujuu bali

huchunguza kwa umakinifu, uhakikifu na kwa jicho la ndani zaidi ili kutambua jinsi lugha, itikadi na mamlaka huwekwa wazi katika jamii husika. Choge anahoji kuwa kuna haja ya kuhakiki diskosi kwa kina na kwa jicho pevu ili matokeo yawe ya kutopendelea hali yoyote ile. Van Dijk (1993) anaeleza kuwa hakuwezi kuwa na njia moja ya kuchanganua diskosi wala njia moja ya wataalam kadhaa kuchanganua diskosi. Umakinifu ni hali ya kuwa na msimamo dhabiti kuhusu unachokichanganua au hata kuchukua msimamo wa kisiasa (Van Dijk 2001; Wodak 2007; Atanga 2010). Ninakubaliana nao kwa vile masuala ya ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* katika jamii ya Waisukha hayawezi kuchanganuliwa kwa mtazamo mmoja.

Nadharia hii hutazama usemi kama aina ya desturi za kijamii (Fairclough na Wodak, 1997). Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi si nadharia moja bali huchukuliwa kama njia iliyo na mitazamo tofauti ya kuchunguza uhusiano baina ya matumizi ya lugha na miktadha ya kijamii. Teneti ambazo hurejelewa zaidi ni zile za Fairclough na Wodak (1997). Hata hivyo, mawazo ya Van Dijk pia yana mchango katika kazi hii kwa vile utafiti huu ulihusisha, lugha, historia, itikadi na masuala mengine ambayo mtaalam huyu amechangia.

Fairclough (1992) anahoji kuwa mchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni sharti aanze kwa kuvichanganua vipengele vya chini (vidogo) vinavyopatikana katika matini kama vile, msamiati, nomino na vishazi na aendelee hadi kwa vipengele vikubwa vya kijamii ambavyo matini huchota kwayo. Umuhimu wa mwelekeo huu ni kwamba mtafiti hupata fursa ya kuchagua vipengele vya kiisimu anavyohitaji kuangazia kulingana na maswali

ya utafiti, suala la utafiti au kichocheo cha utafiti husika (Fairclough 2003). Walsh (2003) akiunga mkono mawazo haya anaeleza kuwa matini huchota kutoka kwa jamii na wanaotoa matini. Lengo kuu la nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni kushughulikia matini na muktadha (Walsh 2001). Ndiposa utafiti huu uliitumia nadharia hii ili kupeana mwelekeo katika uchanganuzi wa diskosi na vilevile matini ya majigambo.

Hapo awali kabla ya kuasisiwa kwa nadharia hii ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi, tafiti zilizoko zinaonyesha kuwa wanaisimu walichunguza lugha kinadharia na kutotilia maanani matumizi na uamilifu wa lugha katika jamii. Inaaminika kuwa uchunguzi wao ulijikita katika umilisi wa wazawa wa lugha (Chomsky 1957). Uamilifu wa lugha haukuzingatiwa bali waliegemea katika uhusiano baina ya lugha na muktadha au Isimu Amali (Levinson 1983). Kwa kuzingatia umilisi wa kipragmantiki, sentensi na vipashio vya sentensi vilichukuliwa kama viambajengo vya kimsingi katika uchanganuzi wa lugha (Matinde 2015).

Nadharia ya UCHAMAWADI ni muhimu katika utafiti huu kwa vile hutambua uamilifu wa lugha katika jamii (Fairclough na Wodak, 1997). Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika mkondo wa Fairclough (1992) anayedai kuwa, Usemi ni lugha semwa inayotokana na tukio la usemi. Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya usimulizi. Vilevile, Fairclough anafafanua utanzu kama matumizi ya lugha yanayohusishwa na utendaji fulani wa kijamii.

Anachukulia usemi kama kipengele cha jamii na kuhusisha lugha na mamlaka. Wazo muhimu katika mawazo ya Fairclough kwa utafiti huu ni dhana kuwa usemi ni historia na hueleweka katika muktadha wa historia yake. Wodak katika mwelekeo wake ameihusisha diskosi na masuala ya isimu na historia. Wodak (2001) anasisitiza umuhimu wa muktadha wa jumla wa usemi. Wodak anachukua mwelekeo wa mtazamo wa kuhistoria katika falsafa yake. Kwa kuangazia nadharia hii ya UCHAMAWADI, usemi huhakikiwa kwa kuzingatia mitazamo mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kihistoria. Taswira inayojitokeza katika utafiti huu ni namna ambavyo mitazamo hii husimbwa na kusawiriwa katika majigambo na vipashio mbalimbali vya lugha.

Utafiti huu ulilenga katika kuhusisha historia ya ubabedume na vipera vya majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha kwa kuchunguza vipashio mbalimbali vya lugha kama vile jazanda, takriri, kejeli, tanakali za sauti miongoni mwa vingine. Kipengele cha Semantiki kilichunguzwa na kupata kutambua jinsi kinavyojitokeza katika majigambo ya Waisukha. Hivyo, hali hii ilitupa haja ya kuhusisha Fasihi Simulizi na Isimu kwa kuchunguza vipengele vya Isimu ndani ya Fasihi Simulizi. Kwa hivyo, tunatarajia kuonisha taaluma ya Isimu na uwanja wa Fasihi Simulizi kwa kutumia nadharia mbili; nadharia ya Uwezo-uume na nadharia ya UCHAMAWADI. Kwa kutumia mtazamo wa Kiisimu katika kuhakiki ubabedume katika Majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mayo*, mtafiti atakuwa anaupa utanzu wa maigizo nguzo mpya ya uhai. Aidha, *Mayo* ni sherehe inayouleta upya wa *Shilembe* kama sanaa ya maigizo.

Baada ya kupitia tafiti kwa mfano, Wandera (1996), Mwita (1997 & 2005), Wanjala (2007, 2011 & 2015), Matinde (2012 & 2015), na Mung'ahu na Kobia (2016), imebainika kwamba watafiti hawa walishughulikia vipengele kama vile usawiri wa mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili, miviga ya tohara katika jamii ya Wabukusu kwa kuangazia Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa *Embalu* na *Mwaka Kogwa* na ubabedume katika majigambo ya Wakuria pamoja na ubabedume katika utenzi wa Fumo Liyongo miongoni mwa tafiti nyingine. Tafiti hizi zilishughulikia vipengele vingine vya Fasihi Simulizi na hazikulenga kushughulikia utafiti wa ubabedume katika lugha ya majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mayo* miongoni mwa Waisukha kwa kutumia mtazamo wa kiisimu hususan Semantiki. Isitoshe, kila jamii ina utamaduni wake wa kipekee na kwa hivyo kulingana na tahakiki za utafiti zilizoko, hakuna ufafiti wowote ambao umefanywa katika jamii hii kwa kuyarejelea majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mayo* katika sherehe ya kupiganisha fahali. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kufanya utafiti ili kuliziba pengo hilo.

## **2.9 Mkabala wa Ufasiri na Uchanganuzi wa Majigambo**

Matinde (2015) katika tasnifu yake ya Uzamifu anapendekeza kwamba mchanganuzi yeyote wa masuala ya majigambo hana budi kuutumia mkabala wa Ufasiri na Uchanganuzi wa majigambo kama ulivyofasiriwa na De Beaugrande na Dressler (1991). Wataalam hawa wanafasiri matini kama tukio la kimawasiliano ambalo ni sharti likitwe katika vigezo saba muhimu. Wanahoji kuwa, matini sharti iendane na kanuni za utanzu mahsusi au aina maalum ya utanzu. Kila utanzu wa fasihi huwa na sifa mahsusi za kiisimu, uamilifu mwafaka na hukitwa ndani ya mipaka maalum ya uzalishajina upokeaji

wa hali za kijamii (Swales 1991). Ni muhimu kutaja kuwa kuna maana ya kijuujuu na maana ya ndani ya matini husika. De Beaugrande na Dressler (1981) waliorodhesha vigezo saba vya ufasiri na uchanganuzi wa matini na semi. Vigezo hivi ni kama vifuatavyo:

- a) Mshikamano: Huhusisha vigezo vya matini katika umbo la nje mintoarafu ya uhusiano na uwiano wa vipashio vya Kisintaksia. Mshikamano hutokana na matumizi ya uradidi, udondoshaji na uunganishaji wa vijenzi vya matini husika. Katika majigambo ya Waisukha, wasanii ambao ni fanani watambaji na fanani wajigambi hujenga mshikamano katika majigambo kwa kutumia mbinu mbalimbali kwa mfano, matumizi ya nomino, vishazi, chuku, tashbihi na jazanda.
- b) Mchukuano: Huhusisha maana ya matini. Hurejelea elementi ambazo hazihitaji utambuzi au maarifa ya kiisimu. Hujikita kwenye maarifa ambayo hayajitokezi wazi katika matini bali ni vimanilizi vinavyodokeza nia ya msanii ambayo kwa kiasi fulani huweza kuathiri upokezi kwa upande wa hadhira (Grice, 1975), Wodak, 1987; Kintsch na Van Dijk, 1983). De Beaugrande na Dressler (1981) wanadokeza kuwa baadhi ya maana husimbwa pamoja kuhusiana na uhusiano na utambuzi wa umbo la nje na umbo la ndani la matini.
- c) Dhamira: Hurejelea mtazamo, mwelekeo na azma ya mtunzi wa matini husika. Huhusisha kile ambacho mtunzi amenuia kukiwakilisha kwa hadhira. Katika majigambo, wasanii hulenga kupitisha mitazamo, mielekeo, itikadi na imani za jamii ambazo kwa namna mbalimbali hujenga na kudumisha ubabeduma na mfumodume katika jamii. Kwa kutumia weledi na ubunifu wao, wasanii husika

husetiri ama husimba hali mbalimbali za kijamii ambazo kwa namna ya kipekee hujenga na kudhihirisha mitazamo, mielekeo, imani, itikadi, desturi na historia ya jamii. Mambo haya yote kijumla huwa ni vijenzi mwafaka vya ubabedume katika jamii kama iliyobainika katika jamii ya Waisukha.

d) Ukubalifu: Dhana hii hutumika kama kioo cha dhamira ya mtunzi. Matini sharti itambuliwe na kukubalika na hadhira husika ndani ya mipaka ya hali mahsusi. Katika jamii ya Waisukha, utanzu wa majigambo hubainisha sifa za ukubalifu. Jambo hili ni la ukweli kwa vile mwanajamii hawezi kuamka tu na kuanza kujigamba peke yake. Huweza tu kufanya hivyo katika hafla na sherehe mbalimbali za kijamii kama ilivyodhihirika katika miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Sherehe hizi huwepo na hadhira ambayo huwa ni tendi hususan wanaoshiriki katika ngoma ya Isukuti (Taz. Kiamb. D, P5, P14, P15, P16, P17, P18 na P19). Ukubalifu hutokana na pia hutegemea maandalizi ya wasikilizaji na wasomaji wa kusikiliza au kusoma matini ambayo bila shaka wanatumaini kuwa na manufaa na maana katika jamii.

e) Uarifishaji au ueleweshaji: Hurejelea upya na thamani ya taarifa inayotarajiwa. Hurejelea ubora na kiasi cha taarifa inayowasilishwa. Katika utanzu wa majigambo, fanani watambaji na fanani wajigambi hujitahidi kadri ya uwezo wao ili kusimba upya katika majigambo yao, hali ambayo huakisi uhai wa jamii. Aghalabu huwepo na hadhira ambayo huakisi uhai wa jamii na mabadiliko andamizi. Kwa kufanya hivyo, msanii wa majigambo ambaye ni fanani hubuni na kusimba njeo tatu katika jigambo lake, hali inayodokeza mabadiliko ya kijamii



kutegemea mpito wa wakati kama tulivyoona ujinyambuaji wa sherehe ya *Shilembe*.

- f) Muktradha na hali: Kundi la matamko na hali mbalimbali za uneni huwa na mchango muhimu katika uzalishaji wa matini (Wodak na Wenzake, 1989). Kuna aina za pekee za matini, mitindo ya uneni na maumbo mbalimbali ambayo hujitokeza katika hali na muktradha halisi wa utamaduni na itikadi za kijamii. Kwa hivyo, utafiti huu ulijikita katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* pekee wakati wa upiganishaji wa fahali kwa kurejelea itikadi na utamaduni wa jamii hii
- g) Mwingiliano tanzu: Huwa na maana mbili; maana ya kwanza hurejelea matini ambazo ni tangulizi au zinazojitokeza sawia na usemi. Maana ya pili ni vigezo kubalifu vya kuunganisha matini moja na nyingine katika utanzu mahsusi au aina mbalimbali za matini (Wodak 1986). Majigambo kwa namna ya pekee hudhihirisha maana hizi mbili. Katika utafiti huu, haya yalidhihirika wazi nyanjani kwa vile fanani kwa ustadi na ubunifu aliweza kusimba tanzu mbalimbali kwenye jigambo lake. Kwa mfano, katika mijadala huu na Utazamaji pamoja na Uchunzaji-Shiriki (taz. Kiamb. A, B, C, D na E) fanani waliweza kutamba ngano, kutega na kutegua vitendawili na methali miongoni mwa tanzu nyingine za tanzu za Fasihi Simulizi ya Waisukha.

Matinde akishadidia mawazo ya Tischer na wenzake (2002) anaeleza kuwa kila matini ni sharti iwekwe ndani ya muktradha mahsusi na huhusiana na matini nyingine kisinkronia na kidaikronia. Wanachomaanisha wataalam hawa ni

kwamba, ni muhimu uchanganuzi wa data uweze kuzingatia uhakiki makinifu unaofuata hatua moja baada ya nyingine badala ya kuzingatia tu vipashio vya kiisimu, mshikamano na uchukuano. Kwa kujikita katika ukweli huu, uchanganuzi matini huhusisha viwango vya; Mofolojia, Sintaksia, Semantiki na Pragmatiki. Kwa mujibu wa utafiti huu, maoni, mielekeo na mawazo ya wataalam hawa yalikuwa uti wa mgongo na msingi faafu katika uchanganuzi wa ubabedume katika majigambo ya miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mayo* miongoni mwa Waisukha. Haya yalikuwa muhimu hususa mpangilio na ufuataji wa hatua katika mchakato wa uchanganuzi wa majigambo yaliyoteuliwa kwa njia ya kimapokezano mintaarafu ya malengo ya utafiti na misingi ya nadharia.

## **2.10 Hitimisho**

Kwa ujumla, sura hii imeshughulikia mapitio ya maandishi ya awali ambayo yana uhusiano na uchunguzi ambao umefanywa katika tasnifu hii. Lengo kuu lilikuwa kuweka wazi mwanya ambao utafiti huu ulikusudia kuuziba. Baadhi ya kazi hizi zilichangia katika kuufanikisha utafiti huu kwa njia moja au nyingine hususan ile hali ya kuyapanua mawazo ya mtafiti kuhusu suala la utafiti. Miongoni mwa kazi zilizotafitiwa na kuhakikiwa ni zile zilizohusiana na ubabedume, majigambo, miviga, utamaduni, historia, lugha, itikadi, usemi, uana, fasihi na vipengele vya lugha miongoni mwa masuala mengine. Sura hii inadokeza vigezo saba vya ufasili na ufasiri wa matini kwa mujibu wade Beaugrande na Dressler (1981) ambavyo vilipendekezwa na Matinde (2015) kama vigezo mwafaka katika uchanganuzi wa majigambo.

Nadharia za Uwezo Uume na Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi zilikuwa muhimu katika kuupa utafiti huu mwongozo wa kutambua uamilifu wa utamaduni wa jamii. Jambo hili lilionyesha dhana ya dhakari kuwa kama kielelezo cha kumpa mwanamume mamlaka na uwezo dhidi ya mwanamke katika jamii, kama ilivyodhihirika katika fahali na jinsi Waisukha husawiri ubabedume.

## **SURA YA TATU**

### **MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii ilishughulikia muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, umma lengwa, uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data na sampuli teule. Aidha, sura hii imeshughulikia uchanganuzi na uwasilishaji data, uthabiti wa vifaa, uaminifu wa vifaa, majaribio ya vifaa vya utafiti, uhalali na uthabiti wa vifaa, uwasilishaji wa matokeo, maadili na changamoto nyanjani.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ni wa kimaelezo kwa sababu data iliyokusanywa na kuchanganuliwa ni ya kithamano, mikabala ya kihistoria na kiethnografia. Muundo wa kithamano ni mwafaka kwa utafiti wa aina hii. Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza kuwa mkabala wa kithamano unafaa zaidi katika kufanya utafiti barani Afrika kwa vile taarifa nyingi hupitishwa kwa njia ya masimulizi. Kwa hivyo, data iliyokusanywa si ya kitakwimu kwa vile ililenga kufafanua tabia na mahusiano ya kibinadamu. Mawazo ya Donald (2006) yanakubaliana na ya wataalam hawa anaposema kuwa utafiti wa kithamano ni wa kimaelezo na hulenga kuchanganua tamaduni na tabia ya binadamu na makundi yao kutokana na mtazamo wa wale wanaotafitiwa. Anaongezea kuwa ni utafiti ambao huzingatia mazingira halisi. Ni wa kihistoria kwa vile ulihusu kuchunguza asili na usuli wa jamii ya Waisukha hususan mfumo wao wa kinasaba.

Malengo ya utafiti yalijikita katika kufafanua hali za kijamii ndani ya muktadha halisi ya jamii tafitiwa. Utafiti huu ulihusisha miktadha mbalimbali ya masimulizi na mtagusano na fanani wa jamii husika. Utafiti huu ni wa kiethnografia kwa sababu mtafiti alipata nafasi ya kwenda kuishi na Waisukha, kuwahoji, kutazama na hata kushiriki katika utendaji wao wakati wa kuyasema majigambo katika sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Khakasa (2018) akimnukuu Kerlinger (1978) anapendekeza kuwa ni bora kuitumia mbinu ya uchunguzi wa kinaelezo kwa sababu inapotumika hutoa maelezo mengi ya kutegemewa. Ndiposa utafiti huu ulifanywa kwa lengo la kukusanya majigambo ya Waisukha yanayoghaniwa na fanani watambaji na wajigambi wakati wa upiganishaji fahali ili kuelezea sifa za ubabedume zinazosawiriwa kupitia kwa vipashio vya lugha kama nomino na tamathali za semi kama vile jazanda.

### **3.3 Mahali pa Utafiti**

Utafiti wa nyanjani ulifanywa katika sehemu mbalimbali katika kaunti ya Kakamega, eneo bunge la Shinyalu. Ulihusisha sehemu maalum ambapo fahali hupigania, nazo ni; Museno, Khayega, Ilala, Uwanja Ndege, Shinyalu na Mulanda. Hii ni kwa sababu haya ni maeneo rasmi yaliyotengewa sherehe za *Mchezasili* wa *Mayo*. Miviga ya sherehe ya *Shilembe* inahusu wafu na mtafiti alipata fursa ya kuhudhuria sherehe tatu katika kaunti hii: katika kata ya Mulanda, nasaba ya Vashitaho mnamo tarehe 5 Septemba, 2018 (Tazama Kiamb. D, P10). Sherehe ya *Shilembe* ya pili ilifanyika kule Uwanja Ndege katika nasaba ya Vasalwa tarehe 3 Oktoba, 2018 (taz. Kiamb. D, P9) na ya tatu ilifanyika Mulanda katika nasaba ya Vamilonje tarehe 4 Januari, 2019. Sherehe hizo zilimwezesha mtafiti kupata data kwa vile fanani na washiriki walipata jukwaa la kujigamba na

kutamba majigambo. Shughuli hiyo iliweza kufaulishwa na uteuzi wa kimapokezano kama ilivyoelezwa katika sehemu ya usampulishaji. (Taz.3.5.2) Uchunguzi huo ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile ulimwezesha mtafiti kuwajua magwiji wa majigambo na lugha iliyotumiwa pamoja na kuwafahamu wenye tajriba pana kuhusu jamii ya Waisukha kijumla, desturi na mila zao. Kuelewa mila na desturi za Waisukha na kutagusana nao kulimwezesha mtafiti kuipata data ya kutegemewa.

### **3.4. Umma Lengwa**

Utafiti huu ulilenga Waisukha, waliokuwa fanani wajigambi na watambaji na pia walioshiriki katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Majigambo yaliyoghanwa katika sherehe hizi ndiyo yaliyolengwa.

### **3.5 Uteuzi wa Sampuli**

Utafiti huu ulilenga kukusanya majigambo ishirini na saba kutegemea nasaba za Waisukha. Uteuzi wa kimapokezano ulimwongoza mtafiti hadi kwa fanani na nasaba zenye ujuzi zaidi. Majigambo saba yaliteuliwa kimaksudi na majigambo tisa yakateuliwa kinasibu. Jumla ya majigambo kumi na sita yaliweza kutumiwa katika utafiti huu. Kothari (2004) anaeleza kuwa haiwezekani kuchunguza kila kijenzi cha umma lengwa, na wakati mwingine inawezekana kupata matokeo halali ya umma lengwa kwa kuchunguza sehemu ndogo tu ya umma husika. Utafiti huu ulitumia sampuli ya majigambo kumi na sita kama kiwakilishi cha nasaba ishirini na saba za Waisukha ili kuweza kupata data ya uhakika na ya kuaminika.

### **3.5.1 Uteuzi wa Wasailiwa**

Jumla ya wasailiwa kumi na sita waliteuliwa (wanne kutoka kila ukoo) wanaume kumi na wanawake sita (Tazama Kiamb. C). Sababu ya idadi ndogo ya wanawake ni kuwa baadhi ya wanawake hawakuwa huru kujadili bayana mambo yanayohusiana na utamaduni, mila na desturi ya jamii hii ya Waisukha. Uteuzi dhamirifu na wa kimapokezano ulitumiwa katika kuwateua wasailiwa ambao wengine wao walikuwa weledi katika kughani majigambo na wenye maarifa ya kina kuhusu itikadi, historia, mila na desturi za jamii ya Waisukha. Waliosailiwa walikuwa watu wazima katika jamii hiyo na ambao walikuwa na umri wa zaidi ya miaka arobaini (Rejelea K C). Mtafiti alikusanya jumla ya majigambo kumi na sita na masimulizi maalum kutoka kwa wasailiwa kulingana na mada, madhumuni na maswali ya utafiti (Tazama Kiamb. B).

### **3.5.2 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli**

Kwa mujibu wa utafiti huu, dhana ya sampuli imetumiwa kurejelea wasailiwa na ukusanyaji wa majigambo mwafaka kwa kujikita kwenye mada, malengo na maswali ya utafiti. Milroy (1987) anadokeza kuwa sampuli zinazotumiwa katika utafiti wa kiisimu ni wakilishi na matokeo yake huwa sawa kutokana na sampuli ndogo iliyoteuliwa bora usampulishaji ulifanywa bila dosari yoyote. Jambo hili ni muhimu kwa utafiti huu ambao ulihusisha nyanja za Isimu na Fasihi Simulizi. Mtafiti alipata fursa ya kutumia sampuli ya kimaksudi au dhamirifu kuteua majigambo. Kulingana na Kothari (2004), sampuli maksudi ni sampuli inayodhamiria kuteua vipengele maalum kuwakilisha kundi zima. Ikiwa vipengele hivi huteuliwa kutokana na uwepo wao, usampulishaji unaohusika huitwa usampulishaji mwafaka. Katika hali hii, mtafiti huamua kuviteua vipengele

ambavyo vitawakilisha kundi zima. Kwa mujibu wa Kuzzel 1992 katika Yun (2011) anasema kuwa ni muhimu sampuli dhamirifu ilenge kundi pana ili kuhusisha vipengele ambavyo huenda vikasababisha matokeo tofauti na yale yanayotarajiwa. Katika msingi huu, majigambo yaliteuliwa kimaksudi kwa vile kuna nasaba fulani katika jamii ya Waisukha ambazo ni maarufu katika kupiganisha fahali na pia katika kujigamba.

Sifa maalum ziliongoza uteuzi wa majigambo yaliyoteuliwa. Sifa hizo zilijikita katika vipashio mbalimbali vya lugha vikiwemo, sitiari, jazanda, kejeli, taswira, majazi, taashira miongoni mwa sifa nyingine. Utafiti wa awali uliusaidia utafiti huu kuzitambua sehemu zilizokuwa na umaarufu katika masuala ya majigambo na upiganishaji wa fahali katika jamii hii ya Waisukha. Baadhi ya sifa hizo zilidhihirisha masuala ya ushujaa, uwezo, ushindani, ustahimilivu na dhana ya kujitegemea miongoni mwa sifa nyingine. Majigambo yalisampulishwa kidhamirifu. Kama anavyodokeza Patton (2002), hakuna sheria za idadi katika usampulishaji kimaksudi. Jambo muhimu ni mtafiti kufikia sampuli kifu. Kothari (2004) anapendekeza thuluthi moja ya idadi ya jumla. Hata hivyo, uteuzi wa kimapokezano hutegemea mwongozo wa watafitiwa kwa vile ndio humwongoza mtafiti katika kukusanya data. Kutokana na jumla ya nasaba ishirini na saba za jamii ya Waisukha, majigambo kumi na sita yalisampuliwa kwa kutumia usampulishaji wa kimapokezano kwa vile fanani walikuwa wakimwelekeza kulikokuwa na sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Kati ya majigambo yaliyoteuliwa saba yaliteuliwa kimaksudi kutoka kwa nasaba mahiri katika kujigamba na majigambo tisa yakateuliwa kinasibu kutoka kwa majigambo ishirini. Uteuzi wa kinasibu uliwashirikisha washiriki katika kuteua vijikaratasi vya 'ndio' na 'la' ili kuzuia hali yoyote ya



kimapendeleo. Kutokana na sampuli hii, majigambo hayo kumi na sita ndiyo yalichanganuliwa na yakatumiwa kama vielelezo vya data katika utafiti huu.

### 3.5.3 Sampuli Teule

Sampuli iliyotumiwa katika utafiti huu iliyahusisha jumla ya majigambo kumi na sita.

Tazama jedwali lifuatalo:

**Jedwali 3.1 Sampuli Teule**

<b>SAMPULI</b>	<b>IDADI YA JUMLA</b>	<b>IDADI TEULE</b>	<b>ASILIMIA</b>
NASABA	27	16 - UTEUZI KIMAPOKEZANO	59%
<b>SAMPULI</b>	<b>IDADI YA JUMLA</b>	<b>IDADI TEULE</b>	<b>ASILIMIA</b>
MAJIGAMBO KINASIBU	16	9	56%
MAJIGAMBO KIMAKSUDI	16	7	44%
	<b>JUMLA</b>	16	100%

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

### **3.6 Mbinu za Kukusanya Data**

Mtafiti alitumia mbinu zifuatazo kukusanya data: Mahojiano, kinasasauti, uhakiki wa yaliyomo-kamera za video, utazamaji na uchunzaji-shiriki.

#### **3.6.1 Njia za Ukusanyaji wa Data**

Ili kuweza kuchunguza ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* ya Waisukha, utafiti huu ulifanywa nyanjani katika sehemu zilizo maarufu katika masuala ya upiganishaji fahali. Sehemu hizo ni; Museno, Khayega, Ilala, Uwanja Ndege, Shinyalu na Mulanda. Mbinu anuwai zilitumiwa ambazo zilimsaidia mtafiti kukusanya data. Mtafiti alitumia vifaa mbalimbali vya utafiti kutekeleza kazi hii.

##### **3.6.1.1 Vifaa vya Utafiti**

Vifaa vifuatavyo vilihusishwa katika utafiti huu:

###### **3.6.1.1.1 Mahojiano**

Mbinu hii ilikuwa mwafaka katika utafiti huu kwa vile inadhihirisha upekee wa fasihi simulizi. Utafiti huu uliwahusisha fanani na washiriki katika mahojiano kwa kuwauliza maswali na kuyanasa masimulizi ili kuweza kudondoa vipashio vya lugha katika majigambo na katika utendaji. Haya yalifanywa kwa kuongozwa na madhumni ya utafiti.

###### **3.6.1.1.2 Uhakiki wa yaliyomo**

Utafiti huu uliihusisha mbinu hii kwa kuchukua picha za video ili kuonyesha hali halisi ya utendaji wa Waisukha katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mayo* (Rej. Kiamb. D kuhusu picha zilizochukuliwa uwandani). Mtafiti alipata fursa ya kuzihudhuria sherehe hizo kwa kuongozwa na fanani katika sehemu husika. Uteuzi wa kimapokezano

ulimsaidia mtafiti kuelekezwa kulikokuwa na sherehe hizo. Sherehe hizo zilifanyika katika kipindi cha Septemba 2018 hadi Januari 2019 (Taz. Kiamb. A kuhusu ratiba ya Utazamaji na Uchunzaji-Shiriki).

### **3.6.1.1.3 Utazamaji na Uchunzaji-Shiriki**

Mbinu hii iliufaa utafiti huu kwa vile ilijumuisha maswali, kutazama na kushiriki. Mtafiti alilenga kuuliza fanani maswali, kutazama na kushiriki katika sherehe ya upiganishaji fahali kwa kuitikia wimbo. Katika mbinu hii, mtafiti alitumia mpangilio au ratiba ya utazamaji na uchunzaji-Shiriki kama kifaa muhimu cha ukusanyaji data (tazama kiambatisho A). Mbinu hii ya uchunzaji-Shiriki huhusisha kutazama, kuchunguza, kushiriki, kushuhudia, kuhoji na kusaili katika harakati za kukusanya data. Mtafiti aliweza kushiriki na kushuhudia sherehe mbalimbali zilizohusu majigambo katika utendaji wa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* katika sehemu mbalimbali kama vile, Museno, Ilala, Uwanja Ndege, Mulanda, Khayega na Shinyalu. Uteuzi wa sherehe hizi ulifanywa kwa kutumia uteuzi wa kimapokezano na kwa hivyo mtafiti aliweza kufahamishwa na fanani na washiriki wa sherehe hizo kulikokuwa na sherehe fuatili katika kipindi cha utafiti huu kama nilivyotangulia kueleza. Hali hii ilikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa vile weledi wa kujigamba wanafahamika katika jamii hii na hualikwa na kupata fursa ya kuhudhuria takriban sherehe zote, hivyo, ilitubidi tuteue baadhi ya sherehe tajwa ili kuepukana na uradidi au urudiaji wa ukusanyaji wa majigambo hayo. Jambo hilo lilikuwa faafu kwa utafiti wetu kwa vile tuliweza kuyakusanya majigambo kumi na sita tu yaliyotumiwa katika utafiti huu.

#### **3.6.1.1.4 Kinasasauti**

Mtafiti alitumia kinasasauti katika kurekodi majigambo hayo wakati ambapo magwiji mbalimbali walikuwa wakighani majigambo yaliyobeba falsafa, mitazamo, itikadi, mila, matarajio na utamaduni wa jamii ya Waisukha kuhusu ujumla wa maisha yao.

#### **3.6.1.1.5 Mijadala huru**

Mbinu za mijadala huru pamoja na mahojiano yalitumika ambapo mtafiti alipata fursa ya kunakili majibu na habari muhimu kulingana na malengo ya utafiti. Hadhira katika sherehe hizo ilikuwa tendi na fanani walijigamba kwa usanii na ufundi wa hali ya juu.

Hatimaye, mtafiti aliweza kunakili lugha ya majigambo hayo kwa maandishi katika lugha ya Kiisukha na kisha akaweza kuyatafsiri katika lugha ya Kiswahili. Mbinu hii ilikuwa muhimu sana kwa vile mtafiti alipata data halisi ya lugha ya majigambo kupitia kwa wasanii na wasailiwa husika. Mtafiti aliweza kupata data hiyo kupitia kwa mahojiano ya ana kwa ana pamoja na kujihusisha na mijadala huru na waliohudhuria sherehe hiyo hususan wapigaji na wachezaji wa ngoma ya Isukuti kama ilivyoonyeshwa katika Viambatisho A, C na E mtawaliwa. Lengo kuu la mbinu hizi lilikuwa kumwezesha mtafiti kupata mtazamo na maoni yao kuhusu namna ambavyo ubabedume huundwa na kujengwa miongoni mwa Waisukha. Hali hii ilikuwa muhimu kwa mtafiti kwa sababu mtafiti ni mmojawapo wa wanajamii na ambaye amewahi kuhudhuria na kushiriki sherehe mbalimbali za upiganishaji fahali ambamo majigambo ni kipengele cha kimsingi katika sherehe hizo.

Katika mantiki hii, mbinu hizi zilishughulikiwa kwa kujengana na kukamilishana ili kumwezesha mtafiti kukusanya data mwafaka, ya kuaminika na tegemezi katika uhalisia

wake kwa kujikita katika malengo mahsusi ya utafiti. Ndiposa Patton (1999) anahoji kuwa kule kuchanganya kwa mbinu za utafiti ni mwafaka kwa vile humwezesha mtafiti kupata uelewa wa kina wa kile kinachoendelea wakati wa utendaji, kwa vile yeye huwa miongoni mwa watafitiwa kupitia kwa ushiriki wake. Anaongezea kuwa hali hii humpa mtafiti fursa ya kuweza kupata maoni, hisia, mtazamo na mwelekeo wa watafitiwa wake kupitia kwa mbinu za kutazama na kuhoji. Jambo lililo muhimu katika mawazo ya Patton ni kwamba matumizi ya mbinu tofauti za ukusanyaji data humwezesha mtafiti uelewa wa kina wa kile kinachoendelea wakati wa utendaji. Mtafiti aliweza kupata data au ujumbe halisi usio na upendeleo wala usioegemea upande wowote.

### **3.7 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Jumla ya majigambo ishirini na saba yalikusudiwa kukusanywa kutegemea nasaba takriban ishirini na saba za Waisukha. Hata hivyo, majigambo kumi na sita yaliteuliwa kwa kutumia uteuzi wa kimapokezano kwa ajili ya uchanganuzi. Majigambo hayo kumi na sita yaliwekwa kwenye maandishi ya lugha ya Kiisukha na tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili. Tafsiri huru na maana zilitumiwa. Nilichanganua data kwa kuzingatia malengo, nadharia na kurejelea madondoo mahususi kuhusu majigambo na vipashio vya lugha; nomino, vishazi na vitenzi pamoja na kuhakiki tamathali za usemi kwa kujikita katika kipengele cha kiisimu ambacho ni semantiki.vipashio. Data nyingine za ziada zilikuwa katika mfumo wa maoni, majibu na maelezo ya wasailiwa na wanajamii kuhusu dhana ya ubabedume iliyojitokeza kupitia kwa Utazamaji, Uchunguzi-Shiriki, maelezo ya wahojiwa na wasailiwa pamoja na wanajamii waliohudhuria sherehe ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* katika sehemu tajwa. Jambo lililodhihirika katika

baadhi ya majigambo ni kuwa baadhi ya beti zilijirudia katika baadhi ya majigambo ya wasanii mbalimbali. Ilimbidi mtafiti aweze ateue baadhi ya beti na kuchuja nyingine katika uchanganuzi wa data kwa kutumia uteuzi nasibu na uteuzi wa kimatilaba ili kuweza kujikita katika mipaka na malengo mahsusi ya utafiti pamoja na nadharia mbili za utafiti.

Mtafiti aliwahasisha baadhi ya wasailiwa na fanani katika shughuli za ufasili na ufasiri kwa vile wengine walitumia Kiisukha cha kale na cha ndani zaidi. Hali hii ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile ilimpa mtafiti nafasi ya kuutumia umilisi na utendaji wa wasailiwa katika kuweza kuchambua data viliyo. Mawazo haya yameibuliwa na kauli ya Wanjala (2015) anayesema kuwa uelewaji ni mchakato unaotokana na ushirika kati ya utendaji, unenaji pamoja na usemezano kati ya mchambuzi na jamii tafitiwa. Mawazo haya yanaungwa mkono na Matinde (2015) anayeongezea kwa kusema kwamba tukio linaeleweka tu kupitia kwa kuuliza maswali kati ya fanani, hadhira na mchambuzi ndani ya muktadha wa unenaji. Wataalam hawa wanakubaliana kwamba ushirikiano, mashauriano na maafikiano baina ya mchambuzi, msanii na hadhira ni jambo muhimu sana katika utafiti wa fasihi simulizi. Ushirikiano kati ya mtafiti na watafitiwa katika mchakato wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu kwa vile ulisaidia katika kuondoa hali ya kuegemea upande wowote ule. Kauli ya kuwashirikisha watafitiwa katika hatua ya uchambuzi wa data imeungwa mkono na baadhi ya wataalam kama kama vile Wanjala (2015) anayeunga mkono mawazo ya Alembi (2002) na kuhoji kuwa kushirikishwa kwa watafitiwa katika uchambuzi wa data ya fasihi simulizi hutokana na ukweli kwamba, kila jamii huwa na viwango na vigezo

vya kuhakiki kazi yao. Jambo lililo muhimu katika kauli za wataalam hawa ni kwamba watafitiwa hawafai tu kutoa data pekee bali pia wanafaa kushirikishwa katika uhakiki na uchambuzi wake kama anavyodhukuru Wanjala.

Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa kulenga vipashio vya lugha na vipengele vya kiisimu vinavyosawiri ubabedume. Uchanganuzi ulivihusisha vipashio vya lugha kama vile majazi, tashbihi, chuku na jazanda kwa kuvifungamanisha na kipengele cha kiisimu ambacho ni semantiki. Utafiti ulibaini kuwa kipengele cha kisemantiki ndicho kilichokuwa mwavuli wa vipengele vingine vya kiisimu kama wanavyodai Habwe na Karanja (2004). Hii ni kwa sababu, umuhimu wa lugha ya binadamu ni kuleta mawasiliano yanayosababisha maendeleo katika jamii. Mawasiliano hayo hutokana na hali ya binadamu kuweza kufasiri maana ya kile kinachosemwa au kuandikwa na binadamu mwenzake. Kipengele cha kisemantiki ndicho kilicho na uwezo wa kutekeleza jambo hili na kuleta maendeleo katika jamii husika (Simala 2013).

Uchanganuzi wa data ulitalii kiwango cha sauti, neno, kirai, kishazi, sentensi neni na andishi au matini na maana. Mihimili miwili ya nadharia ya Uwezo-uume ilitumiwa ili kuweza kutathmini jinsi jamii hii inavyojenga ubabedume, itikadi, mitazamo na mikakati ya kusawiri mahusiano ya kiuana katika jamii ya Waisukha iliyo na mfumo dume. Nadharia ya UCHAMAWADI nayo ilitumiwa kushughulikia viambajengo vya lugha ambavyo hutumiwa katika kubainisha namna ambavyo vipashio hivyo husawiri ubabedume kwa kuangazia sifa za kiubabe ambazo ndio msingi wa utafiti huu. Mihimili ya nadharia ya UCHAMAWADI kwa kuiangazia mitazamo ya Van Dijk (1993) juu ya ubaguzi wa watu katika jamii, mwelekeo wa Wodak (1996) na ule wa Fairclough (1993)

kuhusu uamilifu wa lugha katika jamii ilitumika katika kuangazia na kufidia masuala mbalimbali katika jamii hii ya Waisukha.

Mihimili hii ilikuwa kama dira ya kuweza kuhakiki namna ambavyo lugha katika majigambo ya Waisukha hukuza na kudumisha ubabedume na mamlaka na uwezo miongoni mwa mwanamume Mwisukha kinyume na yule wa jinsia ya kike ambaye anasawiriwa kama aliyedhalilishwa na mtegemezi tu. Hali hii iliweza kufanyika kwa kujikita katika malengo na maswali ya utafiti. Nadharia ya Uwezouume na UCHAMAWADI ziliusaidia utafiti huu kuchanganua majigambo kumi na sita ili kubaini uamilifu wa lugha, utamaduni, historia na itikadi za jamii ya Waisukha. Kwa kutumia nadharia hizi mbili kama dira, mtafiti aliweza kurejelea sehemu zifuatazo ili kuyatimiza malengo ya utafiti huu:

Kwanza kabisa kulikuwa na umuhimu wa kuchunguza vipashio vya lugha hususan nomino na vishazi. Pili, kuangazia taashira na tamathali za usemi kwa kujikita katika kipengele cha kiisimu, semantiki kwa vile husheheni maana. Tatu, ujenzi wa itikadi na ubabedume. Nne, umuhimu wa yaliyomo katika lugha ya majigambo na fahiwa mbalimbali. Tano, sifa na majukumu ya mwanamume na mwanamke. Mwisho, ubabedume kama sifa za jinsia ya kiume.

### **3.8 Uthabiti wa Vifaa**

Mtafiti yeyote yule ni sharti aweze kuupima ukamilifu wa vifaa vya utafiti ili utafiti wake uwe na kigezo cha usayansi. Mugenda na Mugenda (1999) wanapendekeza kuwa uthabiti wa vifaa utekelezwe kwa kufanyiwa majaribio awali. Kulingana na kauli hii,



majaribio awali yalifanywa kwa lengo la kupata uthibiti na uhakikishaji wa vifaa vya utafiti huu. Kombo na Tromp (2006) wanahoji kuwa uthabiti wa vifaa vya utafiti ni mbinu mwafaka ya kupima ukamilifu wa matokeo bora ya utafiti. Mawazo haya yanaungwa mkono na Khakasa (2018) akiwanukuu Best na Khan (1993) kwa kueleza kuwa uthabiti hurejelea kiwango cha kupima ukamilifu wa kitu kinachotarajiwa kupimwa. Kutokana na maelezo ya wataalam hawa, vifaa vya utafiti huu ambavyo ni; mahojiano, uhakiki wa yaliyomo uliohusisha kamera za video, utazamaji na uchunzaji-shiriki, kinasasauti na orodha ya mijadala huru vilipewa wataalam katika idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu cha MMUST.

Wataalam hao waliweza kuvichunguza na kutathmini ubora wa kila kifaa na ufaafu wake pamoja na uwiano wa malengo ya utafiti. Walivipima vifaa hivyo kwa mizani ya kisayansi na mapendekezo yao yalitumika hatimaye katika kuunda na kuyachuja maswali ya usaili, mada za mijadala huru na mwongozo wa uchunzaji-shiriki ili kuzua data tegemezi. Fanani watambaji na wajigambi pamoja na Waisukha walioshiriki katika miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* ndio waliolengwa katika mahojiano, mijadala huru na uchunzaji-shiriki, kupigwa picha na pia kurekodiwa wakati wa kughani majigambo hayo. Kwa hivyo, mtafiti alipata fursa ya kuelekezwa na wasimamizi wake ili kuhakikisha uthabiti wa vifaa vya utafiti. Marekebisho yalitekelezwa katika vifaa hivyo ili kuhakikisha vinalingana na malengo ya utafiti. Katika mantiki hii, uthabiti ulirejelea matokeo ambayo yalieleza athari ya majigambo ya miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* katika kusawiri ubabedume kupitia kwa vipashio vya lugha na tamathali za usemi na pia kwa kujikita katika mtazamo wa kisemantiki.

### **3.9 Uaminifu wa Vifaa**

Kulingana na Mugenda (2003) akiunga mkono mawazo ya Patton (2002), anaeleza kuwa uaminifu wa vifaa vya utafiti ni muhimu kwa vile, kando na kuonyesha uthabiti wa vifaa ni lazima viwe vya kuaminika ili ufaafu wake udhihirike katika utafiti. Naye Orodho (2004) anafidia mawazo haya kwa kusema kuwa vifaa vinaweza tu kuwa na uaminifu iwapo matokeo yale yale na yaliyo sawa yatatolewa kwa vipindi vingine tofauti. Mtafiti alizingatia maoni ya wataalam hawa na akaweza kufanya majaribio awali kwa idadi ndogo ya fanani na washiriki katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Haya ni kwa mujibu wa Patton (1990) anayependekeza kuwa idadi ndogo inayotumiwa katika majaribio awali isirejelewe tena katika utafiti halisi. Kwa hivyo, idadi ndogo ya fanani na washiriki haikuhusishwa tena katika utafiti huu.

### **3.10 Majaribio ya Vifaa vya kukusanya data**

Utafiti wa awali ulifanywa ili kutathmini ufaafu wa vifaa vya ukusanyaji data. Hali hii ilikuwa muhimu sana kwa vile ilimwezesha mtafiti kujifahamisha na sehemu ya utafiti na vilevile kutangamana na wasailiwa. Kulikuwa na mkutano wa fanani na watafiti wasaidizi katika maeneo yaliyoteuliwa. Katika mikutano hiyo, fanani wajigambi, fanani watambaji na watafiti wasaidizi kutoka maeneo ya Museno, Ilala, Khayega, Shinyalu, Uwanja Ndege na Mulanda walisailiwa katika mahojiano ya ana kwa ana na mijadala huru ili kutoa majibu.

Jambo hilo lilikuwa muhimu kwa vile lilisaidia katika kuthibitisha ufaafu wa vifaa vya utafiti. Wakati wa kusailiwa, walipewa nafasi ya kuuliza maswali kuhusiana na sehemu

wasizoelewa, vilevile, mtafiti alipata fursa ya kutumia vifaa vya teknolojia kama vile tepurekoda, kinasasauti, video pamoja na kuchukua picha. Kulikuwa na mkutano na msimamizi wa eneo bunge la Shinyalu na wazee ambao ni viongozi wa miji kumi husika kutoka kila sehemu ya utafiti ambao walihusishwa katika kuhojiwa ili kupata idhini yao iwapo maswali hayo yalikubalika kuulizwa kuhusiana na swala hili. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa vile majaribio hayo ya awali ya nyenzo yalimwezesha mtafiti kugundua udhaifu wa nyenzo zake kama wanavyodai Mark na Peter (2001) katika Khakasa (2018).

### **3.11 Uwasilishaji wa Matokeo**

Jambo la kwanza katika mchakato huu lilikuwa kuyaweka majigambo kwenye maandishi katika lugha ya Kiisukha. Hii ilikuwa hatua muhimu kwa vile lugha ya majigambo ndiyo iliyokuwa data yetu. Ie hali ya kuwa na umilisi wa lugha ya Kiisukha na kusaidiwa na watafitiwa katika kufasili na kufasiri majigambo ndiyo iliyokuwa hatua fuatili. Watafiti wasaidiwa waliokuwa na umilisi wa lugha zote mbili yaani Kiisukha na Kiswahili walisaidia sana katika hatua ya uwasilishaji wa matokeo. Majigambo hayo yalitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi, tafsiri maana na tafsiri mawasiliano kwa kuzingatia mtindo wa kishairi na kutolewa maelezo ya ziada ilipobidi.

Hatua ya mwisho katika uwasilishaji wa ripoti ilikuwa ni ile ya kuandika ripoti ya utafiti kimaandishi na kutoa maelezo ya kiufafanuzi. Maelezo hayo yameandikwa kwa kurejelea ithibati ya lugha ya majigambo yaliyokusanywa na kuteuliwa kimatilaba ili yatumike vilivyo katika uchanganuzi wa data kwa kuegemea katika madhumuni na maswali ya utafiti. Baadhi ya picha zilizochukuliwa nyanjani zimeambatanishwa katika ripoti hii

kama ithibati kwamba mtafiti alienda nyanjani kwa kutumia mkabala wa kiethnografia na hivyo akapata fursa ya kuishi na Waisukha, kutazama, kuhudhuria na hata kushiriki katika utendaji wa sherehe tajwa. Kusudi la picha hizo ni kuwawezesha wasomaji wa kazi hii kupata fursa ya kukisia hali halisi ilivyokuwa katika kipindi cha utafiti kwa kutazama uhusika, ushiriki na utendaji wa wanajamii katika kipindi hicho chote cha utafiti wa takriban miezi mitatu kuanzia mwezi wa Septemba hadi Novemba, 2018. (Tazama Kiamb. D).

### **3.12 Maadili ya Utafiti**

Dhana ya maadili hurejelea ile hali ya kutenda matendo ya haki kama vile kupata kibali na kuwa na siri wakati wa kufanya utafiti. Hizi ndizo kanuni zinazostahili kuzingatwa hususan katika utafiti wa nyanjani. Kwa hivyo, utafiti huu ulizingatia maadili kwa vile unalenga kuwachunguza binadamu kama watafitiwa. Bryman (2006:88) anasema kuwa:

Mtafiti yeyote yule anayeshughulikia masuala yoyote ya kijamii na ambaye analenga matokeo ya utafiti wake yawe ya kuaminika anapaswa kuwaza kuhusu maadili ya kitafiti. Hii ni kwa sababu, utafiti usio wa kitakwimu aghalabu hugusa maisha ya watu na hata kuingilia maisha yao ya siri (Tafsiri yangu).

Kauli hii inaungwa mkono na Berg (2001:48) anaposema:

Watafiti ambao wametumia ridhaa iliyoandikwa na inayotolewa kabla ya utafiti kufanywa, wameripoti kuwa, kuna uwezekano mkubwa wa kupata habari ambazo siyo kamilifu kwa sababu, wasailiwa ama wanakataa kuhojiwa, wanajiondoa wakati utafiti unapoendelea au wanapinga utafiti husika. Ili kuepukana na hali hii, watafiti wengi hutumia mbinu ya kupata ridhaa kwa njia isiyo ya moja kwa moja ( Tafsiri yangu).

Baada ya kuwaeleza wasailiwa malengo husika, kama hawakatai basi wamempa mtafiti ridhaa. Katika mantiki hii, mtafiti aliweza kupata ridhaa ya Waisukha ili kuweza kuwafanyia utafiti na kuwaomba ruhusa ya kwenda kuishi nao kupitia kwa wakuu wa serikali wa miji kumi husika kutegemea nasaba zao.

Hatua ya kimsingi ilikuwa kupata kibali cha utafiti kutoka kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia -NACOSTI (Taz. Kiamb. J). Mtafiti pia alipata kibali kutoka kwa serikali ya kaunti ya Kakamega (Taz. Kiamb. H ) pamoja na idhini kutoka kwa watafitiwa. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro kilinipa kibali cha kimsingi cha kwenda nyanjani kufanya utafiti (Taz, Kiamb. G). Niliweza kuwafafanulia watafitiwa sababu zangu za kutaka kufanya utafiti kama vile, kuniwezesha kupata shahada ya Uzamifu, kutoa mchango katika taaluma ya Isimu na Fasihi Simulizi kwa kuonyesha jinsi mwanamume Mwisukha anasawiriwa na pia kuwahakikishia kuwa data itakayokusanywa ingetumiwa tu kwa ajili ya utafiti. Mtafiti aliweza kukadiria ili kubaini iwapo watafitiwa walihitaji kulipwa au la. Jambo hili lilitegemea kwa vile alihitaji data halisi na isiyoegemea upande wowote. Katika mantiki hii, kuna wale ambao mtafiti aliweza kuwalipa hela kiasi fulani kulingana na jinsi tulivyoelewana na wengine walinisaidia kupata data kwa hiari yao wenyewe.

### **3.13 Changamoto za utafiti**

Uchunguzi huu ulikumbwa na changamoto kadhaa. Nazo ni:

- 1) Kulikuwa na tatizo la kutafsiri na kufasiri baadhi ya maneno yaliyokosa visawe vyake katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, ile hali ya mtafiti kuwa na umilisi na utendaji katika lugha ya Kiisukha na lugha ya Kiswahili ilimwezesha kutumia

mbinu mbalimbali za tafsiri kwa mfano mbinu ya tafsiri sisisi na tafsiri maana miongoni mwa mbinu nyingine.

- 2) Utanzu wa majigambo una uchangamano. Hii ni kwa sababu majigambo hutegemea utamaduni na itikadi za jamii husika. Dhana hii ilikuwa tata kwa vile ilimlazimu mtafiti kufanya utafiti wa kina kwa kupitia takriban kila kipengele cha utamaduni wa jamii ya Waisukha kinachorejelea majigambo. Hali hii ndiyo iliyomwezesha mtafiti kupata data ya kutumia katika utafiti huu, aliweza kupata picha halisi ya jinsi majigambo hukuza, huendeleza na kudumisha ubabedume.
- 3) Tatizo la usafiri kwa vile utafiti huu ulifanywa katika eneo bunge la Shinyalu ambapo barabara zake ni mbovu. Kulikuwa na tatizo la kuvurumishiwa vumbi na pia wakati mwingine kulikuwa na utelezi wakati wa mvua. Sehemu zilizozua shida ni kama vile Shinyalu, Uwanja Ndege na Mulanda hususan wakati wa kupiganisha fahali.
- 4) Kuna baadhi ya wasailiwa hasa wanawake ambao walikuwa waoga na wengine walishindwa kujibu maswali kwa sababu ya hali yao duni katika jamii.
- 5) Wengi wa data ulikuwa tatita kwa vile, mwanzoni tulidhamiria kukusanya majigambo yenye beti ishirini na saba kulingana na idadi ya nasaba za Waisukha, lakini katika harakati zetu za kukusanya data tuligundua ya kwamba majigambo mengine yalijiradidi. Uteuzi wa kimapokezano uliwezesha utafiti kubakia na majigambo kumi na sita ambayo yalimwezesha mtafiti kuyachanganua

kutegemea madhumuni, maswali ya utafiti na mihimili ya nadharia mbili zilizouongoza utafiti.

- 6) Kulikuwa na changamoto ya mtafiti kuweza kushikwa na uoga wa kusongea karibu na mahali ambapo fahali walikuwa wakipigania kwa vile wengine walikuwa wakubwa na wakali sana.
- 7) Ili kupata na kushuhudia miviga halisi ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*, mtafiti alihudhuria sherehe tatu za mazishi ya mashujaa walioaga katika jamii hii, kwa hivyo, mtafiti alizipata sherehe hizo kwa kuelekezwa na fanani wajigambi katika sherehe hizo. Ingawa hivyo, dhana ya kifo si ya kutegemea kwa kuwa kulikuwa na watu kutoka katika nasaba mbalimbali walioaga dunia lakini hawakupata fursa ya kufanyiwa sherehe hiyo kwa vile hawakuwa mashujaa. Ingawa hivyo, mtafiti pia alipata data kutoka kwa sherehe za *Mchezasili* wa *Mayo* kwa vile ni *Shilembe* katika upya na hutokea karibu kila Jumamosi au kila kunapokuwa na sherehe kama za siku ya Mashujaa na kadhalika.
- 8) Mtafiti alikumbwa na changamoto ya kukosa baadhi ya sherehe kwa vile nyingine hufanyika asubuhi na mapema zaidi mwendo wa saa moja hadi saa tatu asubuhi, hivyo basi, mtafiti alikuwa akifika wakati mwingine sherehe zikiwa zimeisha kwa sababu ya shida ya usafiri. Kwa hivyo, mtafiti alipata nafasi ya kwenda kuishi na watafitiwa na shida hiyo ikatatuliwa.

### **3.14 Hitimisho**

Sura hii imejadili muundo na mbinu za utafiti wetu. Imefafanua namna ambavyo utafiti ulifanywa. Sura hii imebainisha mbinu mahsusi za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu. Imeweza kuufafanua muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, umma lengwa, uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data, uthabiti wa vifaa, uaminifu wa data, majaribio ya vifaa vya utafiti, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, maadili ya utafiti pamoja na changamoto zilizokumba utafiti huu.



## SURA YA NNE

### UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

#### 4.1. Utangulizi

Katika sura hii, kuna uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yaliyokusanywa uwandani kwa kutumia mahojiano, uchunzaji-shiriki na utazamaji, kamera za video, kinasasauti na mijadala huru. Data ilichanganuliwa kwa mtindo wa kimaelezo kwa kutumia maelezo ya kifafanuzi na mifano, picha, vielelezo na filamu halisi. Imejikita katika uhakiki, ubainishaji na upambanuzi wa jinsi vipashio mbalimbali vya lugha; nomino, vishazi na vitenzi pamoja na kipengele cha kiisimu; semantiki katika majigambo ya Waisukha husawiri ubabedume. Lugha ni chombo muhimu sana ambacho msanii yeyote yule hukifumbata ili kumwezesha kuyapitisha maudhui, ujumbe na matakwa yake hadi kwa hadhira husika. Vilevile, lugha husheheni mila, utamaduni, desturi, itikadi, mitazamo, matarajio na mielekeo mbalimbali ya jamii. Utafiti ulijikita katika kuchunguza nafasi ya lugha, kuangazia historia na itikadi yao na namna zinavyojenga, kuendeleza na kudumisha ubabedume kupitia kwa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Ili kulifikia lengo hili, tumetumia majigambo mbalimbali yanayoghaniwa na wasanii wakati wa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* kama ithibati mwafaka ya kuendeleza uchanganuzi na mijadala wetu.

## **4.2 Nomino, vishazi na vitenzi vinavyosawiri ubabedume**

Uchunguzi ulifanywa kuhusu ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha. Msingi wa shabaha hii ni kauli ya Matinde (2015) akimnukuu Fiske (1994) na kuhoji kuwa maneno yaliyoandikwa au kusimuliwa husimba fahiwati pana kuhusu hali mbalimbali za kijamii, kiitikadi, kihistoria, kisiasa na kiuchumi. Hali hizi zote husawiri uhalisia wa kijamii hususan falsafa, mitazamo, mielekeo na matarajio ya wanajamii kuhusu mahusiano ya uana na mamlaka katika jamii.

### **4.2.1 Kipashio cha nomino**

Habwe na Karanja (2004) wanafafanua nomino kama neno ambalo hutaja mtu, kitu, hali, mahali, dhana na tendo. Kisintaksia nomino ni kategoria ya kileksika ambayo uamilifu wake hubainika katika hali zifuatazo;

- i. Nomino ni neno kuu katika kirai nomino au kiima.
- ii. Nomino huchukua nafasi ya shamirisho au yambwa.
- iii. Ni kijalizo.
- iv. Hutawala utokeaji wa maneno mengine katika sentensi ili sentensi iwe na upatanisho wa kisarufi.

Nomino huwa ni za aina mbalimbali. Kuna nomino za pekee, za kawaida, nomino dhahania, za makundi, za wingi na za kitenzi Jina.

Kigezo cha nomino kama kipashio cha lugha kinachosawiri ubabedume kilibainika katika baadhi ya majigambo ya Waisukha.

Tunaweza kuyarejelea majigambo ya 4 na 6.

#### **Jigambo la 4**

*Osama mwana wa tata  
Mumbulihitsi bulayi  
Uwira mundu mushikuri shukhulwaninya*

*tsichilishi yakura ichilishi ingali*

*Nivakhupa itsifirimbi  
Nabo bakhali bakhuba tsisauti tsindayi  
Venyalanga amenyali*

Osama mwana wa baba  
Mnisikilize vizuri  
Aliyeua mtu kwenye mlima wa  
Kupigania  
Mafahali walishinda fahali  
Mkubwa  
Wakapiga filimbi  
Nao wanawake walipiga sauti nzuri  
Wanaenda haja ndogo  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

Katika jigambo hili la 4 kuna matumizi ya nomino zilizobeba ubabedume. Mshororo wa tano una nomino ya kawaida ‘itsifirimbi’ lililo na maana ya filimbi au kipenga katika Kiswahili. Neno hili limetumika kurejelea ushindi unaotokana na fahali aliyeshinda katika sherehe ya miviga ya *Shilembe* au *Mchezasili* wa *Mayo*. Katika jamii ya Waisukha, wakati wa sherehe hizi, kipenga hupulizwa tu kama ishara ya ushindi. Dhana hii hutumika kurejelea fahali wenye ‘nguvu’ na vilevile kumdhalilisha fahali ‘mzembe’. Mshindi hujulikana kama mume kamili ilhali mshinde hujulikana kama mume aliyehasiwa au mwanamke asiye na nguvu.

#### **Jigambo la 6**

1. *Inzi ni muyayi wa tata  
Wavaya tsichilishi tsinyishi  
Tsiamela tsinziga  
Tsiasinjila vulahi  
Bahilana ni bibula bana banyishi  
Ni bilachi ya malova  
Indavu nende imwamu, manya isekese*

2. *Tata ni mubayi witsichilishi tsiakhomela  
Sindateshia tawe habula omwana wanje  
Alangungwa Spana  
Utechilitsanga shibala shiosi shi  
Tsimbia tsiosi tsi Isukha*

Mimi ni kijana wa baba  
Aliyewafuga fahali wengi  
Wameota pembe  
Zilizosimika vizuri  
Wakaoana na kuzaa watoto wengi  
Wengine ni wa kikahawia  
na meusi mfano wa tausi

Baba ni mfugaji wa fahali wanene  
Sijaoa ila mwanangu  
Anaitwa Spana  
Anayetemesha nchi yote  
Na koo zote za Waisukha.

*Bakhali vosi bamuyanza*

Wanawake wote wanampenda  
(Tafsiri: Mtafiti)

Katika jigambo hili la 6, nomino ya kawaida pia imetumika. Nomino hiyo inapatikana katika mshororo wa tatu wa jigambo hilo. Nomino hiyo ni ‘tsinziga’ linalomaanisha pembe katika Kiswahili. Kulingana na jamii ya Waisukha, pembe za fahali hunolewa siku tatu kabla ya mapigano. Kwa mujibu wa nadharia ya UCHAMAWADI, huku kunolewa kwa pembe ni ishara ya ubabe kwa vile, ushindi hupatikana kwa kupenyeza pembe zilizosimika katika mshindani wake. Ubabe hujitokeza pale ambapo pembe inamithilishwa na dhakari ambayo ikishasimika inapata uwezo na nguvu za kutenda tendo la ngono kwa kubikiri, kupachika mimba na kumstarehesha mwanamke miongoni mwa dhima zake. Ndiposa Izugbara (2005) anaeleza kuwa umbo la dhakari la ubenuzi na hali ya kutokuwa na haya na kuwa ngumu, kubwa na dhabiti na yenye nguvu wakati wa mchechemo inaonyesha uwezo wake. Dhana hii ndiyo inayomithilishwa na nguvu za pembe na kuibua dhana ya ubabedume katika majigambo ya Waisukha.

### **Jigambo la 6**

2. *Tata ni mubayi witsichilishi tsiakhomela  
Sindateshia tawe habula omwana wanje  
Alangungwa Spana  
Utechilitsanga shibala shiosi shi  
Tsimbia tsiosi tsi Isukha  
Bakhali vosi bamuyanza*

Baba ni mfugaji wa fahali wanene  
Sijaoa ila mwanangu  
Anaitwa Spana  
Anayetemesha nchi yote  
Na koo zote za Waisukha.  
Wanawake wote wanampenda  
(Tafsiri: Mtafiti)

Katika jigambo hili, kuna nomino ya kawaida katika ubeti wa pili mshororo wa tatu ambapo nomino Spana limetumiwa. Jina hili Spana katika jigambo hili ni mfano wa jina la majazi kama lilivyo Osama. Spana kimsingi ni kifaa kitumiwacho kufungulia nati, (TUKI, 2004), kwa hivyo, jigambo hili linarejelea dhakari ya mwanamume iliyo na

uwezo wa kufungulia nati za aina mbalimbali. Katika hali hii, dhana hii inarejelea fahiwa ya uhuru na ukware wa watu wa jinsia ya kiume au wanaume. Wao wana uwezo wa kuwa na wanawake wengi, wawe wa halali au wa nje ya ndoa.

Katika jigambo hili, fanani mjigambi anaonea fahali uhodari wake wa kuweza kutongoza na hata kupata fahali wengi ilhali hajaoa. Hali hii ndiyo inayojenga ubabe wake. Kwa mujibu wa Izugbara (2005) anadhukuru kuwa matokeo muhimu huhusishwa na amali ya dhakari na upenyezi wake katika kupoteza ubikira na kutia mimba, hali inayoitawaza dhakari uwezo juu ya uhai na ufu. Dhakari ni kiungo muhimu cha mwanamume kinachonasibishwa na spana ambacho pia ni kifaa muhimu cha seremala na huwa na uwezo wa kufungua si nati tu bali hufanya kazi mbalimbali za kiufundi. Katika mantiki hii, mwanamume anajitokeza kama jinsia iliyo na silaha maalum inayokuza na kuujenga ushindi wake na kufanya kazi mbalimbali dhidi ya jinsia ya kike. Silaha hii ni chombo muhimu kinachojenga ubabedume katika jamii ya Waisukha.

Spana huyu anasemekana kuwa anaitetemeshwa dunia nzima na wanawake wote Waisukha na koo zao zote wanampenda. Inaonekana kwamba mwanamume huyu ni hawara kwa sababu wanawake hawa watampenda vipi kama hawajakumbana na spana yake? Hali hii inadokeza kuwa mwanamume anajitokeza kama jinsia yenye mamlaka na pia mwenye uamuzi dhidi ya masuala mbalimbali yanayohusiana na mapenzi. Kwa hivyo, muamuzi katika jamii ni mwanamume kwa vile ana akili ya kutumia spana yake ili kukidhi mahitaji ya wanawake. Dhakari ya mwanamume kama ilivyo spana ni silaha anayoitumia kuonyesha uwezo na mamlaka yake dhidi ya jinsia ya kike. Matumizi ya nomino *Spana* ni kidokezi cha mamlaka aliyo nayo mwanamume dhidi ya jinsia ya kike.

Ubabe unaojengwa na kudumishwa hujikita katika itikadi, falsafa, mielekeo na matarajio ya jamii ya Waisukha.

### **Jigambo la 9**

*Nachenda Isukha yiosi  
Nise Eminyi -elinyoni  
Nakona khali uwanja ndege  
Havakwanyinga tsichilishi  
Bakhanga khuli mulilu  
Mulili mwichenda nyama  
Babimanga bura  
bura bwi sumu  
Khumanyinya buhaka bwabwo  
Nibalwaninyanga tsichilishi*

Nimetembea Isukha kote  
Ndimi Eminyi-ndege  
Nikalala hata Kiwanja Ndege  
Wanaopiganisha fahali  
Wamewaka kama moto  
Moto wa jangwani  
Wanalenga mishale  
Mshale ukiwa na sumu  
Ili kuonyesha ushujaa wao  
Wanapopiganisha fahali  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

Tukirejelea jigambo hili mshororo wa pili, tunapata ya kwamba nomino inayotaja aina ya ndege imetumiwa. Neno hilo ni Eminyi, katika muktadha huu ni nomino ya pekee. Eminyi ni aina ya ndege anayetoka katika sehemu hii ya Magharibi mwa nchi ya Kenya. Ndege huyu huwa na sifa za hekima, ujasiri na ujanja. Fanani wanapojigamba katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* hupenda kulitumia jina hili kwa sababu wao hujihusisha na ndege ambaye si rahisi kumtega, husafiri kwa mwendo wa zigizagi na inaaminika kuwa anaweza kutumwa katika nchi za miungu. Sifa za hizi za uungu huhusishwa na ubabedume kama anavyodai Ruether katika mhimili wa tatu wa nadharia ya Uwezo-Uume. Mtaalam huyu anaeleza kuwa, katika mgawanyo wa majukumu, wanaume wameweka utambulisho wao katika sura na mfano wa mungu wa kiume kwa manufaa yao wenyewe. Anahoji kuwa mwanamume alipewa mwanamke kama mwenzi kutoka kwa mungu wa kiume.

## Jigambo la 11

*Nitsi Mike Tysoni  
Nuwisunda himbi handi  
Kenyanga wekasie ubulahi  
Habula ndio alanyakhana  
Rulanga mumuliango kwa Abisende  
Mwene itsichirishi tsyobucheli  
Vamanya khukhola avakhali vanyole tsinda*

Mimi ni Mike Tyson  
Ukisogea karibu nami  
Ni sharti ujihami vilivyo  
La sivyo utajutia laitani  
Mimi ni wa ukoo wa Avisende  
Mwenye fahali walio na hekima  
Wanajua kufanya ili wa kike wapate  
Mimba  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

Katika jigambo hili mshororo wa kwanza, fanani mjigambi anajirejelea kama Mike Tyson. Nomino hii ni ya pekee iliyojaa sifa tele za ubabedume. Kwanza kabisa, Tyson anajulikana kama bingwa wa uzani mzito na mpiganaji wa kutajika wa wakati wake. Kisa chake kimejulikana katika jamii nyingi redioni, runingani na hata katika vyombo vingine vingi vya habari. Amejulikana kote ulimwenguni kama shujaa wa upiganaji. Wenye fahali huwapa jina hili ili kuonyesha ushujaa. Tukirejelea nadharia ya UCHAMAWADI, mhimili wa nne unaeleza kuwa usemi ni historia. Tunapoitalii historia ya Mike Tyson na kulinganisha na usemi wa Waisukha katika majigambo tunapata ya kwamba hakisoma. Aliachia shule katika madarasa ya chini. Hata hivyo, ni shujaa kwa sababu anahusishwa na jela, ubakaji na upiganaji. Nadharia ya UCHAMAWADI inatusaidia kutambua kuwa, mwanamume ni mwanamume tu na ana sifa za ubabe hata kama hajasoma. Haijalishi kiwango chake cha elimu wala kimo chake, bora ana sifa za ubabe kama vile ujasiri, uvumilivu, ukware, uwezo na kuthubutu mambo miongoni mwa sifa nyingine. Dhana hii pia inasisitizwa na mhimili wa nne wa nadharia ya Uwezo-Uume. Izugbara anaeleza kuwa sifa angama za uwezo-uume ni sifa ambazo ni sharti mwanamume awe nazo ili kuweza kujenga, kudumisha na kudhihirisha ubabedume. Sifa hizi anazitaja kama; ukware, ujasiri, uvumilivu, kuthubutu mambo miongoni mwa sifa nyingine. Kulingana na

majigambo ya Waisukha, ni wazi kuwa Tyson ni shujaa kwa vile anamiliki sifa za ubabe kama ukware kwa sababu anahusishwa na kitendo cha ubakaji.

**Jedwali 4.1 Nomino zinazosawiri Ubabedume katika Majigambo**

<b>Jigambo</b>	<b>Nomino</b>	<b>Ubabedume</b>
1	Osama	Ushujaa
5	NARC	Nguvu za Mamlaka
6	Tsinziga	Kusimika kwa dhakari
6	Spana	Ukware
7	Master key	Ukiritimba
9	Eminyi	Hekima, Ujasiri na Ujanja
11	Mike Tyson	Bingwa wa ndondi
15	Bundi	Hatari kiitikadi

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

**4.2.2 Kipashio cha Kishazi**

Matinde (2012) akiunga mkono mawazo ya Vuzo na wenzake (2004) anafafanua kishazi kama neno au kifungu cha maneno chenye kiima na kiarifu peke yake ambacho huwa ni sehemu ya sentensi kuu. Kishazi humilikiwa na kutawaliwa na kifungu kingine cha maneno katika sentensi chenye hadhi kubwa. Maana ya kishazi hutegemea kifungu



kinachokimiliki na kukitawala. Kipashio kilicho muhimu ambacho hakina budi kuwepo katika kishazi ni kitenzi. Kitenzi kinaweza kuwa kinajitosheleza au hakijitoshelezi. Kishazi hupatikana katika kiwango cha Kisintaksia Kiisimu. Vishazi vimejitokeza katika majigambo ya Waisukha kama ifuatavyo:

#### **Jigambo la 4**

<i>Osama mwana wa tata</i>	Osama mwana wa baba
<i>Mumbulihitsi bulayi</i>	Mnisikilize vizuri
<i>Uwira mundu mushikuri shukhulwaninya</i>	Aliyeua mtu kwenye mlima wa kupigania
<i>tsichilishi yakura ichilishi ingali</i>	Mafahali walishinda fahali mkubwa
<i>Nivakhupa itsifirimbi</i>	Wakapiga filimbi
<i>Nabo bakhali bakhuba tsisauti tsindayi</i>	Nao wanawake walipiga sauti nzuri
<i>Venyalanga amenyali</i>	Wanaenda haja ndogo
	<b>(Tafsiri: Mtafiti)</b>

Katika jigambo hili mshororo wa saba, kuna kishazi ambacho kimetumika; ‘Wanaenda haja ndogo’. Kishazi hiki kimetumika kurejelea hali kuwa fahali wanapopigana wakati wa miviga ya *Shilembe* au *Mchezasili wa Mayo* wanastahili kwenda haja ndogo kwa vile hii ni ishara ya kuhusisha fahali na miungu aambayo inaaminika kuishi ardhini. Aliye na uwezo wa kumzalisha mke ni mume kwa hivyo kishazi hiki kinarejelea hali ya uendelezaji wa jamii kupitia kwa kuzaa. Katika muktadha huu, fahali wawili wanapopigana na mmoja wao aende haja ndogo, hiyo huwa ni ishara ya ubabe.

#### **Jigambo la 1**

<i>Mumbulihitsi bulahi</i>	Nisikilize vizuri
<i>Muhulili lwambolanga</i>	Msikie ninavyosema
<i>Khuli lwanza khuhila makhuba</i>	Nitavyozungusha usukani
<i>Khuli manyanga nitsi Osama</i>	Kwa vile ninavyojua ndimi Osama
<i>Wavananga tsinyanda</i>	Mvunja miamba
<i>Neshikulumi shisinjiye</i>	Na rungu iliyosimama wima
	<b>(Tafsiri: Mtafiti)</b>

Katika jigambo hili mshororo wa sita, kuna kishazi ‘rungu iliyosimama’. Wakati wa upiganishaji fahali, huwa kuna rungu na vijiti vinavyotumiwa na wapiganishaji fahali na fanani. Vifaa hivyo huwa vinasalia vikiwa vimesimamishwa wima angani wanapoendelea kushangilia fahali na ushindi wao. Rungu au fimbo ya nyayo kama tujuavyo ni ishara ya uongozi na ubabe. Hali hii ilijitokeza bayana katika majigambo ya Waisukha.

UCHAMAWADI unajibu madhumuni ya kwanza ambayo yalibainisha ubabedume kwa kuchunguza vipashio vya lugha ambavyo ni nomino na vishazi katika majigambo ya Waisukha. Uchanganuzi huo ulijikita katika kuchanganua majigambo yaliyoghaniwa na fanani wajigambi na fanani watambaji ili kubaini nomino na vishazi ambavyo hudhihirisha sifa hizo za ubabedume miongoni mwa Waisukha. Hali hii ilihusisha kutambua, kueleza na kufasiri majigambo yanayoathiri jinsi maana inasawiriwa na majigambo hayo na kuweza kudhihirisha ubabedume Van Dijk anapendekeza kuwa, ikiwa utafiti unalenga jinsi wazungumzaji fulani au waandishi wanavyosawiri uwezo na mamlaka kwa kutumia diskosi zao; basi uchunguzi utazingatia vile vipengele vya kimsingi katika diskosi kutegemea uamilifu wa mamlaka kijamii. Ndiposa utafiti huu ulijikita katika kuchunguza vipashio vya kimsingi vya lugha katika majigambo ambavyo vilikuwa ni nomino na vishazi katika muktadha huu. Vipengele hivi vilichanganuliwa kutegemea itikadi na utamaduni wa Waisukha.

#### Jedwali 4.2 Vishazi vinavyosawiri Ubabedume katika Majigambo

Jigambo	Vishazi	Ubabedume
1	Rungu iliyosimama	Uongozi au dhakari iliyosimika
4	Wanaenda haja ndogo	Uendelezaji wa jamii kwa kuzaa
14	Wanaotingisha viuno	Ukware

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

#### Jedwali 4.3 Vitenzi vinavyosawiri Ubabedume katika Majigambo

Jigambo	Vitenzi	Ubabedume
7	Ninajua kupiga isukuti	Uwezo kwa kumfurahisha mke kimapenzi
9	Wanalenga mishale	Wanatumia dhakari kubikiri mabinti
15	Ninasikia mnaniita	Bingwa katika vita au ukware

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

#### 4.3 Vipashio vya Lugha vinavyosheneni Ubabedume kwa mtazamo wa Kisemantiki.

Sehemu hii inashughulikia madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ambayo ni kubainisha, kuhakiki na kueleza namna ambavyo vipashio vya lugha katika majigambo ya Waisukha kwenye miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* husawiri ubabedume. Msingi wa madhumuni haya ni mawazo ya Van Dijk (2000) anayedai kuwa maneno ya wenye uwezo katika jamii huchukuliwa kuwa ya ukweli na yenye uamilifu wa kipekee katika

kuhalalisha hali mahsusi za kijamii, ilhali kwa wale ambao hawana uwezo maneno yao hudunishwa na kupuuzwa na kusemekana kuwa yanashangilia jinsi hali ilivyo katika jamii. Hali hii ndiyo iliyouwezesha utafiti wetu kupata jukwaa la kuweza kuchanganua namna vipashio mbalimbali vya lugha ya majigambo huweza kujenga, kusawiri, kudumisha na kushamirisha ubabedume katika jamii ya Waisukha kwa kurejelea kipashio cha kiisimu ambacho ni semantiki.

Lugha ni kipengele muhimu katika maisha ya binadamu. Lugha inapostawi, fasihi yake pia hupata mwanya wa kujiendeleza. Katika mantiki hii, tajriba za maisha ya watu huhifadhiwa na kukuzwa. Kwa hivyo, majigambo kama kipera cha ushairi ni sehemu mojawapo ya utamaduni wa jamii (King'ei na Kemoli 2000). Kwa hivyo, kwa kuzingatia uwasilishaji wa majigambo ya Waisukha, inabainika kuwa kuna kauli teule zinazotumika. Hivyo, kauli hizi huweza kuwa zile zinazojikita katika mapokeo ya jamii na zile zinazobuniwa kibinafsi au kimaksudi na wasanii au fanani. Hii inatokana na sababu kuwa fanani ni mwanajamii ambaye ameshuhudia au ameathirika kwa mambo au masuala mbalimbali yanayotendeka katika jamii husika. Baadhi ya mambo hayo ndiyo yanayomhamasisha na kumpa ilhamu au kariha ya utunzi (Wamitila 2008).

Katika muktadha huu, fanani huteua maneno mahsusi ili kuusawiri ujumbe unaoakisi uhalisi wa maisha ya watu. Ingawa kimsingi sajili ya ushairi huwa ni mchanganyiko wa lugha ngumu na ile ya kawaida, ile ya kawaida ndiyo hutumika zaidi katika majigambo ya Waisukha. Labda ni kwa vile ni lugha ambayo inapatikana kwa urahisi katika maongezi ya kila siku katika jamii (Gibbe 1998). Hivyo, kutokana na matumizi hayo,

kipera hiki cha majigambo kinakuwa ni mwonzi wa maisha ya Waisukha kinachoakisi mila, desturi, itikadi na utamaduni wao na kusawiri ubabedume.

Fasihi ni sanaa inayotoa maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno yanayotamkwa au kuandikwa (Senkoro, 1982). Mawazo haya yanaungwa mkono na Mohamed (1995) anayehoji kuwa, aghalabu, kama si kila wakati, lugha huitikia wito wa kukidhi mahitaji ya falsafa na itikadi za msanii na jamii yake. Lugha ni kipengele muhimu sana kwa vile hutumiwa katika kuitenga fasihi na sanaa nyinginezo. Hivyo, lugha ndiyo nyenzo muhimu ambayo hutumiwa na msanii au fanani kupitisha itikadi, maudhui, mielekeo, mitazamo, falsafa na matarajio ya kijamii kwa hadhira. Katika hali hii, msanii wa majigambo hutumia vipashio mbalimbali vya lugha katika kutekeleza kusudi lake. Yaliyo ya manufaa kwa utafiti wetu ni kwamba msanii au fanani huweza kuibuni miundo na maumbo ya sauti yake, maneno, ujengaji wa jazanda, taswira na mpangilio wake ili kuitikia wito huo. Hali hii inadhihirika wazi katika baadhi ya majigambo. Kwa mfano tukirejelea jigambo la kwanza ubeti wa kwanza, tunaweza kutambua sifa za ubabe zikilinganishwa na Osama bin Laden aliyekuwa gaidi wa Al-Qaeda. Osama ni mmojawapo wa wale waliotekeleza mashambulizi ya kigaidi kule Urusi. Wanaotekeleza mashambulizi kama hayo huchukulia vitendo vyao kuwa vya kishujaa. Kuitwa waoga ni kama matusi kwao. Sifa za Osama zilitetemeshwa dunia nzima kwa ajili ya ujasiri aliokuwa nao, (Owala 2015). Kwa hivyo, ubeti huu unadhihirisha ushujaa na vilevile kuweka wazi itikadi, falsafa na matarajio ya kijamii kuhusu umuhimu wa sifa za kishujaa hususan za Mwanamume Mwisukha katika jamii ya Waisukha. Tazama jigambo hili la kwanza:

## **Jigambo la 1**

*Mumbulihitsi bulahi  
Muhulili lwambolanga  
Khuli lwanza khuhila makhuba  
Khuli manyanga nitsi Osama  
Wavananga tsinyanda*

Nisikilize vizuri  
Msikie ninavyosema  
Nitavyozungusha usukani  
Kwa vile ninavyojua kuwa ndimi Osama  
Mvunja miamba  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

Katika ubeti huu, ukoo wa Vayokha wanaopenda kuwanasibisha fahali wao na shujaa Osama umeweza kudhihirisha na kuonyesha wazi itikadi na imani za nasaba hii. Kulingana na data tuliyoipata, si ukoo huu pekee ambao hujihusisha na shujaa huyu bali koo nyingine kama vile Avamilonje kutoka katika kata ya Ilala na pia Avayokha wanaotoka katika kata za Khayega na Museno na pia Avitsende walijinasibisha na jina hili la kishujaa kwa vile majigambo yalikuwa mengi na baadhi yao yalifanana. Hali hii ilikuwa muhimu katika koo hizi kwa vile kila wakati walitarajiwa kuwa juu kishujaa wakati wa kupiganisha fahali na nasaba nyingine zilizoaminika kutokuwa na ushujaa wa hali ya juu kama vile wa Osama. Koo hizi zilipoenda kupiganisha fahali na koo nyingine, iliaminika kuwa koo hizi zingeibuka washindi dhidi ya koo zile nyingine zilizoaminika kuwa za hali ya chini kishujaa. Umuhimu wa ng'ombe katika jamii umeoneshwa katika ubeti huu, muhimu ni kwamba, kulingana na Waisukha, wanaofaa kumiliki fahali wanaotumika katika mapigano ni wanaume na wala si wanawake. Hali hii inaweka wazi ujenzi na udumishaji wa ubabedume dhidi ya itikadi za jamii. Inaaminika kuwa Osama aliyetajwa ni mvunja miamba. Hii ina maana ya kwamba, hakuna shujaa mwingine kuliko Osama. Anaposhika usukani kila mtu hunyamaza na kumsikiliza, yaani anapoingia uwanjani kupigana, wote wanaomtazama; wazee kwa vijana na wakubwa kwa wadogo

huweka roho mikononi na kujua kuwa bila shaka ataibuka mshindi. Kisa na maana ni kwamba, yeye ni *mvunja miamba* kumaanisha ana nguvu zaidi za kuweza kupasua miamba kwa pembe zake tu. Nadharia ya UCHAMAWADI ilitusaidia hasa kwa kuurejelea mhimili wa pili unaoelezea kuwa uhusiano wa kimamlaka hutokana na usemi. Kwa kutumia mhimili huu, nguvu za kupasua miamba kwa pembe ni ile hali ya wanaume kuweza kuwabikiri wasichana kwa kutumia dhakari. Dhana hii inadhihirisha usemantiki katika majigambo haya.

Licha ya kwamba Osama alitekeleza mashambulizi ya kigaidi na akaaga dunia, wanaume Waisukha bado wameishikilia dhana hiyo ya kishujaa na inapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi kupitia kwa majigambo ili kuendeleza na kudumisha ubabedume. Wanawake na watoto nao hushuhudia tu sherehe hii kwa ajili ya kupata burudani wakati wa kucheza isukuti na kuimba nyimbo na vilevile kwa minajili ya kuchekeshwa na kupitisha wakati.

Fanani hutegemea ubunifu wake katika harakati ya kuteua sauti, neno, kirai, kishazi, sentensi na maana kwa ajili ya matumizi maalum hususan yanayolenga ujenzi wa taswira fulani. Hali hii ndiyo hurejelea vipengele mahsusi vya kiisimu kama vile, Mofolojia, Sintaksia na Semantiki. Uteuzi wa vipashio vya lugha katika majigambo hufumbata tamathali mbalimbali za usemi zinazojenga taswira tofautitofauti. Usemi huwa ni zaidi ya kipashio cha kiisimu kwa vile hufumbata na kusheheni mila, imani, itikadi na tajriba zinazowaelekeza wanajamii katika namna ya kuwaza na kufikiria, kutagusana, kuhusiana, kutenda, kusema na kushirikiana.

Matinde (2015) akiwarejelea De Beaugrande na Dressler (1981) anafasiri matini kama tukio la kimawasiliano na ambalo sharti likitwe katika vigezo saba muhimu: mshikamano, mchukuano, dhamira, ukubalifu, ueleweshaji au uarifishaji, muktadha na hali pamoja na mwingiliano tanzu (Rejelea maelezo zaidi katika 2.9 ). Wanaeleza kuwa, matini ni sharti iendane na sheria za utanzu mahsusi kwa vile kila utanzu wa fasihi huwa na sifa mahsusi za kiisimu, uamilifu faafu na hukitwa ndani ya mipaka maalum ya uzalishaji na upokeaji wa hali za kijamii. Kuna maana ya kijuujuu na maana ya kindani. Katika msingi huu, uchanganuzi na ufasiri wa vipashio vya lugha ya majigambo ya Waisukha ulijikita katika vigezo hivyo saba vya ufasiri na uchanganuzi wa matini au usemi vilivyopendekezwa na wataalam hao.

Katika muktadha huu, kwa kutumia ubunifu, mtafiti pia alijikita katika kutafuta dhana maalum iliyoweza kuonisha vipengele vya kiisimu na lugha ya kisanii ya fasihi. Dhana hiyo inajulikana kama tamathali za usemi kama anavyodai Simala (2013). Anaeleza tamathali za usemi kama maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na msanii ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi au kusema. Dhana hii iliusedia utafiti huu kuzua hali ya mwingiliano taaluma kwa vile kuna vipengele kadhaa katika maelezo ya Simala vinavyohusu taaluma ya Isimu na vilevile taaluma ya Fasihi. Kwa mfano, katika maelezo yake kuna dhana ya sauti inayojikita katika taaluma ya Kifonetiki na Kifonolojia. Kuna dhana ya nomino inayorejelea taaluma ya Kimofolojia, vishazi inayoashiria taaluma ya Kisintaksia na maana inayorejelea taaluma ya Semantiki. Mtindo nao hurejelea mbinu inayotumiwa na msanii ili kudhihirisha upekee wa kazi



yake. Hali hii ndiyo iliyosaidia utafiti huu kutambua kipengele cha kiisimu, Semantiki na vilevile vipashio vya lugha hususan nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo.

Kwa upande mwingine, tamathali za usemi hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya Fasihi na kuongeza utamu wa lugha (Senkoro, 1985; Gafkosoft, 2017). Mawazo ya wataalam hawa yanasisitiza dhima ya tamathali ya kuwasilisha maana, mtindo na kupamba lugha. Hata hivyo, ingawa neno tamathali lina asili yake katika neno mithilisha lenye maana ya kufananisha, ni muhimu kufahamu kuwa tamathali za usemi hufanya kazi ya kufananisha dhana moja kwa nyingine tofauti. Aghalabu hutumiwa kurejelea usemi ubadilishao maana dhahiri au za kawaida za maneno kuleta maana maalum ya fasihi iliyokusudiwa na msanii. Wataalam hawa wanakubaliana kwamba ni fungu la maneno lililogeuzwa maaana yake ili kuwakilisha maana nyingine. Kwa hivyo, katika tamathali za usemi kuna maana na matumizi mengine ya kisanii (Msokile, 1992; Mwamanda, 2008). Janovsky (2014) anahoji kuwa tamathali za usemi kwa ujumla ni hali ya kuzungumzia jambo kwa kumaanisha jingine. Katika kazi hii, tamathali za usemi zimetumika kurejelea kipengele cha kiisimu ambacho ni semantiki na pia vipashio vya lugha kama vile majazi, taswira, chuku, takriri miongoni mwa vingine.

#### **4.2.1.1 Majazi na Semantiki**

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2015) inasema kuwa majazi ni jina analopewa mtu ambalo hufanana na tabia au umbile lake kwa mfano Cheupe, Kidevu na Majivuno. Mwita (2005) anaeleza kuwa dhana ya majazi inarejelea mbinu wanayotumia wasanii wa kazi za kifasihi ili kumpa mhusika jina linalolingana na sifa, matendo au hulka zake.

Naye Wafula (1999) anafafanua kuwa majazi ni mbinu kongwe, aghalabu inapotumiwa na wanafasihi huwa imenuiwa kuoanisha majina ya wahusika au mahali na dhana, hisia au tajriba zinazowasilishwa na kukisiwa katika katika majina hayo. Wamitila (2003) anasema majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi au yanayotuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Kutokana na fasili za wataalam hawa, hadhira huweza kubaini tabia ya mhusika au fanani na nafasi yake katika kuweka wazi lengo la jigambo lake.

Katika majigambo ya Waisukha, fanani hutumia vipashio mbalimbali vya lugha kufumbata majazi yanayolenga katika kujenga, kuendeleza na kudumisha picha mbalimbali za ubabedume kutegemea mjigambi husika. Mawazo ya Simala (2012) yanaonyesha utata katika dhana ya mafumbo ambayo huwa na istilahi nyingi kama vile tashbihi, uhaishi na jazanda. Anahoji kuwa, hizi ni tamathali za usemi zinazohusiana na maana za kauli. Katika msingi huu, cha kigezo cha maana pia huweza kudhihirika katika majazi. Anavyodai Matinde (2012), semantiki ni taaluma inayojikita katika ufasiri wa maana katika kiwango cha sentensi kwa kuchunguza miundo mbalimbali kwa mfano anomali, ukinzani, itkisadi na utata miongoni mwa miundo mingine. Katika majigambo ya Waisukha, hali hii pia ilidhihirika katika baadhi ya majigambo. Tazama jigambo la 6, ubeti wa pili:

### **Jigambo la 6**

1. *Inzi ni muyayi wa tata*  
*Wavaya tsichilishi tsinyishi*  
*Tsiamela tsinziga*  
*Tsiasinjila vulahi*  
*Bahilana ni bibula bana banyishi*

Mimi ni mvulana wa baba  
Aliyewafuga fahali wengi  
Wameota pembe  
Zilizosimika vizuri  
Wakaoana na kuzaa watoto wengi

*Ni bilachi ya malova  
Indavu nende imwamu, manya isekese*

Wengine ni wa kikahawia  
na meusi mfano wa tausi

2. *Tata ni mubayi witsichilishi tsiakhomela  
Sindateshia tawe habula omwana wanje  
Alangungwa Spana  
Utechilitsanga shibala shiosi shi  
Tsimbia tsiosi tsi Isukha  
Bakhali vosi bamuyanaza*

Baba ni mfugaji wa fahali wanene  
Sijaoa ila mwanangu  
Anaitwa Spana  
Anayetemesha nchi yote  
Na koo zote za Waisukha.  
Wanawake wote wanampenda  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

#### **4.2.1.2 Tashbihi na Semantiki**

TUKI (2004) wanaeleza tashbihi kama msemu wa kulinganisha ambao hufananisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno: kama, ja, mfano wa, kana kwamba au mithili ya.

Mwita (2005) akikubaliana na hoja hii anahoji kwamba tashbihi ni maneno yanayofananisha jambo, kitu, hali au kitendo na kingine kwa kutumia vihusishi kama vile, kama, mfano wa, ja, mithili ya na mengine mengi. Mawazo ya wataalam hawa yanakaribiana na Kimani na Chimera (1999: 32) wanaodhukuru kuwa tashbihi ni maneno yanayofananishwa (au kushabihisha) kitu, jambo au kitendo na kingine kwa kutumia vihusishi kama vile kama, ja, mithili ya, mfano wa na kadhalika. Hivyo, fasili za wataalam hawa zinafumbatwa na Arege (2002: 61) anayesema kuwa:

Tashbihi ni dhana ambayo inatumiwa katika kurejelea hali yoyote ile ya ulinganishi wa watu au vitu na watu au vitu vingine kwa kutumia maneno ya kuungia kama vile, mithili ya, mfano wa, kana kwamba, ja, sawa na miongoni mwa mengine. (TY).

Kauli za wataalam hawa ni muhimu kwa vile zinarejelea ile hali ya kufananishwa kwa vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno ya kulinganisha. Hii ni mbinu inayotumiwa katika kulinganisha kwa kuchora picha au taswira halisi kuhusu kusudi la msanii.

Anayejigamba hujifananisha na vitu au hali nyingi na wala si wanyama tu. Anaweza kujifananisha na aila yake, wazazi wake, mashujaa fulani katika jamii, waasisi wa jamii yake, miamba, moto na vitu vingine vilivyo hatari katika ulimwengu kijumla. Msanii hutumia vipashio mbalimbali vya lugha vinavyosheheni tashbihi na ambavyo hujenga ubabedume. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi fanani mjigambi anavyotumia kipashio hicho cha lugha katika kukuza na kudumisha ubabe na taswira za kiuwezo kwenye majigambo ya Waisukha wanapopiganisha fahali. (Taz. jigambo la 8, mshororo wa nne). Fanani mjigambi anasema, ‘Mwenye nguvu kama simba’ kurejelea fahali wa ukoo wa Avateheli ambao hawashindwi kamwe vitani hususan wanapopiganisha fahali. Tashbihi hii inarejelea ukali wa mwanamume ambaye akiwa katika boma hakuna anayethubutu kuleta mchezo au kufanya mambo ya kiupuzi, awe ni bibi au mkewe, watoto na hata majirani. Ukali wa simba umetumiwa kama kiarifu kidokezi cha nguvu na uwezo alio nao mwanamume bila kuhitaji msaada wowote. Isimu maana ama semantiki huchunguza maana katika lugha ya binadamu (Habwe na Karanja, 2004).

Katika hali hii, ni bora kutambua kuwa Majigambo ya Waisukha yalijikita katika kuweka wazi matumizi ya tashbihi na vilevile matumizi ya kiwango cha Kiisimu cha Semantiki ili kudhihirisha na kusawiri ubabedume. Katika kuangazia kiwango cha Kisemantiki, (tazama mshororo wa kwanza katika jigambo la 16 kwenye kiambatisho B) Fanani mjigambi hutumia tashbihi kujilinganisha na ushujaa fulani. Katika majigambo, tashbihi aghalabu hutumiwa katika ulinganishi wa watu, wanyama, hirimu, hali, ukoo au nasaba na vitu vingine mbalimbali ili kuonyesha sifa za kiubabe. Kwa upande mmoja, mwanamke huweza kupewa sifa zilizo duni au zilizodhalilishwa na kumlinganisha na

wanyama waoga kama vile kunguru ilhali mwanamume hulimbikiziwa sifa za kumjenga kama mwenye uwezo, maamuzi, mamlaka, shujaa na huweza kulinganishwa na wanyama hatari, hali ngumu na vitu mbalimbali na vyenye nguvu katika jamii kama vile, moto, radi, mwamba, ngwena, chatu na kadhalika. Hivyo, mwanamke huonekana kama jinsia tegemezi ambayo, kulingana na mila, itikadi, desturi na utamaduni wa Waisukha, wako chini ya mamlaka ya jinsia ya kiume. Hebu rejelea majigambo ya 8, 9 na 16 yanavyozua ubabedume kitashbihi kwa mtazamo wa kisemantiki:

### **Jigambo la 8**

*Luyia lwa Bateheli*  
*Khali namenesh angwetsanga*  
*Khuvumishi masamba kishimwa*  
*Mwene tsingulu khuli isimba*  
*Hurenjitsanga shibara shioishi*  
*Khuli shivala shia shikuri shitsi ndege*  
*Khuli shiahionilwa vulavu*

Wa ukoo wa Avateheli  
Hata akivunjika huungwa  
Kwa kutumia dawa ya kienyeji  
Mwenye nguvu kama simba  
Anayetemesha dunia nzima  
Kwenye eneo kame la uwanja ndege  
Kama kwamba linachochewa nuru  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

### **Jigambo la 9**

*Nachenda Isukha yiosi*  
*Nise Eminy-linyoni*  
*Nakona khali uwanja ndege*  
*Havakwanyinga tsichilishi*  
*Bakhanga khuli mulilu*  
*Mulili mwichenda nyama*  
*Babimanga bura*

Nimetembea Isukha kote  
Mimi ndiye Eminy-ndege  
Nikalala hata Kiwanja Ndege  
Wanaopiganisha fahali  
Wamewaka kama moto  
Moto wa jangwani  
Wanalenga mishale

*bura bwi sumu*

Mshale ukiwa na sumu

*Khumanyinya buhaka bwabwo*

Ili kuonyesha ushujaa wao

*Nibalwaninyanga tsichilishi*

Wanapopiganisha fahali

**(Tafsiri: Mtafiti)**

## **Jigambo la 16**

1. *Omuhaka nitsi wonyene*

Shujaa ni mimi tu

*Mwene tsingulu khuli isimba*

Mwenye nguvu kama simba

*Nitsi owamanya okhulwanya itsichirishi*

Mimi ninajua kupiganisha fahali

*Sinjendananga vutswa tawe*

Sitembeitembei tu ovyo

*Khandi mbula bulalu*

Tena sina kichaa

2. *Inzi mwaaninya*

Mimi ninapiganisha

*Tsichirichi khuli*

Fahali kama ambaye

*Manya sinanwaninje*

Sitafanya hivyo

*Kho khandi*

Tena

**(Tafsiri: Mtafiti)**

### **4.2.1.3 Chuku na Semantiki**

Dhana ya chuku imefasiliwa na Kimani na Chimera (1999) kama hali ya kutia chumvi kwa minajili ya kuathiri hisia. Wanaeleza kuwa chuku hudokeza hali ambayo inakiuka mipaka ya kiuhalisia. Tamathali hii imetumika na semantiki katika utafiti huu kuonyesha kuwa inajengwa na vipashio vya lugha ambavyo kwa namna ya kipekee hutumiwa na msanii kujenga picha aliyoikusudia yeye mwenyewe. Katika majigambo ya Waisukha kuna upigaji chuku ambao mjigambi anatomia ili kujenga na kukuza sifa za ubabedume. Kwa mfano, katika jigambo la 11 mshororo wa 6, kuna upigaji chuku kwa vile msanii anasema kuwa ‘fahali wa wa ukoo wa Avisende wanajua kufanya ili wanawake wapate

mimba.’ Msanii ametumia sifa ya kujua kufanya kama kidokezi muhimu cha ubabedume unaojengwa na utendaji wa umbile la kiume kisemantiki. Rejelea jigambo la 11 lifuatalo.

### **Jigambo la 11**

<i>Nuwisunda himbi handi</i>	Ukisogea karibu nami
<i>Kenyanga wekasie ubulahi</i>	Ni sharti ujihami vilivyo
<i>Habula ndio alanyakhana</i>	La sivyo atajutia laitani
<i>Rulanga mumuliango kwa Abisende</i>	Mimi ni wa ukoo wa Avisende
<i>Mwene itsichirishi tsyobucheli</i>	Mwenye fahali walio na hekima
<i>Vamanya khukhola avakhali vanyole tsinda</i>	Wanajua kufanya wake wapate mimba
<i>Avasiani avarambi tsifuti tisa</i>	Wavulana warefu futi tisa
	<b>(Tafsiri: Mtafiti)</b>

Upigaji chuku pia umejitokeza katika jigambo hili la kumi na moja katika mshororo wa mwisho unaosema ‘wavulana warefu futi tisa’. Fanani mjigambi ameitumia sifa ya urefu wa mwanamume kuashiria dhana ya ubabedume unaojengwa na maumbile ya wanaume. Wanaume wa ukoo wa Abisende wanaaminika kuimiliki sifa hii ya urefu wa futi tisa ambao ni urefu unaoweza kukatwa mara mbili na kuumba watu wengine wawili. Hali hii inazua ubabedume kwa misingi kuwa urefu wa mwanamume huangazwa kwa njia chanya ilhali ufupi wa mwanamume huangazwa kwa njia hasi. Hata hivyo, kuna baadhi ya fanani watambaji wanaodokeza kuwa urefu au ufupi wa mwanaume haujalishi, lililo muhimu ni sifa za ubabe.

Katika ubeti huu, fanani mjigambi anapiga chuku kwa kutudokezea kuhusu kumiliki fahali wenye hekima ambao ni wanaume wanaojua kutafuta mali katika jamii. Wanaume ndio wanarejelewa kuwa wenye akili katika jamii hii. Kwa hivyo, wao ndio wana akili ya kuweza kumiliki mali dhidi ya wanawake nahata kuweza kuitunza mali hiyo.

#### 4.2.1. 4 Jazanda na Semantiki

Mwita (2005) anasema kuwa jazanda ni maneno yanayotumika kugubika ujumbe fulani. Msikilizaji au msomaji hana budi kulifumbua fumbo hilo iwapo atapata ujumbe unaodhamiriwa. Kimani na Chimera (1992) nao wanahoji kuwa jazanda ni mafumbo ambayo ndanimwe maana ya kitu imefichama. Ni sawa na istiara, yaani, ‘kilichosetiriwa’. Naye Wamitila (2003) anaihusisha jazanda na taswira. Mawazo ya wataalam hawa yalikuwa msingi bora katika utafiti huu. Katika mantiki hii, tukirejelea majigambo ya Waisukha, wasanii wengi hutumia jazanda hususan katika kuibua taswira mbalimbali zinazoonesha ubabedume. Jazanda hizi hutumiwa kisemantiki katika usimbaji na matumizi ya baadhi ya maneno ambayo yanatumika katika kurejelea falsafa, mitazamo, mielekeo, matarajio na thamani za kijamii kuhusu sifa mbalimbali za ubabedume. Rejelea jigambo la 14 lifuatalo:

#### Jigambo la 14

*Nitse mwirolu wamanyikhana  
Owamanya okhulwanyanga itsichirishi  
Ndayanzwa ni tsingombe tsinyingi  
Tsisievitsanga visindi  
Khurula muluyia lwa Vayokha  
Ndahura vandi voosi  
Mbetsaanga imberi vuri lwosi  
Ndahura khuri itai  
Vandi vali inyima khuri likoti*

Mimi ni mjigambi hodari  
Ninayejua kupiganisha fahali  
Ninapendwa na ng’ombe wengi  
Wanaotingisha viuno  
Kutoka ukoo wa Vayokha  
Ninawashinda wengine wote  
Niko mbele kila mara  
Kama tai  
Wengine wako nyuma kama koti  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

Katika jigambo hili, jazanda imejitokeza katika kauli hii ‘mimi ni fahali hodari ninayependwa na ng’ombe wengi’. Jazanda hii inaashiria ukware kama sifa kuu ya ubabedume. Hii ina maana kwamba wanaume ndio wana uwezo wa kuoia wanawake wengi katika jamii kinyume na wanawake.



#### 4.2.1.5 Methali na Semantiki

Arege (2002) katika Matinde (2015) anaeleza kuwa methali ni fungu la maneno yaliyotumiwa pamoja kisanii yenye maana ambayo ni ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa. Methali huwa na dhima mbalimbali katika jamii, kwa mfano huweza kutoa maadili, kukejeli, kukaripia na kupitisha hekima mbali na kusawiri na kuyakinisha mandhari ya kitamaduni ya jamii inayozitunga na kuzitumia.

Katika utafiti huu kuna methali ambazo zimetumika katika majigambo ili kubainisha itikadi za kiubabe. Mathalan katika jigambo la pili, 'Fahali n moto wa koko, usipowaka utafuka'. Methali hii katika Kiswahili huwa hivi: Mume ni moto wa koko, usipowaka utafuka. Katika utafiti huu, methali hii inarejelea sifa za mwanaume au hata kuzisambaza mbegu zake mahali pengi, yaani kuzaa watot wengi na wanawake tofauti. Rejelea jigambo la pili lifuatalo:

#### Jigambo la 2

*Bisukha oyee!*

*Nitsi itaywa*

*Bisukha yaa!*

*Mbulili mnanganga*

*Muliango kwa mundu hu moyo mulayi*

*Ichirishi no muliro mukali*

*Nikulahamba kulatuma*

*Mulwani hatari hukhabaila*

Waisukha oyee

Ni mimi jogoo

Waisukha yaa

Nimesikia mmeniita

Mlango wa mwenye moyo safi

Fahali ni moto wa koko

Usipowaka utafuka

Mpiganaji hodari msimchezee

**(Tafsiri: Mtafiti)**

#### Jedwali 4.4 Tamathali za Usemi zinasawiri Ubabedume katika Majigambo

Jigambo	Tamathali za Usemi	Mfano	Ubabedume
2	Methali	Fahali ni moto wa koko usipowaka utafuka	Sifa za mwanamume kusambaza mbegu zake mahali pengi
6	Tashbihi	Mwenye nguvu kama simba	Nguvu za kiume
7	Majazi	Master key	Uwezo wa dhakari kufanya kazi anuwai
11	Chuku	Wavulana warefu futi tisa	Ubabe wa kimaumbile
14	Jazanda	Fahali kutoka katika ukoo wa Vayokha wanaopendwa na ng'ombe	Ukware

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

#### 4.3 Lugha, historia na itikadi zinavyosawiri ubabedume katika majigambo

Itikadi ni dhana inayorejelea mfumo wa fikra na imani katika jamii yoyote ile aidha ni mchakato wa kijamii ambao hujenga na kushamirisha mtazamo wa kiulimwengu wa jamii husika. Itikadi za kijinsia ni kama seti ya imani ambayo hutawala uhusika wa wanajamii katika nyanja mbali mbali kufuatana na matukia ya jamii.

Katika jamii ya Waisukha, tofauti za kiwana huanza kujengwa punde tu mtoto anapozaliwa, hapo ndipo wanajamii wanaanza kutoa majukumu mbalimbali kwa jinsia ya kike na jinsia ya kiume. Nafasi ya mwanamke na mwanamume katika jamii hii ni muhimu sana kwa vile huonekana katika majukumu mbalimbali, kwa mfano, wasichana hupewa majukumu ya kupika, kuosha vyombo na kadhalika. Kwa upande mwingine wanaume hupewa majukumu ya kiume katika jamii hii ni kuchunga ng'ombe, kufyeka na

kulinda mji. Kwa hivyo nafasi ya mwanamume na mwanamuke katika jamii hii ni muhimu sana kwani ndiyo huratibu wakilishi uhusika na utendaji wao katika majukumu mbalimbali kuanzia utotoni hadi utu uzima.

Fasihi simulizi kupitia kwa lugha ya majigambo ya Waisukha ilikuwa na nafasi muhimu katika kukuza na kuendeleza ubabedume katika jamii hii.

#### **4.4 Sifa angama za ubabedume**

Jamii ya waisukha kupitia kwa lugha ya majigambo ilikuwa na uwezo wa kudhihirisha ubabedume kupitia kwa miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* katika upiganishaji wa fahali. Majigambo yalidhihirisha kwamba mwanamume ni shujaa, shupavu, mwenye akili na anayetokeleza majukumu muhimu katika jamii. Hivi kwamba, mwanamume husawiriwa kama aliye na mamlaka juu ya mwanamke.

##### **4.4.1 Ushujaa**

Jamii ya waisukha humkuza mwanamume kama shujaa katika vitendo vya upiganishaji fahali, hivyo basi ushujaa na uwezo ni sifa ambazo mwanamume mwisukha anafaa kudhirisha kila mara kinyume na sifa zinazomfanya achekwe na wanaume wengine na hata wanawake.

Mwanamume Mwisukha anafaa kuwa na tabia na mazoea ya kustahimili shida na vitendo vya hatari kama vile kupiganisha fahali. Ifahamike kwamba, fahali wanapopigana ni tendo la hatari na hata huweza kusababisha kifo. Kwa hivyo, kila mwanamume anayejihusisha na upiganishaji wa fahali anafaa kuwa mkakamavu na asiyeogopa chochote hata kifo. Kwa mantiki hii, mwanamume yeyote anayedhihirisha tabia ya uoga hukeyeliwa na kulinganishwa na mwanamke.

Majigambo mengi ya waisukha yalionyesha kuwa wanaume ni mashujaa katika jamii hii.

Tazama jigambo lifuatalo:

### **Jigambo la 15**

<i>Sanditsi mno vaherwa</i>	Ahsante sana wapedwa
<i>Mburiranga munanganga</i>	Ninasikia mnaniita
<i>Itse mbuchiriye Ndiho!</i>	Nami nimeitikia Abe!
<i>Afwananga ichirishi ilwaninjwa kushirindwa</i>	Mithili ya fahali anayepigana kaburini
<i>Habula olwanwananga khusaya unangenge</i>	Lakini ninapopigana ninaomba uniite
<i>Khuriila likhuure</i>	Kwa jina bundi
<i>Ohuli nende elira lyahunya vukundu</i>	Mwenye jina lenye uvundo
<i>Eshibwi-inzogu khu bura</i>	Mbweha-ndovu kwa mishale
<i>Obura bululu vulisinja</i>	Mishale mikali iliyotisha
<i>Vasatsa niverukha nokhutsia mumilitu</i>	Wanaume wakitoroka na kuepea Msituni

**(Tafsiri: Mtafiti)**

Katika jigambo hili, ni wazi kuwa mjigambi anaufananisha ushujaa wake na ndege anayeogopwa sana aitwaye bundi. Inaaminika kuwa ndege huyu akiimbia karibu na boma, mtu huwa anakufa katika boma hilo au kijiji hicho. Rejelea mshororo wa sita katika ubeti huu. Hali hii inadokeza ujasiri wa mjigambi ambaye haogopi kuwa bundi ni ndege mbaya bali yuko radhi kujihusisha naye hata kama huleta kifo. Ina maana kuwa Mwanamume Mwisukha haogopi hata kifo. Yeye ni shujaa na jasiri. Kwa upande mwingine, bundi pia huashiria dhana ya hatari katika jamii. Katika muktadha wa jamii ya Waisukha, mwanamume Mwisukha amesawiriwa kama aliye na sifa za hatari na ambaye hatishwi na jambo lolote la hatari.

#### **4.4.2 Mvumilivu**

Khaemba (2013) anahoji kuwa mara nyingi mwanamume anatarajiwa kuwa na hekima na uwezo wa kumfanya kudumisha mamlaka, uvumilivu na uongozi katika jamii hali hii ndiyo huchangia katika kuwaweka wanajamii katika makundi mawili; mwenye uwezo na

asiye na uwezo kutegemea jamii husika. Mwanamume katika jamii ya Waisukha hafai kuonyesha udhaifu wowote na hastahili kukubali kushindwa katika sherehe yoyote ile ya kupiganisha fahali. Hata akishindwa hafai kuridhika kuwa ameshindwa hivyo anastahili kudhihirisha ubabedume hata kama tendo ni la hatari. Hivyo basi ni sharti awe tayari kufaulu katika azma yake bila kujali maumivu atakayokumbana nayo. Kwa hivyo anafaa kuwa mkakamavu anayevumilia shida, asiye mwepesi wa kuvunjika moyo awe radhi kuvumilia uchungu unaotokana na maumivu ya kimwili ilimradi apate anachokitaka. Hali hii ilijitokeza katika lugha ya majigambo ya waisukha. Rejelea jigambo la tisa lifuatalo:

### **Jigambo la 9**

*Nachenda Isukha yiosi  
Nakona khali uwanja ndege  
Havakwanyinga tsichilishi  
Bakhanga khuli mulilu  
Mulili mwichenda nyama  
Babimanga bura  
bura bwi sumu  
Khumanyinya buhaka bwabwo  
Nibalwaninyanga tsichilishi*

Nimetembea Isukha kote  
Nikalala hata Kiwanja Ndege  
Wanaopiganisha fahali  
Wamewaka kama moto  
Moto wa jangwani  
Wanalenga mishale  
Mshale ukiwa na sumu  
Ili kuonyesha ushujaa wao  
Wanapopiganisha fahali  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

Jigambo hili linadokeza jinsi msanii alivyotembea Isukha kote na akavumilia kwa kulala katika Uwanja wa Ndege. Anaeleza vile wanaopiganisha fahali wamewaka kama moto wa jangwa na pia kuna mishale inayolengwa ikiwa na sumu lakini wanastahili kuvumilia. Hali hii inamsawiri mwanamume huyu kama mtu mvumilivu na anayeweza kuikabili hatari yoyote. Dhana ya msanii huyu kuweza kutembea Isukha kote linaashiria ile hali ya mwanamume kuweza kuwa na uhuru wa kutembea pahali popote ili aweze kumpata

msichana wa kuo na kumtolea mahari. Hali inayoifanya jinsia ya kike kuendelea kuwa tegemezi huku ubabedume ukiendelea kudumishwa.

**Jedwali 4.5 Lugha, Historia na Itikadi zinavyosawiri Ubabedume**

<b>Jigambo</b>	<b>Uamilifu</b>	<b>Mfano</b>	<b>Ubabedume</b>
<b>5,6,7</b>	Lugha	Vipashio vya lugha kama nomino kmf. Spana, master key na NARC	Uongozi, Ushujaa, Ukiritimba nk
<b>2,3,4</b>	Historia	Majukumu wanayopewa wanaume na wanawake kijamii	Kujihusisha na kuumeni kuliko kuukeni kmf. J2.....chui wa baba (Ushujaa)
<b>1</b>	Itikadi	Mwanamke akiwa hedhini haruhusiwi kumkaribia fahali anayehusika katika <i>Shilembe</i> au <i>Mchezasili wa Mayo</i>	Huashiria bahati mbaya wakati wa upiganishaji fahali.

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

## **Jigambo la 1**

*Mumbulihitsi bulahi  
Muhulili lwambolanga  
Khuli lwanza khuhila makhuba  
Khuli manyanga nitsi Osama  
Wavananga tsinyanda  
Neshikulumi shisinjiye  
Nuli mumusayi ulisunda himbi*

Nisikilize vizuri  
Msikie ninavyosema  
Nitavyozungusha usukani  
Kwa vile ninavyojua kuwa mimi ni Osama  
Osama mvunja miamba  
Na rungu iliyosimama wima  
Ukiwa hedhini usikaribie  
**(Tafsiri: Mtafiti)**

## **4.5 Hitimisho**

Sura hii imejishughulisha na uchanganuzi wa majigambo kulingana na madhumni ya utafiti, maswali ya utafiti na mwongozo wa teneti za nadharia mbili zilizoteuliwa. Katika uchanganuzi wa lugha inayotumiwa majigambo katika jamii ya waisukha, imebainika kuwa, majigambo hutumiwa katika kudhihirisha na kudumisha ubabedume katika jamii hii. Vilevile, majigambo katika jamii hii hutumiwa kuwahimiza au kuwarai wanaume na wanawake kukubali hali jinsi ilivyo na kuendeleza falsafa, matarajio, mielekeo na itikadi za kijamii zinazojenga na kudumisha mfumo dume wa jamii. Ni katika msingi huu ambapo ubabedume wa jinsia ya kiume hujitokeza kama yenye uwezo, nguvu, uhuru, mamlaka na sifa nyingine za juu dhidi ya mwanamke. Kutokana na utafiti huu imedhihirika wazi kwamba mwanamume Mwisukha husawiriwa kama aliye na uwezo na mamlaka na vilevile mwenye uwezo wa kumiliki ardhi na mifugo hali hii humwezesha kuendeleza ruwaza mbalimbali za kiuwezo zinazompa hadhi ya juu na kumtofautisha kiuwezo na mwanamke hivyo kuchangia katika kuendeleza ubabedume katika jamii hii ya Waisukha.

## SURA YA TANO

### MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano ambapo kila mojawapo inashughulikia mambo maalum japo yana uhusiano wa moja kwa moja na kazi ya utafiti mzima. Utafiti umeshughulikia kila sura kwa kina na kiukamilifu kulingana na malengo ya utafiti. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti. Sura hii pia ilianguzia sababu ya uteuzi wa mada ya utafiti, upeo wa utafiti, umuhimu wa utafiti na maelezo ya nadharia mbili zilizouongoza utafiti. Aidha, ufafanuzi wa istilahi na akronimu umehitimisha sura ya kwanza.

Sura ya pili imeshughulikia uhakiki wa maandishi yaliyolenga mada ya utafiti na yaliyokuwa ya manufaa kwa utafiti huu. Udurusu wa maandishi haya ulihusishwa na suala na malengo ya utafiti. Katika sura ya tatu, njia na nyenzo za utafiti zilishughulikiwa. Sura hii ilijadili muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, majaribio ya vifaa vya kukusanya data, sampuli teuliwa, nyenzo na njia za kukusanya data na utaratibu wa kuchanganua data. Sura ya nne ilishughulikia uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo pamoja na mjadala. Haya yalifanywa kwa kujikita katika matumizi ya majedwali, maelezo na vielelezo. Mwishowe ni sura hii ya tano.



## 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu ulinuia kuyatimiza malengo matatu na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Namna nomino, vishazi na vitenzi vinadhihirisha ubabedume

Kwa mujibu wa Choge (1997), akiunga mkono mawazo ya Firth (1890-1969), anaeleza kuwa lugha imeshehenezwa na utamaduni wa wanajamii husika. Kwa hivyo, wanapendekeza kuwa uchunguzi wa kipengele chochote cha lugha fulani sharti ufanywe katika muktadha wa utamaduni unaosheheneza lugha inayochunguzwa. Choge alitafitia anthroponimu asilia za Kinandi kwa mtazamo wa Kisemantiki na matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa anthroponimu yoyote ile ya Kiafrika si alama tu ya kutambulisha na kutofautisha bali ni kioo chenye nguvu kinachoakisi tamaduni za daikronia na sinkronia ya wanajamii husika. Ndiposa, utafiti huu ulijikita katika kubainisha namna nomino, vishazi na vitenzi katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* ya Waisukha hudhihirisha ubabedume. Majina/animonimu kama vile Spana, tsinziga, bundi, Emini, 'Master key' na Mike Tyson zimetumika ili kudhihirisha sifa mbalimbali za ubabedume. Majina/animonimu hizi hazipatikani katika ombwe tupu bali katika muktadha wa jamii ya Waisukha hususan katika sherehe tajwa. Vishazi pia vilichunguzwa katika majigambo ya Waisukha kwa mfano 'Wanaenda haja ndogo' ili kuonyesha jinsi ubabedume unavyojitokeza. Aidha, vitenzi kama vile 'Ninasikia mnaniita' vilichunguzwa ili kuzitambua sifa hizo za ubabe. Utafiti ulibainisha kuwa majigambo yanayoghaniwa katika sherehe hizo za Waisukha si kama burudani tu bali yanasheheni vipengele vya lugha na vinavyosawiri ubabedume.

### **5.2.2 Tamathali za Usemi zinazosawiri Ubabedume kwa mtazamo wa kisemantiki**

Kulingana na Litosseliti (2010), usemi ni zaidi ya kipashio cha kiisimu, kwani husimba pia imani, itikadi na tajriba za kijamii ambazo huwaongoza wanajamii namna ya kufikiri, kusema, kutenda na hata kutagusana. Lugha inayotumiwa katika majigambo ya Waisukha katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* husheheni matumizi mbalimbali ya vipashio vya lugha ambavyo husimba tamathali nyingi za usemi na kujenga taswira kadhaa. Mawazo ya Litosseliti yanakaribiana na ya Simala (2012) anayeeleza kuwa utata wa dhana ya mafumbo huongezeka kwa ajili ya istilahi nyingi zinazohusiana na mafumbo kama vile taswira, uhuishi, takriri na jazanda. Kinachorejelewa hapa ni tamathali za usemi ambazo ni semi zinazohusiana na maana za kauli. Wataalamu hawa wanapendekeza kuwa maana katika tamathali za usemi zinahitaji kufasiriwa na kuchunguzwa kwa kina ili kueleweka kwa urahisi kama vile kwa mfano nadharia ya UCHAMAWADI inavyoelezea.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa tamathali za usemi mathalan majazi kama vile ‘master key’ katika jigambo la 6, tashbihi mfano ‘mwenye nguvu kama simba’, chuku kwa mfano ‘wavulana warefu futi tisa’ na jazanda kama vile ‘fahali kutoka katika ukoo wa Vayokha wanavyopendwa na ng’ombe wengi’ ili kuashiria ukware katika jigambo la 14. Tamathali hizi za usemi zinasheheni sifa mbalimbali za ubabedume katika majigambo ya Waisukha. Sifa za ubabe zilizobainika kupitia kwa tamathali hizi za usemi ni kama vile ukakamavu, uvumilivu, mwanamume kama aliye na mamlaka kuhusu masuala ya mapenzi, ya umiliki wa mali, jasiri, aliye na ukware, shujaa na sifa nyinginezo.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa wasanii wa majigambo ya Waisukha yanayoghaniwa wakati wa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* hutumia vipashio anuwai vya lugha kusimba tamathali za usemi zinazoakisi na kudumisha ubabedume katika jamii ya Waisukha. Kwa hivyo, kila kipengele cha tamathali ya usemi tulichokichunguza katika majigambo hayo kilisheheni ubabedume na hayo yote yaliwekwa wazi kwa kutumia mtazamo wa kisemantiki.

### **5.2.3 Nafasi ya lugha, Historia na Itikadi za Waisukha katika kujenga Ubabedume**

Kulingana na Habermas (1997), lugha hutumika kushamirisha na kuhalalisha ubabedume na pia mahusiano ya kiuwezo katika jamii. Kwa hivyo, utafiti huu umedhihirisha kuwa ubabedume hautokei tu bure bali hujengwa, hushamirishwa na kudumishwa kutegemea matarajio na mielekeo ya kiitikadi, historia na kitamaduni kuhusu wanajamii. Baadhi ya sifa ambazo husisitizwa kupitia kwa lugha ni uvumilivu, ukatili, ubabe na uwezo miongoni mwa sifa nyingine za kiubabe. Ni kutokana na matarajio hayo ya kijamii ambapo sifa hizi na nyingine husisitizwa (Mwagike 2005). Katika majigambo ya Waisukha, hali hii husimbwa kisanii kwa vipashio teule vya lugha. Lugha ni mfumo amilifu unaojenga na kuendeleza vitendo, mielekeo na mitazamo ya kijamii na kubainisha hali halisi ya kijamii (Matinde 2015). Utafiti huu uliweza kutalii na kuchunguza historia ya koo za Waisukha kwa sababu mazingira, historia na itikadi za jamii hii zina uamilifu wa kuendeleza na kudumisha hali halisi ya Waisukha kupitia kwa majigambo ya miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*.

Itikadi ni mfumo wa fikra na imani katika jamii. Mfumo huu hutawala hali na miktadha mbalimbali katika kipindi fulani cha kihistoria na huendelezwa na kundi fulani lenye

uwezo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, sanaa, dini na sayansi. Ni mchakato wa kijamii unaojenga na kubainisha mtazamo wa kiulimwengu wa jamii husika (Wanjala 2015). Kwa hivyo, itikadi katika jamii ya Waisukha ni dhana ambayo imetumika kuashiria uwepo wa nguvu mbalimbali za kijamii ambazo huyapatia majigambo uwezo wa kusawiri, kujenga, kuimarisha na kudumisha ubabedume kupitia kwa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Kwa vile majigambo ni aina ya usemi, hukitwa katika miktadha mahsusi kupitia kwa sherehe hizi za kupiganisha fahali na ndani ya miktadha hiyo, huzungumzia masuala ya kihistoria, kisiasa, kiuchumi, kifalsafa kitamaduni na hata kiitikadi.

Tasnifu hii imechunguza majigambo kumi na sita ya Waisukha na kubainisha uamilifu wake katika kujenga, kusawiri na kuendeleza itikadi za ubabedume katika jamii ya Waisukha. Matumizi ya vipashio mbalimbali vya lugha katika majigambo hayo yamedhihirisha jinsi fanani hutumia ubunifu na usanii wao kuendeleza fikra, mielekeo, mitazamo, misimamo na falsafa ya jamii ambayo hushamirishwa na utamaduni na mfumo wa jamii ya Waisukha. Hivyo basi, ubabedume katika jamii ya Waisukha umebainika kuwa ni zao la mazingira, historia na itikadi kupitia kwa lugha inayoteuliwa na kutumiwa na fanani watambaji na fanani wajigambi wakati wa miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo*. Utafiti huu umedhihirisha kuwa lugha ni nguzo muhimu ya utamaduni ambayo huongoza wanajamii jinsi ya kuwaza, kuamua na hata kutenda. Uchanganuzi wa majigambo kwa kutumia nadharia mbili za UCHAMAWADI na Uwezo-Uume uliwezesha uchanganuzi na ufafanuzi wa matini husika kwenye muktadha mpana na jamii ya Waisukha.

Dhana ya ubabedume huanza kuchipuka kuanzia utotoni wakati ambapo watoto hutambua jinsia yao. Watoto wa jinsia ya kiume hupewa majukumu yao katika jamii ambayo ni pamoja na kuchunga mifugo, kufyeka, kuwinda miongoni mwa majukumu mengine. Kwa upande mwingine watoto wa jinsia ya kike hupewa majukumu kama vile kuosha vyombo, kuteka maji mtoni, kuwalea watoto wadogo, kutenya kuni miongoni mwa mengine. Mambo hayo hujikita katika utamaduni wa jamii husika. Malezi ya wanajamii hujikita kwenye mfumo wa jamii ambao hujengwa na kushamirishwa kupitia kwa itikadi, imani na kanuni za jamii ambazo hubainisha mitazamo, falsafa, matarajio na mielekeo kuhusu hali mbalimbali za kijamii ikihusisha hali na nafasi ya jinsia ya kiume na kike. Ni katika muktadha huu ambapo ubabedume wa jinsia ya kiume hukuzwa na kuendelezwa, jambo ambalo humfanya mtoto wa kiume kuwa na uwezo, ushujaa, mamlaka, nguvu na ushari dhidi ya jinsia ya kike. Kwa upande mwingine hali hii ndiyo humfanya mtoto wa jinsia ya kike kusawiriwa kama aliyedunishwa na kudhalilishwa katika jamii. Mambo hayo yote yamejikita katika mafunzo ya kitamaduni kutegemea jamii husika.

Utafiti huu umebainisha wazi kuwa hali ya ubabedume hukuzwa na kuendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kulingana na mila na desturi za Waisukha zinazodhihirika kupitia kwa miviga ya sherehe ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha. Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa majigambo kama kipera cha Fasihi Simulizi kinachoweza kutumiwa kudhihirisha hali hii.

Majigambo yana majukumu mengi katika jamii na yanaweza kutumika katika kuweka wazi masuala ibuka kama vile magonjwa kama vile UKIMWI na namna ya kuyaepuka, matumizi ya mihadarati na matumizi ya utandawazi na kadhalika.

Wanajamii wanapaswa kutambua kuwa miviga katika jamii ni muhimu kwa vile hutumika kama jukwaa la kuendeleza mila, desturi na itikadi pamoja na utamaduni wa jamii husika. Miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* ni matukio katika jamii ya Waisukha ambayo hayafai kupuuzwa tu na wanajamii bali yanafaa kuchukuliwa kama jukwaa la kupitisha maarifa na ujuzi na pia kuelimisha vizazi baada ya vizazi kupitia kwa masimulizi ya fanani. Utafiti huu umedhihirisha wazi kuwa Fasihi Simulizi ni hai na tendi kwa vile mtafiti aliweza kutangamana na Waisukha katika miviga ya sherehe ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* na kushiriki katika sherehe hizo na vilevile kuwahoji wanajamii kuhusu miviga husika.

Uchunguzi huu umedhihirisha kuwa jamii ya Waisukha ina mgogoro baina ya ubabedume na mfumodume. Kwa hivyo, katika jamii ya mfumodume, Waisukha wakiwa mojawapo humwinua mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Mwanamke hupewa majukumu ya chini katika jamii ilhali mwanamume hupewa majukumu yenye nguvu, mamlaka na uwezo katika maswala yote ya kijamii.

Utafiti huu vilevile umebainisha namna taasubi za kiume zinavyompa mwanamume uwezo na mamlaka juu ya jinsia ya kike. Katika jamii hii, mwanamume Mwisukha amelimbikiziwa sifa zote za kishujaa kama vile mamlaka, uwezo, ujasiri, ukakamavu, uhodari miongoni mwa sifa nyingine huku mwanamke akijitokeza kama jinsia tegemezi,

anayetarajiwa kumhudumia na kumridhisha mwanamume. Isitoshe, mwanamume ndiye anayemiliki fahali wanaotumiwa wakati wakupiganishwa. Fahali hao ndio hubeba ushujaa husika kutegemea nasaba mbalimbali za Waisukha. Majigambo kama utanzu wa Fasihi Simulizi ya Waisukha huendeleza na kudumisha mila, itikadi, imani, desturi na utamaduni wa Waisukha. Hali hii ni ya kipekee kwa sababu itikadi ya Waisukha na uamilifu wa lugha ya majigambo hukuza na kuhalalisha tofauti za kiuwezo au kimamlaka baina ya wanajamii, hali ambayo huigawa jamii katika sehemu mbili; ya wenye uwezo – wanaume na wasio na uwezo - wanawake. Itikadi hizi ndizo hutumika katika kuendeleza mfumo wa jamii, mamlaka na madaraka katika jamii ya Waisukha. Katika muktadha huu ni wazi kuwa lugha ya majigambo ina uwezo wa kusababisha mgawanyiko na ukosefu wa usawa katika jamii hii.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu unatuongoza katika kutamatisha kwamba, sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* huchukuliwa tu kama burudani katika jamii ya Waisukha. Wengi wa wanajamii hawa huhudhuria sherehe hizi ili kuburudishwa na ngoma ya ‘Isukuti’ bila kutilia maanani matumizi ya lugha katika majigambo mbalimbali yanayoghaniwa na fanani wajigambi na fanani watambaji. Sherehe hizi zimekuwa sehemu ya utamaduni wa Waisukha ya kutimiza majukumu tofauti kama mazishi na burudani. Uchanganuzi wa data zilizopatikana nyanjani kuhusiana na suala la utafiti unatuelekeza katika kuhitimisha kuwa sherehe hizi hupendwa sana na wanajamii katika jamii hii wakiwemo wazee kwa vijana. Wengi wao hupitisha tu wakati bila kuzingatia umuhimu wake. Utafiti ulionyesha kwamba wasanii huteua vipashio mbalimbali vya lugha kama vile nomino, vishazi na

vitenzi vinavyosheheni ubabedume. Isitoshe, fanani watambaji na fanani wajigambi pia huteua tamathali mbalimbali za usemi kama vile jazanda, chuku, kejeli na taswira ili kusawiri ubabedume kama vile utafiti ulivyodhihirisha kwa mtazamo wa Kisemantiki. Majigambo hayo yalipokuwa yakighaniwa wakati wa miviga ya sherehe ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*, wengi wa washiriki walikuwa wakicheka tu na kucheza ‘isukuti.’ Hata hivyo, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa majigambo ya Waisukha katika miviga ya sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo* husheheni ubabedume kupitia kwa vipengele mbalimbali vya lugha.

#### **5.4 Mapendekezo**

Utafiti huu umebainisha kuwa Waisukha hawatili maanani majigambo yanayoghaniwa wakati wa sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa Mayo*. Majigambo hayo kupitia kwa vipengele vya lugha kama vile nomino, vishazi na vitenzi husheheni ubabedume. Sifa hizi za ubabe zimedhihirika kupitia kwa anthroponimu na animonimu mbalimbali kama vile Osama, Mike Tyson, chui, Emini miongoni mwa majina mengine. Vishazi kama vile ‘kwenda haja ndogo’ na vitenzi kama vile ‘kusimika’ vimechunguzwa na kubaini sifa za ubabedume. Aidha, tamathali za usemi kama vile tashbihi, majazi, jazanda na chuku zimechunguzwa katika majigambo hayo ili kudhihirisha ubabedume. Nafasi ya lugha, historia na itikadi pia imechunguzwa ili kubaini sifa za kiubabe katika jamii hii. Utafiti huu unapendekeza kuwa:

Majigambo yanayoghaniwa wakati wa sherehe hizi yasipuuzwe bali yazingatiwe kwa kudondolewa vipengele zaidi vya lugha na kurekodiwa ili yaweze kupitisha utamaduni na itikadi za Waisukha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hali hii itasaidia katika kuhifadhi



majigambo hayo kwa kutumia teknolojia ya kisasa na pia kueneza utamaduni huu ili ufahamike mtandaoni na kufaa taaluma za fasihi linganishi na isimu kijumla.

Utafiti huu pia unapendekeza kuwa tamathali nyingine za usemi zitafitiwe ili kuweka wazi sifa zaidi za ubabedume. Aidha, mbinu za uandishi zichunguzwe katika majigambo haya ya Waisukha.

Utafiti unapendekeza kuwa nafasi ya lugha katika majigambo izingatiwe kwa misingi ya isimu dayakronia, isimu sinkronia, utamaduni na itikadi mintaarafu ubabedume. Kwa msingi wa matokeo ya utafiti huu, watafiti waweze kuchanganua vipera vingine vya Fasihi Simulizi kwa kuangazia vipashio vingine vya lugha kwa mtazamo wa Uamali au kipashio kingine chochote kile cha kiisimu.

Utafiti umebainisha kuwa uwezo wa mwanamume umetamalaki katika mahusiano ya kijinsia. Kwa hivyo, mwanamume Mwisukha anasawiriwa kama aliye na mamlaka zaidi kuliko mwanamke. Hivyo basi, utafiti huu umedhihirisha ubabedume katika majigambo ya Waisukha.

Isitoshe, kuna haja ya wanajamii kuelimishwa namna utamaduni na itikadi za kijamii kutawala falsafa, mielekeo, matarajio na mitazamo yao ya kiulimwengu. Hali hii itawawezesha kubuni mikakati faafu ya kubadili baadhi ya imani, desturi na itikadi kwa kuangazia maendeleo ya kiulimwengu.

Utafiti huu unapendekeza kuwa sherehe za *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* katika jamii hii ya Waisukha zipewe mtazamo mpya ili ziweze kutumika kama kitega uchumi katika masuala ya kiakademia na wala si burudani tu.

### **5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi**

Utafiti huu unapendekeza tafiti zaidi zifuatazo zifanywe juu ya ubabedume:

